ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Pili - Tarehe 23 Januari, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kuweka mezani hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 6

Utaratibu wa Masheha Kuweka Kumbukumbu

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza**:-**
Kwa kuwa Masheha hufanya kazi zao kwa niaba ya Serikali. Na ili Masheha wafanye kazi zao vizuri wanatakiwa waweke kumbukumbu mbali mbali katika maeneo yao ili kuondoa utatanishi baina ya masheha na wananchi waliomo katika Shehia zao.

(a) Je, utaratibu huu wa kuweka kumbukumbu unafanyika.
(b) Kama unafanyika ni masheha wangapi wamefanya hivyo.
(c) Na kiasi gani utunzaji wa kumbukumbu hizo unakuwa salama wakati Ofisi za Masheha hao zimo majumbani mwao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kabla ya kumjibu swali lake Na. 6 Mhe. Mwakilishi, naomba kwanza nikubaliane na maelezo yake ya awali kuwa Masheha wanafanya kazi zao kwa niaba ya serikali kuu na kwamba wanapaswa kuwa na kumbukumbu mbali mbali za maeneo yao.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu wa kuweka kumbukumbu unafanyika na ndio zinazowawezesha Masheha kutekeleza majukumu yao. Aidha, ili kuoanisha mfumo wa taarifa, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Tume ya Mipango tumeandaa daftari la taarifa ambalo kila Sheha atatakiwa kulijaza na litaondoa kutofautiana kwa mfumo wa mtunzaji wa taarifa na baadae tarifa hizo zitawekwa katika mfumo wa kompyuta.

(b) Masheha wote wanaweka kumbukumbu katika Ofisi zao.

(c) Utunzaji wa kumbukumbu hizo uko salama na hatujawahi kupata taarifa ya kupotea kwa kumbukumbu licha ya kuwa baadhi ya Ofisi za Masheha ziko katika makaazi yao.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, ninapenda nimuulize Mhe. Waziri, pamoja na majibu yake mazuri, alisema kwamba wanaandaa daftari hilo lakini, je, nimuulize Mhe. Waziri, hili tunalitegemea kuanza mwaka gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, daftari hili tunategemea lianze mapema mwaka huu.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, kwa vile Masheha hawana ofisi, ofisi zao ni kwenye nyumba zao na hii inachangia kiasi kikubwa kutokuwa na ufanisi katika majukumu kutokuwa na usiri. Serikali ina mpango gani kuwatafutia ofisi Masheha ili waweze kufanya kazi zao kwa uadilifu, ufanisi na kuleta maendeleo katika nchi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Ni kweli hivi sasa Masheha ofisi zao baadhi yao zimo ndani ya

makaazi yao na kweli katika hili inaweza ikatokezea kutokuwepo na ufanisi na kutokuwepo na usiri pia.

Serikali mwaka ujao wa fedha inao mpango wa kuweza kuwawekea Masheha makarani angalau wawili wa kuweza kuwasaidia shughuli zao za kila siku, lakini vile vile, kuwa na uhakika wa taarifa zetu ambazo zinatunzwa katika Shehia.

Katika mpango huo pia tunafikiria kutafuta maeneo maalum kwa ajili ya ofisi za Masheha.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika katika Baraza lako tukufu kwa hali ya usalama na afya nzuri.

Mhe. Spika, katika jibu mama la Mhe. Waziri, ameeleza kwa ufasaha, lakini je,atakubaliana na mimi kwamba ni vyema kwanza waka-*survey*, ni Masheha wangapi ambao hawana ofisi na ni sehemu gani ambazo hizo ofisi zitajengwa ili kutokuwapa shida wananchi ambao wanataka kukamilisha shughuli zao. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Ninakubaliana naye kwamba kufanya *survey* ni jambo la msingi na huu utaratibu ambao tunakuna nao tumefanya *survey* kwanza tukajua matatizo yaliopo na ndio maana tunakuja na huo utaratibu wa kuwa na daftari, tunakuja na utaratibu wa kuajiri makarani angalau wawili katika kila Sheha na vile vile, kuwatafutiwa maeneo kwa ajili ya kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Nam. 10

Hatua za Kudhibiti Wigo wa Tamaduni za Magharibi

Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Aliuliza:-
Utamaduni wa kuiga tamaduni za Kimagharibi (*Western Culture*) umeanza kuchukua nafasi kubwa hapa visiwani kwetu na kuathiri mila, desturi na silka za Wazanzibari jambo ambalo halikuwepo hapo zamani.

(a) Je, Serikali inaliangaliaje jambo hili na imechukua hatua gani za makusudi kuona kwamba vijana ambao ndio wengi wao wameathirika na suala hili la kuiga tamaduni za magharibi, wanaenzi na kuendeleza mila, desturi na silka za Mzanzibari.

(b) Ni kwa namna gani suala la kuiga tamaduni za magaharibi linachangia katika kuporomoka kwa maadili kwa vijana wetu wa Kizanzibari.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu **:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 10 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli suala la kuiga tamaduni za kigeni za Magharibi na Mashariki zimechukua nafasi hapa Zanzibar na kama nchi kadhaa zilizo duniani tamaduni hizi zinaathiri au kuporomoa mila, desturi na silka zao. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali katika kukabiliana na hali hiyo. Miongoni mwa hatua hiyo ni kuwa na Wizara pamoja Kamisheni ya ya Utamaduni na Michezo imekuwa ikitoa miongozo na taaluma juu ya umuhimu wa kuendeleza utamaduni wetu. Kushajiisha kuundwa vikundi vya utamaduni pamoja na kuweka sheria za kuenzi mila, silka na maadili yetu. Hata hivyo, kwa kuwa suala la utamaduni linahusiana moja kwa moja na jamii, wahusika wakubwa wakuendeleza na kuenzi utamaduni haliishii kwa serikali peke yake. Ni suala linalotuhusu sote kwa pamoja hasa viongozi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wazazi, viongozi wa dini na jamii pia ni sehemu ya kulishughulikia hili.

b) Mhe. Spika**,** dunia hivi sasa ni sawa na kijiji. Hivyo, kuporomoka kwa maadili ni kutokana na hali ya utandawazi ni jambo ambao tulitegemee, jambo la muhimu ni kukinga kuporomoka maadili yetu ni kuhimiza vijana na watoto wetu kujiunga katika mafunzo ya dini na kuwajengea mazingira ya kufuata silka na tamaduni zetu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba moja ya sababu zinazopelekea kuporomoka kwa maadili kwa vijana wetu ni ongezeko la utumiaji wa mtandao (utandawazi). Naomba nimuulize Mhe. Waziri, kwamba serikali inajipangaje kuona kwamba huu utandawazi unadhibitiwa kwa kiasi fulani ili vijana wetu wasiwe na *access* ya moja kwa moja kuangalia haya mambo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, suala la utandawazi ni suala ambalo kiulimwengu hivi sasa ni sawa na silaha.

Silaha inategemea utaitumia vipi, ukiitumia vibaya itaathiri sana na ukiitumia vizuri inaweza kukinga vizuri.

Kwa hivyo, suala la msingi ni kwamba hatuwezi kuacha kutumia fursa zilizomo katika utandawazi kwa sababu pia zina fursa nyingi za kimaendeleo. La msingi ni kwamba kama nilivyosema awali suala la malezi ya watoto ndio jambo la msingi sana. Kwa hivyo, sote kama wazazi na viongozi, suala hili ni muhimu ili kujua vijana wetu wanaitumiaje fursa hii ili isiweze kuleta madhara kwa silka na utamaduni wa nchi yetu.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu swali lake, alisema kwamba suala la utamaduni na maadili ni suala la kijamii ambalo linahusu wazazi pamoja na watu wengine katika jamii. Lakini Mhe. Spika, mambo mengi sana yanahusu jamii, lakini kunakuwa na taratibu za kisheria hapa katika Baraza hili tunazitunga. Kwa kuwa suala la mavazi ni suala la kitamaduni na kimaadili. Haoni kuna haja sasa ya kuweka taratibu ya kuonesha namna gani watu wavae ili tuwanusuru vijana wetu kuvaa nusu uchi kwa lugha nyengine. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ni kweli Mhe. Spika, masuala haya yanahitaji taratibu za kisheria. Bahati nzuri sheria tunayo ni ya zamani kidogo.

Ninachokubaliana na Mhe. Mwakilishi, ni kwamba sheria ile inahitaji mapitio. Kwa hivyo, wizara itashirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako hili ili kuiangalia sheria ile na tutachukua maoni ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu ili sheria ile ambayo ni ya zamani kidogo inahitaji mapitio kidogo na vipi ambavyo inaweza kurekebishwa ili iende sambamba na mila, silka na utamaduni wa nchi yetu.

Nam. 46

Urasimu katika Kusajili Jumuiya Zisizo za Kiserikali (*NGO's*)

Mhe. Asha Abdu Haji-Aliuliza**:-**

Serikali pamoja na Jumuiya za Kimataifa zinaamini au zinapendelea zaidi kutoa misaada yao kwa vikundi au Jumuiya za *NGO's* ambazo tayari zimeshasajiliwa na kuwa na hati ya usajili.

(a) Pamoja na sababu hiyo taasisi ya serikali ambayo imepewa dhamana ya kusajili vikundi kama hivyo imekuwa ngumu na urasimu katika kuvisajili vikundi hivyo licha ya kuwa vimekamilisha masharti ya usajili. Je, ni kweli serikali ina nia njema katika uanzishwaji wa vikundi vya aina hiyo.

(b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea taasisi husika kuwa na uzito wa kusajili vikundi vya aina hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, ninapenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 46 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Jumuiya za kiraia ni taasisi binafsi za hiyari zinazoanzishwa kwa lengo la kuiwezesha jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo hasa katika maeneo ambayo serikali haijayafikia kikamilifu. Kwa Zanzibar taasisi iliyopewa mamlaka Kisheria ya kuzisajili taasisi za kiraia ni Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar (*BPRA*) ambayo kabla ilikuwa ni Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, Sheria Nam. 6 ya mwaka 1995 ndiyo inayotumika kuongoza usajili pamoja na kuweka masharti na utaratibu wa usajili, usimamizi na uendeshaji wa Jumuiya za kiraia. Ili kuweza kusajiliwa Jumuiya za kiraia, hutakiwa kukamilisha taratibu mbali mbali ikiwemo ujazaji wa fomu ya usajili, kuandaa barua ya maombi ya usajili pamoja na utayarishaji wa Katiba itakayoongoza mwenendo wa taasisi husika mara baada ya kusajiliwa.

Mhe. Spika, mara baada ya kuwasilishwa kwa vitu hivyo Afisi husika hufanya upembuzi kwa kina kwa kuzipitia nyaraka hizo zilizowasilishwa na Jumuiya husika ili kuhakikisha ukamilifu wake, kuzitoa makosa pale inapobidi pamoja na kutoa maelekezo kwa wanajumuiya juu ya uboreshaji wa nyaraka hizo hadi pale zitakapoonekana zimekamilika na kukidhi vigezo vya usajili kwa mujibu wa sheria, muundo na malengo ya jumuiya hiyo.

Mara nyingi jumuiya za kiraia huwasilisha nyaraka hizo zikiwa na makosa mbali mbali kutokana na ukweli kwamba wengi wa watayarishaji wa nyaraka hizo kutokuwa na utaalamu wa kuzitayarisha. Hata hivyo, Afisi kupitia maafisa wake huzipitia na kutoa maelekezo pamoja na kuwashauri wanajumuiya juu ya njia bora za kuziandaa nyaraka hizo.

Aidha, hutakiwa wajaziwe na maafisa wetu, lakini huwa hawataki pengine kwa sababu tu hawataki kusema ukweli katika kujaza fomu hizo. Upatikanaji

wa nyaraka hizi hufanywa si kwa lengo la kukwamisha usajili kwa jumuiya hizo, bali kujenga na kukuza demokrasia na uwajibikaji ndani ya jumuiya na kulinda usalama mila na desturi za nchi yetu pamoja kuzijengea mazingira mazuri kiuendeshaji taasisi zenyewe binafsi kwa mujibu wa sheria walizojiwekea, mara nyingi kumekuwa na migogoro isiyoisha na mingine kusababisha hata kuhatarisha uhai wa jumuiya zenyewe kutokana kukosekana maandalizi mazuri ama ya Katiba zao au nyaraka nyengine zinazohusiana na usajili.

Mhe. Spika, vile vile, uchelewaji wa wanajumuiya wenyewe kuwasilisha marejesho ya marekebisho waliopewa na maafisa wetu, hupelekea kuwasababishia wao wenyewe binafsi kujicheleweshea kupata usajili huo. Kwa maana hiyo Mhe. Spika, serikali ina nia njema sana ya kusaidia vikundi hivyo kwa kuhakikisha kuwa vinasajiliwa kwa mujibu wa sheria na kwamba mizozo inayoweza kutokea inakingwa ili isitokee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika kutekeleza ule mpango wa SMZ wa kuongeza kipato na kupunguza umaskini kwa wananchi (MKUZA) katika Jimbo langu la Wawi nimetekeleza mpango huu kwa kuanzisha vikundi kadhaa vya akinamama, vikiwemo kilimo cha njugu na tungule katika eneo la Umangani, kikundi cha akinamama cha ubanjaji kokoto Kisiwani na kikundi cha uvuvi wa pweza cha akinamama kilichoopo Matungu katika Jimbo langu la Wawi.

Na kwa kuwa masharti kadhaa tumeyatimiza ikiwemo na pamoja na kufungua akaunti katika benki, lakini huu ni mwaka wa pili ninahangaikia usajili wa vikundi hivyo, lakini hadi hii leo, hata jibu hatujapata. Je, kuendelea kuweka urasimu kwa vikundi hasa vya akinamama kuvikatalia usajili katika kipindi cha miaka miwili kamili, si kwenda kinyume na agizo la SMZ la kuwataka wananchi wapunguze umaskini na kujiongezea kipato.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Ninashukuru kwa swali zuri la Mhe. Mwakilishi, inaonesha Mhe. Mwakilishi, hawatakii mema hivi vikundi vyake kwa sababu ikiwa ni mwaka wa pili hawajasajiliwa Afisi ya Msajili anaijua, Waziri anayehusika anamjua mpaka anasema leo. Mimi ninafikiri ni matatizo.

Mimi ninafikiri yanapotokea kama haya, ni vizuri kushirikiana na Waziri ukamwambia matatizo yako ili na yeye akaweza kukusaidia. Lakini ninachosema Mhe. Spika, ni kwamba fomu zinazojazwa zina matatizo na

tumeshapata matatizo mengi watu wanataka kupigana kutokana na *shareholder* na mambo mengine yote hayo.
Sasa zinapokuja kwetu lazima tuzipitie kwa ukamilifu sana. Sasa ikiwa kuna matatizo ya vikundi kwamba bado havijasaliwa kutokana na utaratibu huo, mimi naomba aniletee haraka tutizame kuna makosa gani na tutamwambia. Lakini Waheshimiwa Wajumbe, musikae miaka miwili mitatu halafu mukaja mukauliza maswali hapa. Mhe. Spika, ninashukuru

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mara kadhaa serikali imekuwa ikiahidi kupitia Kamati ya Katiba na Sheria kufanya utafiti wa kufuta *NGO's* ambazo zilisajiliwa, lakini hazifanyi kazi kama zilivyosajiliwa, lakini pia zipo ambazo hazina *permanent offices* wala uongozi mzima wa *NGO's* hizo.
Je, utafiti ule umefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ninapenda kusema kuwa kazi hiyo tumeifanya, ni kazi kubwa sana. Hivi sasa tunayo majina ya vikundi vingi (*NGO's*) ambavyo utaona hazina ofisi, pengine Katiba zao zina matatizo, kuna mambo mengine yana matatizo.

Sasa baada ya kufika kwangu tunajaribu kuziita moja moja kutaka kujua uhakika zaidi ili tunapofuta tuwe tunafuta kwa uhakika, lakini kazi hiyo imeshafanywa na tunaendelea kuifanya.

Nam. 21

Usalama wa Afya kwa Nyama Zinazouzwa Kwenye Mabucha

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza**:-**
Mhe. Spika, kabla ya swali langu Nam. 21 kujibiwa naomba kidogo nifanye marekebisho madogo kama ifuatavyo:
Ninasema kwamba kwa kuwa maduka ya kuuzia nyama zitokanazo na mifugo liongezwe neno " nyama litokanazo na mifugo" hapo. Baada ya marekebisho hayo Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 21 sasa lijibiwe.

Kwa kuwa maduka ya kuuzia nyama (*butchers*) hapa Unguja na Pemba hususan Wilaya ya Chake Chake hununua aidha ng'ombe wakiwa hai au nyama ikiwa tayari imechinjwa.

(a) Je, mamlaka zinazohusika ni kwa kiasi gani hujiridhisha kwamba '*butcher'* hizo zinauza nyama zinazofaa kuliwa katika jamii ya

Wazanzibari na ni kwa kiasi gani zimechinjwa katika mazingira salama kwa afya ya binadamu.

(b) Ni kwa kiasi gani mamlaka hizo zimejiridhisha kwamba nyama hizo sio za wizi.

(c) Ni lini serikali itaziagiza "*butchers*" hizo ziuze mifugo na sio nyama zilizochinjwa za mifugo hiyo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, unamshughulisha Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:-**
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 21 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, masahihisho yameshafanyika wakati mimi nimeshajibu.Kwa hivyo, kama nitakwenda kinyume na matarajio yake ilikuwa asahihishe kabla.

a) Manispaa na Halmashauri ndizo zenye mamlaka ya utoaji wa leseni kwa shughuli za uchinjaji wa nyama na zinazohusu ma-*butchers* katika maeneo yao. Kwa upande wa Wizara ya Afya, chombo kinachohusika ni Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ndio chenye mamlaka ya kuangalia maeneo na majengo yanayotumika kuchinjia au kuuzia nyama kwa kuyakagua kupitia maafisa mifugo na maafisa wa afya wa wilaya.

Halmashauri na Mabaraza ya Miji ikiwemo Chake Chake. Kama sehemu hizo hazikukidhi sifa zinazotakiwa zinafungwa hadi pale matengenezo au marekebisho yatakapofanyika na ndipo yatakaporuhusiwa kufanya kazi.

Bodi pia huangalia ubora na usalama wa chakula ikiwemo nyama ya mifugo. Nyama hukaguliwa ili kuangalia muonekano wa afya yake kabla hajachinjwa na baada ya kuchinjwa nyama hukaguliwa kama hakuna magonjwa kama vile kimeta na sokota ambayo hayakumuathiri mnyama huyo sehemu za ndani.Na ili kuthibitisha kwamba ukaguzi huo umefanyika alama maalum huekwa baada ya kuchinjwa ili kuonesha kuwa nyama hiyo ipo salama na haina madhara kwa mlaji.

Aidha uingizwaji wa mifugo kutoka nje ya nchi, unadhibitiwa chini ya usimamizi wa Idara ya Mifugo.

b) Suala la kujiridhisha kwamba mnyama au nyama ya mifugo sio ya wizi, Wizara ya Afya sio wahusika wa hilo.

c) *Butcher* huuza nyama si mifugo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, mdogo wangu hapo *Dr* Sira Ubwa Mamboya, naomba niulize swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa vigezo alivyovitumia na taratibu ambazo alisema zinachukuliwa na serikali, mara nyingi hutumia katika maeneo ya mijini.Lakini *butchers* zetu zinazouza nyama inayotokana na mifugo katika maeneo ya vijijini hazikuwahi taratibu hizo na kwa kuwa walaji wa nyama hawana uwezo wa kutambua ni aina gani ya nyama hii wanayokula au nyama hii imeibiwa au haikuibiwa. Kwa kuwa watu wengi hawana vipimo hivyo.

Je, ni lini serikali itatowa uwezo kwa *butchers* zetu hizi za vijijini, kuweza kutambua kwamba nyama hii inayoliwa sio ya wale wanyama wengine kama punda, nyumbu na wengineo, lakini iwe ni nyama ambayo inastahiki kuliwa kama vile nyama ya mbuzi na ya ng'ombe. Je, ni lini serikali itaziwezesha *butchers* zetu za vijijini, kuweza kutambua kwamba nyama zinazoliwa katika maeneo ya vijijini ni halali kwa kuliwa na sio zile ambazo hazistahiki kuliwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba watu wa afya hawako katika sehemu zote, lakini kila wilaya kuna mabwana afya na kuna mabwana mifugo. Tegemeo letu ni kwamba wafanyakazi hao wanajua sehemu gani wana ma-*butchers*. Kwa hivyo, ni tegemeo langu kwamba yamerikodiwa na wilaya inafahamu hivyo. Kama tusingekuwa na wafanyakazi wa kutosha, sisi Wizara ya Afya, kila Kituo cha Afya kilipo, basi panatakiwa awepo bwana afya, lakini kutokana na upungufu wa wafanyakazi hao, ndio maana unakuta angalau kwenye wilaya kuna mfanyakazi huyo.

Mhe. Spika, katika ugawaji wa wafanyakazi wa mwaka huu, tumepata mabwana afya na tumejaribu kuwagawa kwa mujibu wa nafasi zilizokuwepo, lakini hatukujaza zote. Kidogo kidogo tutaongeza mpaka pale vituo vitakapokamilika. Sasa mimi nafikiri watu wa Halmashauri na watu wa Mabaraza ya Mji, kwa kuwa wao ndio wenye dhamana hiyo waangalie, basi uwezekano wa kujua *butchers* zao zilipo na kuweka utaratibu wa kuona jinsi gani watawafuatilia.

Wakiona hawawezi kuwafuatilia, basi wasifunguwe *butchers* nyingi ambazo watashindwa kuzifanyia kazi. Pafanyike pale ambapo patakuwa na uhakika na nyama yoyote ya mnyama, ikishachinjwa ikichekiwa inatiwa alama, yaani

inapigwa muhuri maalum. Kwa hivyo, tuwaombe wananchi wetu wanapokwenda kununua nyama kabla hawajainunua hiyo nyama, basi waambie wale wenye ma-*butchers*, wawaoneshe alama ya ubora uliofanywa ikabadikwa juu yake ili waweze kupata nyama iliyohalali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Saleh Nassor Juma, walizungumzia ma-*butchers* yaani ni sehemu ya kuuzia nyama, lakini wananchi wetu vijijini wakati wa kiangazi na mvua kali, wanyama kama ng'ombe na mbuzi huanguka na wananchi huchukua hatua za kuwachinja na hatimaye huwaita wataalamu wa afya kuja kukagua nyama za wanyama hawa waliochinjwa.

Wanapofika wataalamu wa afya Mhe. Spika, huwa wana kisu na hukata sehemu ya nyama ile ya mnyama aliyechinjwa na kuwaambia wananchi kwamba mnyama huyu ni halali na anafaa kuliwa. Wakati mwengine huwaambia wananchi kwa hivi nyama ilivyo ni tamu sana.

(a) Je, ni vigezo gani vya wataalamu wetu ambavyo hutumia kuwaambia wananchi kuwa hii nyama inafaa kuliwa na ni tamu sana.

(b) Kwa sababu wataalamu hawa huwa wanakuja na sehemu nyeti za wanyama hao huchukuliwa na wataalamu. Kama maini, figo na mapaja ya wanyama hao, ndio fani hasa ya kitaalamu kwamba kwa nini sehemu zile nyeti za wanyama hao huchukuliwa na wataalamu wa afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, linapotokezea suala kama hilo la mnyama kuanguka na kuchinjwa, bila shaka mnyama atakuwa na tatizo. Maana mnyama mzima haanguki tu, atatembea na kufanya shughuli zake kama kawaida. Lakini anapoanguka ina maana mnyama tayari ana tatizo na pengine labda ana ugonjwa.

Sasa kinachotokea anapokuja bwana afya anakata hizo sehemu anazoziona yeye tamu kwa ladha yake, ambapo mimi hilo silijui. Lakini kinachotizamwa pale ni maradhi gani yamemuathiri mnyama yule na maradhi mawili makubwa ambayo huwa yanawaathiri wanyama ni hayo mawili ambayo nimeyataja.

Mnyama yoyote hata binadamu maradhi yake yamo katika sehemu mbili kubwa ambayo ni maini na mafigo, kwa sababu mule ndimo yanamochujwa

maradhi.Pia, kwenye matezi na hata kwenye bandama ni sehemu ambayo hufanya maradhi. Kwa hivyo, kama kaangalia nyama kwenye misuli kaiona ni nzuri, basi nyama ya misuli inaweza kuliwa. Lakini mafigo, maini na bandama, hayo yanahitaji uchunguzi wa ziada. Sasa kama yeye kachukuwa kaenda kula huko, hiyo tena ni hiyari yake, lakini hicho ndicho kinachotakiwa kwenda kuchunguzwa, kwa sababu mule ndimo chujio la maradhi yalipo. Kwa hivyo, sijui kama wana dhamira nyengine zaidi ya hiyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu yake mazuri sana.

Mhe. Spika, zamani tulikuwa na machinjio pale Gulioni na nyama zote zilikuwa zikitoka shamba zinaishia pale kwa ukaguzi uliokuwa ni wa kitaalamu kabisa. Mhe. Naibu Waziri. hivi sasa tuna machinjio yako Kisakasaka na hayapo katika hali ya kitaalamu kutokana na hali halisi ilivyo. Kabla haijakaguliwa hiyo nyama yenyewe, basi hilo chinjio lenyewe linaweza kuleta hatari kutokana na kutokuwa na usafi.

Je, Mhe. Naibu Waziri. mna mpango gani wizara yenu ya kuweka chinjio lililokuwa zuri na wataalamu wa kutosha kabisa ili wananchi wasije kuathirika kwa kula hizo nyama mbovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, naomba kuongeza jibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli zamani palikuwa ma machinjio pale Gulioni, lakini sasa imepitwa na wakati kuweka chinjio ndani ya mji. Hivi sasa tunalo chinjio la Kisakasaka na tayari tuna mchoro mzuri na mkubwa ambao tunatarajia kujenga chinjio la kisasa lenye kuchinjia ng'ombe, kuku pamoja na vyenginevyo ambavyo vitakuwepo.

Mhe. Spika, tuliweka kule kwa sababu ya kuweka mbali na wananchi ili hata yakitokea maradhi makubwa kama ya vimeta na mengineyo, basi kule tunaweza tukayahifadhi kwa umbali wake, sio kuleta karibu na wananchi ambapo yanaweza kuleta madhara.

Nam. 2

Vijana Wanaopata Mafunzo ya Uchimbaji Mafuta na Gesi

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi-Aliuliza:-

Suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ni jambo ambalo linahitaji uelewa kwa wananchi na kwa kuwa hivi sasa wapo vijana wetu ambao tayari wamekwenda kupata utaalamu wa uchimbaji wa mafuta hayo na kwa kuwa hivi sasa yameibuka makampuni mengi ya kigeni kuanza kuwalaghai vijana ambao wanachukua taaluma hiyo.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na suala hilo la vijana wetu hao ambao tutawategemea kuja kutoa taaluma hiyo kwa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

(b) Je, Kuna taarifa gani ambazo serikali imezipata tokea kuondoka kwa vijana hao.

(c) Je, Serikali ina mpango gani kwa vijana hao wa kuwawezesha baada ya kurudi ili wasije kulaghaiwa na makampuni binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati-Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 2 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa tunao vijana wetu katika vyuo mbali mbali nchini na nje ya nchi, ambao wanajifunza masomo ya mafuta na gesi. Vile vile, napenda kukiri kuwa zipo tetesi za Makampuni ya Mafuta, kuanza kuwasogelea vijana hawa ili kutaka kuwatumia kwa baadae.

   Mhe. Spika, katika kukabiliana na hilo, wizara yangu imeanza kuchukua jitihada maalum ya kuwafungulia mawasiliano vijana hao, ili kuweza kuonana nao ana kwa ana na kuwasiliana na baadhi ya vyuo ambavyo wanasoma vijana hao. Vile vile, na kuwaweka karibu na kuwasikiliza vijana hao, pamoja na kuwasaidia.

   Mhe. Spika, wizara yangu pia inachukua jitihada za kuwasiliana na Bodi ya Mikopo katika kuwafuatilia vijana waliokuwepo nje ya nchi, pamoja na kuwasikiliza matatizo yao. Hii itawafanya vijana hao kujisikia vizuri na kuendelea na masomo yao katika hali nzuri.

Mhe. Spika, zipo taarifa ambazo zimekusanywa kutoka kwa vijana hao, ikiwemo idadi na muda wa masomo, aina ya masomo wanayosoma pamoja na matatizo yanayowakabili.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, ni habari njema na kwa vile sasa hivi tunaelekea katika uchumi wa mafuta na gesi Zanzibar. Ni habari njema kwamba kuna vijana wa Kizanzibari ambao wanachukua masomo katika fani mbali mbali kuhusiana na suala zima la mafuta na gesi.

Je, serikali ina taarifa kuhusu hao vijana ni wangapi, wako wapi na wanasomea fani gani katika fani hii ya mafuta na gesi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, serikali kwa kupitia wizara yangu inaelewa na kwa sasa hivi tunao wanafunzi 29 ambao wako katika nchi mbali mbali, ikiwemo vyuo vya hapa nchini pamoja na vyuo vilivyokuwepo nje ya nchi.

Mhe. Spika, wanafunzi 11 wako katika chuo cha Dodoma, wanafunzi 12 wako chuo cha Dar es Salaam, wanafunzi 2 wako China, wanafunzi 2 wako Russia, mwanafunzi 1 yuko Sudan na mwanafunzi 1 Uingereza.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, tunachotaka kukijua Wazanzibari ni kwamba vijana hawa wanachukua fani gani katika sekta hii ya mafuta.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa faida ya Mhe. Mjumbe, na faida ya waliopo vyuoni. Mhe. Spika, fani kubwa za mafuta ni tatu, zipo na nyengine ndogo ndogo, lakini katika mafuta wanafunzi wanachukua fani za *geology*, *geophysics*, *geochemistry* pamoja na fani nyengine ndogo ndogo, hizo ndio fani za kuchimba mafuta.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niipongeze serikali kwa jitihada ambayo inachukua kusomesha vijana wetu kwa fani mbali mbali. Kwa kuwa Mhe. Waziri, ametujibu kwa ufasaha.

Je, hatuoni kwamba ni vyema tukaweka mikataba kwa masomo maalum ambayo kwa kwetu sisi huchukuliwa hawa vijana wetu na kudhibitiwa kufanya kazi wakati serikali imepata tabu kuwasomesha, kama miaka 7 au 8. Hatuoni kuwa kuna haja ya kuwekeana mikataba ili wakimaliza mafunzo yale kurudi makwao?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Mwakilishi, ni ushauri mmoja mzuri, serikali itauchukua ushauri huu na itaufanyia kazi. Lakini pamoja na hayo, mikakati ya serikali tayari imeshawekwa, ikiwemo kuwafuatilia na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanaosomeshwa na serikali, kwa lengo maalum la kuisaidia serikali, basi watabaki ndani ya serikali na wataifanyia kazi serikali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, amekiri kwamba tunao vijana wetu Wazanzibari wanaosoma katika vyuo mbali mbali nje ya nchi, na kwa kuwa fani hii ya jiolojia na mambo ya *extravations of oil* ni fani ngumu sana na ghali. Kwa kuwa sisi hapa katika nchi yetu tunacho Chuo Kikuu cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SUZA). Kwa kuwa tunao wataalamu wazuri pale SUZA wa ndani ya nchi, lakini fani hizi hazipatikani. Kwa sababu kuna uwezekano mkubwa wa nchi hii kuwa na mafuta pamoja na gesi.

Je, ni lini chuo chetu hiki cha SUZA Mhe. Spika, nacho kitaanzisha fani hii ya mambo ya jiolojia na mambo ya uchimbaji wa mafuta, kusudi kuongeza idadi ya wataalamu katika nchi yetu, ili tutakapoanza uchimbaji wa mafuta tuweze kuyafanyia kazi vizuri mno.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, utaratibu huo wa kutaka kuanzisha masomo haya katika vyuo vyetu upo na hivi sasa kwa kushirikiana na Norway tayari SUZA wameanza kupata huo mwelekeo wa kutaka kuanzisha fani hizo za mafuta na yupo mtaalamu mmoja anasaidia katika kufanya utaratibu wa kuanzisha masomo hayo ya mafuta na gesi.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Hakimiliki ya Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea Zanzibar ya 2014

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea, lakini kwa mnasaba wa yale tuliyokubaliana jana, kwamba leo moja kwa moja tunakwenda upande wa majumuisho na kwa kuanzia naomba nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri, wa Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kuweza kukutana katika Baraza letu hili tukufu, hali ya kuwa na afya na uzima.

Mhe. Spika, shukrani za pili zikuendee wewe kwa kukupa uwezo Mwenyezi Mungu kuweza kutuongoza sisi watu wazima kwa hali ya busara na hekima. Pia, niwashukuru wajumbe wote ambao waliochangia mswada huu, ni imani yangu walichangia mswada huu kwa njia ya kuufanya kuwa bora.

Mhe. Spika, vile vile, nisiwe mkosefu wa fadhila niishukuru Kamati ya Fedha na Biashara kwa kazi ngumu waliyoifanya katika mswada wetu huu. Baada ya shukrani hizo, sasa naomba Mhe. Spika, uniruhusu nitowe ufafanuzi wa baadhi ya hoja za wajumbe kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza napenda kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe zinazohusu idadi ya wajumbe wanawake kuwa angalau 3. Katika kifungu cha 9(2) kina maanisha kuwa wajumbe hao wanawake watatoka miongoni mwa wajumbe ambapo sifa zao zitatajwa katika (a) mpaka (i), hili halitazuwia kuwa wajumbe wote wanawake katika Kamati ya Ushauri.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Waziri wa Fedha kupewa mamlaka ya kuanzisha mfuko wa Hakimiliki ya Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea. Suala hili halina utata wowote na limeelezwa wazi wazi katika sheria za fedha, yaani *Public Finance Act* Namba *12 2005* katika kifungu cha 11.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Abdalla Mohammed Ali kuwa cheti ambacho kitatolewa chini ya sheria hii, kitatambulika kitaifa na kimataifa kwa nchi zote ambazo ni wanachama kwa Shirika la *UPOV*.

Kwa mujibu wa mkataba wa *UPOV* taarifa na haki ama vyeti vyote vya hakimiliki vya wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kutoka nchi wanachama, ni lazima zipelekwe katika Makao Makuu ya Shirika hilo, ili kutoa taarifa kwa wanachama wote. Pia, cheti ama haki hii itamuwezesha mgunduzi huyu kuweza kuomba ulinzi wa mbegu kwa nchi wanachama wa shirika hilo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la hakimiliki kwa mbegu za zamani. Mswada wa sheria hii unatoa haki kwa wagunduzi wapya na wale wa karibuni, ambao wataomba kupatiwa haki hiyo ndani ya miezi 12, tokea tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii kama inavyoelezwa katika kifungu cha 54 cha sheria hii.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kuwa iwapo mbegu itabadilika na kupoteza sifa yake kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kuwa sheria imeliona suala hilo. Hivyo, katika kifungu cha 38, kimetoa uwezo kwa mrajisi kufuta hakimiliki za wagunduzi kutokana na mbegu kupoteza sifa iliyokuwa nayo wakati iliposajiliwa.

Mhe. Spika, sasa napenda kujibu hoja ya Mhe. Salim Abdalla Hamad, kuhusu uwezo wa wizara katika kugundua na kutoa majina na ya kukubalika kisayansi kwa mimea na aina nyengine za viumbe walioko Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mjumbe,, kwamba wizara inayo wataalamu wenye uwezo wa kufanya ugunduzi na kutoa majina yanayokubalika. Aidha, kutoa mfano wataalamu wetu katika mwaka 2006 waligundua chura katika Msitu wa Jozani, ambaye amepewa jina la Kasina Jozani. Vile vile, katika mwaka 2009 wataalamu wetu waligundua popo katika Msitu wa Ngezi na akapewa jina la Mopsi Bakarii.

Aidha, taasisi yetu ya utafiti wa kilimo Kizimbani, imefanya utafiti na kugundua aina 4 za mbegu za muhogo ambazo zinakubalika kimataifa, ambazo zimepewa majina ya Kizimbani, Mahonda, Machui na Kama.

Vile vile, tunahifadhi mbegu zetu za asili za mpunga, viazi vitamu, viazi vikuu na migomba na ambazo zinatambulika ndani ya nchi na katika taasisi za utafiti ndani ya Afrika ya Mashariki ya Kati.

Mhe. Spika, pia kuna wajumbe walisisitiza sana juu ya utoaji wa elimu, wajumbe hao walikuwa ni Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Mhe. Suleiman Hemed Khamis. Suala hili tunalikubali na tunalichukua, tutajitahidi wizara kutoa taaluma kwa wananchi kuhusu sheria hii.

Mhe. Spika, baada ya ufafanuzi huo, kwanza niseme tena kwamba nawapongeza wajumbe wote waliochangia hoja hii, nina imani katika mchango wao waliouonesha kuikubali, ila kuna kutofautiana katika makubaliano tu kwa binadamu. Wengine hukubali kwa haraka, wengine kidogo kidogo na mwengine hukubali kwa macho.

Kwa hivyo, nawaomba wajumbe waipitishe ili iwe sheria nzuri katika nchi yetu. Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo naunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kufanya majumuisho ya Mswada wa Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho kutokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kuhusu mswada wa sheria ya hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea, yaani *plant breeders rights* ya 2014.

Mhe. Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe kwa kuchangia vizuri mswada huu, napenda kuwahakikishia kuwa michango yao, maelekezo na ushauri wao tumeupokea na tutaufanyia kazi ipasavyo, kadiri ya uwezo utakavyoruhusu kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii na majukumu ya kazi na maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, mswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 24 akiwemo Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili. Wajumbe 20 wamechangia kwa kutoa maelezo yao ndani ya Baraza hapa jana na wajumbe 3 walileta michango yao kwa maandishi na Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili, amechangia kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za wajumbe ambazo zilijitokeza katika kuchangia mswada huu. Nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, kwa maelezo yake ya ufasaha ambayo bila shaka Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wameyaelewa vizuri sana.

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia katika mswada huu naomba kuwataja kama ifuatavyo:

1) Mhe. Viwe Khamis Abdalla - (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo).
2) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4) Mhe. Salmin Awadh Salmin
5) Mhe. Asha Bakari Makame
6) Mhe. Salma Mohammed Ali
7) Mhe. Saleh Nassor Juma
8) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
9) Mhe. Ali Salum Haji
10) Mhe. Hija Hassan Hija
11) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
12) Mhe. Salim Abdalla Hamad
13) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
14) Mhe. Abdalla Moh'd Ali

15) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
16) Mhe. Mohammed Haji Khalid
17) Mhe. Mussa Ali Hassan
18) Mhe. Suleiman Hemed Khamis
19) Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
20) Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora.

Wajumbe waliochangia kwa maandishi ni:

1) Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
2) Mhe. Marina Joel Thomas
3) Mhe. Fatma Mbarouk Said

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, tukianza na Mjumbe wa Kamati aliyewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti (Mhe Viwe Khamis Abdalla). Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Viwe kuwa wizara imechukua michango ya kamati yake ya kuijumuisha kwenye mswada huu na kupelekea mswada huu kuchapishwa upya. Pamoja na hayo wizara inaichukua michango yote iliyotolewa na kamati yake na tutaifanyia kazi ipasavyo.

Pili Mhe. Spika, hoja ambayo imezungumzwa na wachangiaji wengi, inahusu suala la mswada wa sheria hii, inahusu mambo yasiyo ya muungano na mamlaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika kusimamia mambo yasiyokuwa na muungano kwa pande zote mbili.

Mhe. Spika, hoja hii imetolewa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Abdalla Moh'd Ali, Mhe. Salim Abdalla Hamad na Waheshimiwa wengineo. Tunapenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba suala hili halina utata wowote wa kisheria ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kwa kutoa ufafanuzi wa utangulizi wa kina juu ya suala hili. Hata hivyo wizara inapenda kutoa maelezo ya ziada kuhusu hoja hiyo.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa juu ya masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio yenye

mamlaka Kikatiba ya kuingia na kuridhia mikataba ya Kimataifa. Baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kuridhia mkataba wa *UPOV* mwezi wa Februari 2010. Lilivyokuwa suala la kilimo si la muungano, pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano ziliwajibika kutunga sheria zitakazowezesha utekelezaji wa makataba wa *UPOV*. Kwa upande wa Tanzania Bara Sheria ya Hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ilitungwa na Bunge mwezi wa Novemba 2012 na sio mwaka 2010 kama baadhi ya Wajumbe walivyodai.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyojitokeza, ni kwa nini katika kifungu cha 9(2)(i) cha mswada huu kimependekeza kwamba mrajisi wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu Tanzania Bara kuwa ni mjumbe wa Kamati ya ushauri wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama tulivyoeleza hapo awali sheria hizi kwa pande mbili za Jamhuri ya Muungano zimewajibika kufuata matakwa ya mkataba wa *UPOV* kuwa na sheria zinazolingana. Sheria kama hii ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya muungano mwezi Novemba 2012 katika kifungu cha 9(2)(h) imemtaja mrajisi wa Zanzibar kuwa ni mjumbe wa Kamati ya Ushauri wa Hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ya Tanzania Bara.

Mhe. Spika, na hili nataka nichukue nafasi hii ya kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika sheria hii katika kifungu hiki, mrajisi wa taasisi hii anakuwa bosi na mrajisi wa Tanzania Bara anakuwa katibu katika kamati ya ushauri kule. Kama ilivyo katika sheria yetu inamtaja mrajisi wa Tanzania Bara kuwa mjumbe na katibu na mrajisi wa Zanzibar anakuwa katibu wa kamati ya ushauri.

Mhe. Spika, Wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu wametaka ufafanuzi juu ya tafsiri ya maneno ambayo yametajwa ndani ya sheria kama vile rajisi. Kwa mujibu wa sheria hii maana zilizotolewa zitatumika kwenye sheria hii tu na kama ambavyo kifungu cha 2 kilivyoeleza. Hili si geni Mhe. Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe. Kuna sheria zinazomtaja Mhe. Rais lakini kwa maana ya Katiba ya Zanzibar na sheria nyengine zinazomuhusu Rais wa Zanzibar, maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini kuna Sheria pia kama ya ZFA inamtaja rais lakini kwa maana ya ZFA ni Rais wa ZFA. Kuna sheria pia ya Chama cha Wafanyabiashara Zanzibar kinamtaja rais vile vile lakini kwa maana ya sheria ile ni rais wa *Chamber of Commerce* na sio Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mfano kama huo kuna Sheria ya Mtoto; kuna sheria nyengine ya mtoto inamtambua mtoto akiwa miaka 15 akifikia umri wa miaka 15 anakuwa ameshafikia kutoka katika eneo la utoto. Kuna sheria vile vile ya mtoto inamtambua mtoto mpaka kufikia umri wa miaka 18, lakini kuna sheria nyengine vile vile ya mtoto inamtambua mtoto kwa miaka 21. Kwa hivyo tafsiri ya neno inategemea sheria ile iliyotungwa na iliyokusudiwa ndiyo inatoa maana. Huwezi kutoa maana ya tafsiri ya neno kwa sheria nyengine isipokuwa uitafsiri kwa ile sheria ambayo imetungwa.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Rufaa kufanywa na Waziri. Sio kila bodi mwenyekiti anateuliwa na Rais. Baraza lako hili tukufu limeshapitisha sheria nyingi ambazo wenyeviti wake wanateuliwa na Mawaziri. Kwa mfano Sheria ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma ni kama bodi au ni bodi hasa unaweza ukasema, lakini Mwenyekiti wake hateuliwi na Rais anateuliwa na Bodi, inategemea namna ya sheria ilivyotaka, kwa hivyo sio kila mwenyekiti anaweza akateuliwa na Rais. Wapo wenyeviti wa bodi wanateuliwa na Rais na zipo bodi nyengine ambazo zinateuliwa na waziri. Sababu ya kumteua mrajisi wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu kuwa ni katibu wa kamati ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake, kwa vile yeye ndiye mtendaji mkuu wa ofisi ya hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu. Maelezo zaidi niliyaanza kwenye utangulizi wangu wa mwanzo na nikasema hili suala la kwamba yeye atakuwa mdogo kuliko mrajisi wa Bara nimeshalitolea ufafanuzi. Sheria zote mbili zinawatambua warajisi wote kuwa ni Makatibu wa Kamati ya Ushauri, lakini kwa upande mmoja anakuwa mjumbe na kwa upande mwengine anakuwa katibu. Hili ni suala tu la ku-*harmonize* hizi sheria kwa mujibu wa matakwa ya *UPOV*.

Mhe. Spika, aidha napenda kumshukuru Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk (Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili) kwa ufafanuzi wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Aidha napenda kumshukuru Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mchango wao na ushauri wao ambao wametupatia tokea tumeanza kujadili Mswada huu kuanzia kwenye Kamati mpaka maoni yao ambayo wameyatoa ndani ya Baraza tukufu. Maoni yao na michango yao hasa ile iliyotolewa na Mwenyekiti, imetusaidia sana katika kutoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Pia napenda kumshukuru Mhe. Dokta Mwinyihaji Makame, pamoja na Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza kwa namna moja au nyengine wamesaidia kutoa ufafanuzi juu ya masuala haya.

Mhe. Spika, naomba kukushukuru wewe kwa mara nyengine tena binafsi kwa kukiendesha kikao vizuri wakati wa majadiliano ya Baraza hili tukufu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru. Hoja Waheshimiwa Wajumbe imetolewa, na mimi sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga sheria ili kupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika Pamoja na Marekebisho yake.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipata nafasi ya kuchangia mswada huu na nilipokuwa nachangia nilikuwa nasema naunga mkono lakini kwa masharti kwamba ikiwa una maslahi na Wazanzibari.

Alipokuwa akitoa ufafanuzi Waziri Dokta Mwinyihaji alisema sana kwamba sheria hii zaidi ni ya kibiashara na wale wagunduzi.Sasa mimi nimepata wasiwasi, wasiwasi wangu na hawa GMO ambao wanatumia zaidi makemikali yanaweza kuathiri sana hadhi na afya za watu na pia wanaweza kurudisha kwa kiwango kikubwa sana uchumi wetu. Sasa namuomba Waziri anipe ufafanuzi kwamba sheria hii haitokuja kufikia hii GMO, maana yake ikiwa itafikia hivyo, kwa athari zake mimi nadhani tukubaliane tu basi. Naomba ufafanuzi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, hoja

ya Mhe. Abdalla Juma Abdalla aliyoitoa jana ilikuwa inahusu suala la sheria hii ina maslahi gani kwa Wazanzibari, ndio hoja ya msingi. Mimi na Waheshimiwa wengi tuliokuwepo hapa tunaamini kwamba sheria hii ina maslahi makubwa sana kwa Wazanzibari.

Ndani ya Baraza hili tumekuwa tukizungumzia sana juu ya kuwaenzi na kuwatunza wataalamu. Mpaka sasa bado tunalo tatizo la kuwatunza na kuwaenzi wataalamu. Serikali ya awamu ya saba inachukua juhudi kubwa ya kuweza kuona tunafanyaje ili kuwaenzi na kuwatunza wataalamu wetu.

Sasa katika suala zima la kuweka sheria hii na kutambua watafiti na wagunduzi ambao ni wataalamu wetu hilo ni jambo lenye maslahi makubwa sana kwa Wazanzibari walio wengi katika hili. Kwa hivyo mimi sijaona hasa tatizo kutokuwa na maslahi ya Wazanzibari au ya nchi yetu katika kuitunga sheria hii. Ndio maana sasa sheria hii inawekwa ili tuweze kulinda zile taaluma zao au ule ugunduzi wao watakaoweza kuwa wameuvumbua.
Kwa hivyo Mhe. Abdalla Juma Abdalla nataka nimuhakikishie kwamba hili halina uhusiano wowote na kuweza kuwaathiri wataalamu watakaokuwepo katika sehemu za kutumia kemikali na mambo mengine. Kwa sababu sehemu za maabara zitatoa mchango mkubwa katika kupata ugunduzi wa kile ambacho kinakusudiwa, kupata ugunduzi wa mbegu mpya za aina ya mbegu. Katika mantiki hiyo mimi naona kwamba kutakuwa kuna maslahi makubwa kwa ajili ya kuwatunza na kuwasaidia Wazanzibari. Na utakapowasaidia wataalamu wanaotokana na Zanzibar, maana yake maslahi ya Zanzibar yatakuwa yamezingatiwa. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Maelezo ya Mhe. Waziri ni mazuri lakini hofu yangu miye na nimejenga hofu kwa sababu ya hizi gharama zinazopatikana kwa hii *GMO*. Miongoni mwa athari ya *GMO* ni kwamba inapoteza kabisa uwezo wa ardhi kuweza kuotesha mbegu, halafu ina *contamination* kubwa ambayo itatutia athari mpaka kwenye zao letu ka karafuu. Mazao yanayozalishwa kupitia *GMO* sasa hivi hayana soko duniani na hayatakiwi.

Naomba *hansard* ikae vizuri, sasa ikiwa Mhe. Waziri anatoa *statement* kwamba sheria hii haihusiani kabisa kabisa na mambo ya *GMO* basi mimi sina tatizo, lakini ikija ikitokea, kwa sababu ukisoma kifungu cha 4 au katika madhumuni na sababu ya kuletwa sheria hii inatajwa pale ku- *invite* wawekezaji kutoka nje. Sasa ikija ikitokea kwamba kuna uhusiano wowote kati ya sheria hii na masuala ya *GMO* basi tutakuwa na dhamana kubwa. Itumike *hansard* hii basi kuja kuifuta sheria hii wakati huo. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na Mhe. Abdalla Juma Abdalla kwamba nchi nyingi suala la *GMO Genetically*

Modified Organism ni kitu ambacho hawakikubali, lakini kuna nchi nyingi ambazo suala hilo wanalikubali kwa sababu zao nzuri. Kwa sisi suala la kwamba tunakubali au hatukubali ni suala ambalo linashughulikiwa kwenye sheria nyengine ya kuhusu kilimo na mimea ni sheria mbali.

Suala kwenye sheria hii Mhe. Mwenyekiti ni kwamba kigezo kinachotumika kama atakavyoona kwenye sheria ilivyoelezwa ni vigezo vinne, kama mbegu iliyogunduliwa itakuwa imetimiza vigezo vinne, basi mbegu hiyo inaweza kama Mrajis atathibitisha kwamba imetimiza vigezo vinne hivyo ikasajiliwa.

Vile vile waliopitia sheria hii, maana yake sheria hii imeunda huu Umoja wa Wagunduzi wa Mbegu, nadhani mwaka 1991 walikubali kwamba teknolojia ya *GMO* kama itakuwa itatimiza vigezo vinne, basi nchi ina hiari yake kuweza kuitambua mbegu hiyo na kuisajili. Kwa hivyo, kwanza na mimi niseme kwamba hicho ni kitu kinachowezekana, lakini sheria hii inachotambua ni suala la usajili wa mbegu na jambo la kuingiza nchi na kuitumia ni kitu chengine, na ni kitu ambacho kina sheria nyengine yake mbali kusema kweli.

Kutokana na hali hiyo ni lazima uwe na leseni na ufuate taratibu za kuingiza ile mbegu na kuweza kuitumia nchini, lakini sheria hii haihusiani kabisa na suala la uingizaji wala matumizi ya mbegu, isipokuwa ni kumtambua tu mtu kwamba ametumia utaalamu huu katika kuja na mbegu ambayo imetimiza vigezo vile vinne, kuwa ni mpya, iko *stable*, ni tofauti na nyengine na ni ya kipekee haihitaji kitu chengine kuweza kuingizwa.

Kwa hivyo, nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi pamoja na Waheshimiwa wengine, kwamba sheria hii haihusiani na matumizi ya *GMO*, wala uingizaji wake na hata kukubalika kwake kwa matumizi katika nchi. Kwa maana hiyo, hivyo ni vitu viwili tofauti, lakini mbegu ambayo imegunduliwa kwa kutumia utaalamu huo nchi ikiamua inaweza kuisajili ilimradi imetimiza hivi vigezo vinne, lakini si lazima ukishaisajili uitumie ni sawa na dawa, kwamba unaweza lakini bado nchi ikawa na hiari kwamba dawa hii itumike au isitumike, na hivi ni vitu viwili tofauti na wala havihusiani moja kwa moja katika sheria hii.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante baada ya kupata ufafanuzi huo wa kitaalamu naondoa wasiwasi kwamba sheria hii haitahusiana moja kwa moja na *GMO*, na kwamba Zanzibar mbali ya sheria hii itakuwa na hiari kukubali kwamba bidhaa za *GMO* ziingie au zisiingie kwa sheria nyengine ambazo zitafuata baadaye.

Baada ya maelezo hayo mimi naridhika na ninaomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili
Ofisi ya Hakimiliki za Wagunduzi wa
Aina Mpya za Mbegu za Mimea

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa ofisi.
Kifungu 4

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kifungu hichi cha 4(3) naomba kunukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 4(3) kinaeleza hivi:-

"Kwa madhumuni ya kifungu hichi vigezo vinavyotakiwa vitajumuisha angalau shahada ya Chuo Kikuu kutoka taasisi yoyote inayotambulika katika fani ya sayansi na kilimo, sheria au fani inayofanana pamoja na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano."

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hapa kwamba muhimu ni fani au uzoefu, lakini kama ni uzoefu kwa nini iwekwe miaka mitano ya uzoefu, kwa sababu mtu yeyote anapofanya kazi si lazima awe kuwa lazima awe na uzoefu wa miaka mitano, miaka miwili inatosha kuwa na uzoefu wa kufanya kazi ile ambayo anayotakiwa. Sasa kwa nini kuweka uzoefu, lakini usiopungua miaka mitano na hawa wengine wanaosomeshwa na wakapata hizi fani huu uzoefu kama hawajafanya kazi wataupata wapi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, naelewa hoja ya Mhe. Bikame Yussuf Hamad, hoja yake ni kuona vijana wetu wanaomaliza vyuo wanapata ajira. Suala la ajira na suala la uteuzi ni vitu tofauti. Suala la ajira lina taratibu zake ambazo ndio inazingatia hayo masuala ya vijana ambao wanatoka vyuoni wakiwa na taaluma zao. Sidhani kule kama ajira nyingi zinahitaji uwe na uzoefu hata wa miezi sita.

Mheshimiwa, zipo taasisi au ajira zinazohitaji uzoefu, hili lazima tulikubali. Na katika eneo la taasisi kama hii ya kitaalamu au ya kitaaluma, inahitaji taaluma lakini pili inahitaji na uzoefu. Kigezo cha uzoefu tunachokichukulia sisi basi kisipungue miaka mitano kwa mujibu wa sheria hii, lakini unaweza

ukaenda kwenye taasisi nyengine kigezo kikawa ni miaka mitatu au ikawa ni miaka kumi, inategemea na uzito wa lile jambo lenyewe.

Sasa Mheshimiwa lile tatizo ambalo yeye ana hofu nalo la ukosefu wa ajira kwa vijana ni tofauti kabisa na hoja hii ya hapa. Naomba tu akubaliane na kifungu au maelezo yaliyoelezwa katika sheria hii kwamba hiki kigezo cha miaka mitano, kibakie hapa katika sheria hii ili kuweza kupata mtu ambaye atakuwa na uwezo na uzoefu mkubwa katika kuzifikia nafasi hizi. Ahsante sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu keshasema kwa sheria hii ni lazima mtu awe na uzoefu wa miaka mitano, lakini Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo la miaka mitano kwa uzoefu huu basi ni mkubwa sana, lakini kwa kuwa mwenyewe Mhe. Waziri keshaona ni lazima apate mtu mwenye uzoefu wa miaka mitano, sawa na tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 4	Uteuzi wa Mrajis
Kifungu 5	Kazi za Mrajis
Kifungu 6	Rajisi, Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 7	Ushahidi wa Maelezo na Nyaraka Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 8	Ukaguzi na Rajisi
Kifungu 9	Kamati ya Ushauri wa Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 10	Kazi za Kamati
Kifungu 11	Vikao na Taratibu za Kamati Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 12	Uwezo wa Kamati Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Tatu
Aina za Mbegu Zitakazolindwa

Kifungu 13	Aina za Mbegu Zitakazolindwa
Kifungu 14	Masharti ya Kulinda
Kifungu 15	Upya Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 16	Utofauti
Kifungu 17	Usawa
Kifungu 18	Udadisi

Sehemu ya Nne
Maombi ya Hakimiliki za Wagunduzi wa
Aina Mpya za Mbegu za Mimea

Kifungu 19	Maombi ya Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 20	Yanayotakiwa Katika Maombi

Kifungu 21 Jina la aina za mbegu pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tano
Mazingatio na Kutangazwa kwa Maombi

Kifungu 22 Tarehe ya Maombi
Kifungu 23 Haki ya Kipaumbele
Kifungu 24 Marekebisho ya Maombi

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti hapa naomba ifanyiwe masahihisho. Hiki kifungu cha 24 marekebisho ya maombi, muombaji anaweza kufanya marekebisho katika maombi yake, sasa nilimwambia Mhe. Waziri hapa, wakati hiki kifungu ni cha marekebisho ya maombi, lazima hapa kusemwe kuwa muombaji anaweza au muombaji atafanya marekebisho katika maombi yake, atafanya au anaweza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti mimi ninafikiri lugha inawezekana lakini muombaji anaweza ukisema atafanya maana yake lazima afanye, lakini anaweza ikiwa anaona kuna haja ya kufanya marekebisho ndivyo ninavyoona na ndio lugha ambayo ninahisi ya kisheria iwepo hapa, hakuna lugha ya atafanya. Lugha ya kisheria lazima anaweza maana anaweza ama afanye ama asifanye, maana sio lazima kufanya, kwa hivyo anaweza ndio neno sahihi.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 24 Marekebisho ya Maombi
Kifungu 25 Uchapishaji wa Notisi ya Maombi
Kifungu 26 Pingamizi za Pendekezo la Utoaji wa Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 27 Sababu za Pingamizi
Kifungu 28 Notisi kwa muombaji na majibu ya pingamizi
Kifungu 29 Kutangazwa kwa maombi

Sehemu ya Sita

Ulinzi wa Muda na wa Kudumu

Kifungu 30 Ulinzi wa Muda
Kifungu 31 Maeneo ya Hakimiliki za Wagunduzi yanayotokana na aina nyengine za mbegu
Kifungu 32

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia mbali yale ya jumla nilisema kuna baadhi ya mambo kutokana na mswada huu kuwa ni wa fani maalumu, nilipaswa kupewa ufafanuzi na nilitaja baadhi ya vifungu ambavyo niliomba ufafanuzi, lakini ninasikitika majumuisho ya Mhe. Waziri zaidi yalijikita katika maeneo machache mno ambayo yalizungumzwa jana. Sasa nilikuwa naomba anisaidie tu kwa sababu katika mchango wangu niliomba ufafanuzi wa kilichokusudiwa katika kifungu cha 32(1) (b) na (c), ile (a) nimeifahamu kwamba hakimiliki za wagunduzi hazitatolewa katika maeneo haya, sasa ningeomba ufafanuzi wa kilichokusudiwa katika kijifungu cha (b) na (c).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili:) Mhe. Mwenyekiti, ningeomba akarejea yale maelezo yake ya jana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwenye 32(1) (b) niliuliza kwamba hapa imesemwa kwamba hakimiliki za wagunduzi hazitatolewa kwa kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya kiutafiti. Nikauliza kwamba kwa nini ugunduzi uliopatikana kupitia kazi ambazo zilifanywa kwa madhumuni ya utafiti mtu asiwe na haki nayo. Kwa sababu kimsingi huo ugunduzi wenyewe wa mbegu pengine utakuwa umetokana na utafiti ndio unaupata, sasa kwa nini hili lika-*exclude* au likaondoa kuwa na haki miliki.

Lakini vile vile kijifungu cha (c) kilisema kwa kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya ugunduzi wa aina nyengine za mbegu na isipokuwa pale ambapo maelezo ya kifungu cha 31(5-7) kitatumika kazi zilizoainishwa katika kifungu cha 31(1-4) kulingana na aina nyengine za mimea, niliona haya maelezo mengi mimi nimeshindwa kuelewa makusudio yake, lakini imejikita zaidi kwa haya maelezo ya ufunguzi kwamba kwa kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya ugunduzi wa aina nyengine za mbegu, isipokuwa hayo ambayo yametajwa. Sasa niliomba nipewe ufafanuzi nijue kwamba kwa nini? Kwa sababu kifungu cha 32 kimsingi Mhe. Mwenyekiti, kinaondosha haki hiyo ya hakimiliki za ugunduzi katika mazingira hayo yaliyotajwa hapo.

Sasa (a) liko wazi kwamba lilikuwa limefanywa kwa shughuli binafsi sina sababu ya kudai hakimiliki, lakini kwa kijifungu cha (b) na (c) kuna mazingira mengine nayo pia yameondolewa kwamba yanaondosha ile haki ya kuwa na hakimiliki juu ya ugunduzi huo, kwa hivyo niliomba maelezo juu ya vifungu hivi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba suala hili ni la kitaalamu sana kama alivyoliona mwenyewe Mhe. Jussa kwamba

haya ni mambo ambayo yameondolewa katika hizi haki kwa sababu maalumu na kwa sababu ya uzoefu uliopatikana katika shughuli maalumu, labda pengine hata mimi nikimfahamisha lakini iko *manual* ambayo mimi na yeye Mhe. Jussa tukiisoma nikamfahamisha nadhani ataweza kuelewa madhumuni yake. Lakini kwa ufupi kwa mfano hii ya (b) kilichokusudiwa hasa ukirudi kwenye vile vigezo vinne vya kupata kukubalika kwamba ni haki ya kupewa ile hakimiliki ya ule ugunduzi wenyewe. Kigezo kimoja cha kwanza ni *novelty* yaani kuwa ni kitu kipya.

Mara nyingi utafiti uliokusudiwa hapa ni ule utafiti ambao tayari unahusisha ama watu wengi ama unahusisha kitu maalumu, pengine ule ufafanuzi kwa sababu hii sheria mbali ya hii sheria yenyewe lakini kuna miongozo, kuna kanuni kuna na ule mkataba wenyewe unaoongoza tafsiri ya vifungu mbali mbali ya kwamba kwa mfano utafiti uliokusudiwa hapa, utafiti uliokusudiwa hapa ni kwamba ni ule utafiti ambao kile kigezo cha mwanzo cha upya wake basi kitakuwa cha kupatikana ule upya kinaondoka. Kwa sababu ama unahusisha watu wengi au unahusisha jambo jengine ambalo tayari linajulikana msingi wake, si kitu kwamba mtu kakaa mwenyewe kagundua akaja na hii, kwa hivyo anakosa kile kigezo cha mwanzo cha kupata ile hakimiliki.

Na hiki kigezo vile vile utakuta anakosa vile vigezo vyengine vitatu vya kupata ile hakimiliki pamoja na kile cha nne kwamba hii imekusudiwa kwamba kuna utafiti maalumu ambao unafanywa kwa ajili ya kupata kitu maalumu au matokeo ya kuthibitisha jambo maalumu. Lakini katika jambo lile kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri ikatokea mkagundua kitu chengine na hii imeshawahi kutokea katika kazi hizi. Sasa pale ndio ambapo anakuwa yule mtu hana haki ya kupata hiyo kwa sababu utafiti unakusudiwa iwe ni *individual mission, individual endeavor* ya kukusudia kwamba mimi ninakusudia ninafanya utafiti wa kugundua hii mbegu, isitokee kitu kama kimetokea kwa bahati mbaya au imetokea kwa *incident,* kwa sababu linakuwa ni tatizo kitu kile kinawezekana na watu wengine kwa wakati ule ule mmoja wanaendelea kufanya utafiti katika jambo lile moja. Sasa ndio maana zikawekwa hizi *exception* tokea kwenye mkataba wenyewe, kwenye miongozo ya usajili, vile vile kuna maelezo kusema ya kina, na ambayo yenyewe ndio sasa yanakuwa ni muongozo wakati gani inakuwa, hii ni aina mpya, hii ina *stability,* hii ni mbegu ambayo wanasema ina *stability*.

Katika utafiti wa namna hii yanakuwa hayo yanakosekana kwa sababu ama ni watu wengi, kwa hivyo kuja kukubali kwamba nani aliyeanza mwanzo nani ambaye hili kaligundua wakati mwengine linawapa shida katika utekelezaji. *Actual* ukisoma kwenye zile *process,* ukisoma kwenye ile miongozo yenyewe na kuna mifano mingi ambayo inaeleza ni kwa nini mambo haya

hayakubaliwi. Kusema kweli yana maana yake na ni mambo ambayo hatukuyavumbua isipokuwa yamechukuliwa kutokana na miongozo iliyomo ndani ya mkataba wenyewe na miongozo ambayo imo katika miongozo ya namna ya kusajili hizi aina mpya za mbegu. Naweza kutoa maelezo kwa sababu si mtaalamu wa mbegu ikawa shida yeye kunifahamu na ikawa shida na mimi kumfahamu vile vile, lakini ninachoweza kumuhakikishia tu ni kwamba ni mambo ambayo ni *exception* zina sababu zake na zimo katika mkataba wenyewe na zimo katika miongozo ya usajili wa hizi aina mpya za mbegu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naona kwa hili leo tutakanyaga chechele sote mimi na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa sababu nimeelewa kimsingi mantiki ya hoja zake lakini nilitegemea kwamba hiyo miongozo basi wale ambao wametuletea mswada wawe nayo ili tukihoji waitumie kutujibu, kwa sababu wao ndio walionayo waliotayarisha mswada huu. Sasa hofu yetu kwamba sisi tunapotunga sheria ni kwamba turidhike kwa kile ambacho tumekitunga tumekielewa, na kwa hivyo tunaowapelekea huko kitakuwa kina maslahi nao. Kwa hivyo hilo kidogo linatupa mashaka Mhe. Mwenyekiti. Labda kidogo katika kifungu cha 32(1)(b) nimemuelewa, ingawa ninapata shida kidogo kwa sababu hayo maelezo aliyotupa labda itakapokuja kutokezea *dispute* yoyote itaangaliwa *hansard.* Kwa hivyo yatakuwa yameingia miongoni mwa dhamira zilizopelekea kutungwa mswada huu, lakini ndani ya mswada huu hayaonekani hayo maelezo ambayo yana *limit* katika misingi hiyo ya utafiti aliloeleza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

Lakini hicho nikikiacha bado mimi naomba Mhe. Mwenyekiti nisaidiwe zaidi kuhusu hiki 32(1) (c). Kwa sababu gani, kama nilivyosema kwanza kina rejea nyingi ambazo zinapelekea ugumu wa kufahamu kinasema, "hapa hakuna hakimiliki ya ugunduzi si kwa kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya ugunduzi wa aina nyengine za mbegu na isipokuwa pale ambapo maelezo ya kifungu 31(5-7) kitatumika." Naomba nisite hapo Mheshimiwa kidogo, 31(5) nikikitizama kinataja hayo Mhe. Mwanasheria Mkuu aliyoyataja kwamba kwa mfano kinasema (5) maelezo ya kifungu 1,2,3, na 4 kitatumika kwa (a) hii Mhe. Mwenyekiti nasoma 31(5). Aina za mbegu ambazo uasilia wake unatokana na aina za mbegu zilizolindwa ambazo ni mbegu halisi zisizotokana na aina nyengine za mbegu.

(b) Aina za mbegu ambazo hazitofautiani kwa uwazi kulingana na kifungu 16 kutokana na aina za mbegu zilizolindwa. Na niliposoma hazitofautiani nikaja katika hizo nilizozungumza sifa ya kuwa *distinct* kwamba ina aina ya upekee. Na *still* aina za mbegu ambazo uzalishaji wake unahitaji matumizi ya kudumu ya aina za mbegu zilizolindwa. Halafu pia kuna maelezo sitaki kuyasoma kwa sababu ni marefu haya 6 na 7, lakini hapo hapo inasema nikirudi 32(1) (c),

kazi zilizoainishwa katika kifungu cha 31(1- 4) kulingana na aina nyengine za mimea.

Sasa Mhe. Mwenyekiti 31 ujumla wake *marginal notes* yake inasema maeneo ya haki miliki za wagunduzi wanayotokana na aina nyengine za mbegu, lakini huku ukizisoma zile kilivyoanzia 32 (1) (c) inasema hakuna hakimiliki ya ugunduzi kwa kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya ugunduzi wa aina nyengine za mbegu sasa ndio maana nikasema inatutatiza. Kama alivyosema ni mswada wa kitaalamu sana, lakini nadhani pia pamoja na utaalamu wake ni lazima tuufahamu turidhike tunapitisha nini, sio tu kwamba maadam kuna *manual* turidhike. Kwa hivyo nilikuwa nasema bado mimi nitasema Mhe. Mwenyekiti hapa hizi aina nyengine za mbegu zipi ambazo zinakuwa *excluded* au zinaekewa kwamba hizi mtu atakuwa hana hakimiliki ya ugunduzi wake, wakati hicho cha 31 ambacho kimefanyiwa rejea kinazungumzia *marginal notes* ni maeneo ya hakimiliki za wagunduzi yaliyotokana na aina nyengine za mbegu. Sasa aina nyengine zipi za mbegu huku ambazo zilikuwa zimekubaliwa ambazo huku zinakataliwa katika 32(1)(c) kidogo sijaelewa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nirejee yale maneno ya Mhe. Jussa kwamba kweli huu mswada na sheria yenyewe na fani yenyewe kwanza kama hamkuwa wataalamu basi ni rahisi kukanyaga chechele, tena mkamkanyaga kiunoni, lakini kwa ufupi naelewa hapo anaposema kwamba ni vigumu kufahamu, kwa sababu maana kwenye fani hii bahati mbaya hata na mimi mwenyewe nilipokuwa nikisoma kule Italy nilikosomea fani hii, basi kidogo darasa hili lilikuwa likinipa shida. Mhe. Mwenyekiti nadhani haitokuwa vibaya nikisema tulikuwa na mwalimu mwanamke wa Kijarumani kwa jinsi tulivyokuwa hatumfahamu alikuwa hajaolewa, tukawa tunaambiana labda akipata mume ataeleweka. Kwa sababu ilikuwa shida kumfahamu alipokuwa akisomesha vile vile.

Lakini kwa ufupi msingi wake ni kwamba katika ugunduzi kuna ugunduzi ule wenyewe wa awali yaani *original invention,* halafu ukishagundua ile *original invention* kuna na vitu vinavyoitwa na ambavyo kwa kizungu wanasema ni *upstream invention*, yaani ni ule ugunduzi wa hali ya juu wa mwanzo. Lakini ukishagundua ule ugunduzi wa hali ya mwanzo wa juu kuna kitu kinaitwa chengine *down stream invention*, yaani ni watu ambao watavumbua kutokana na kile ulichokivumbua; yaani kwa kutumia ule uvumbuzi wako wa awali mkubwa kuna kitu kinaitwa *down stream invention* yaani mtagundua vitu vyengine wanasema *inventing around.* Hivi mara nyingi Wamarekani ndio rahisi kuvikubali, nchi nyingi hawakubali katika ile *inventing around.*

Sasa kifungu cha 31 kinachokusudia ni kuongoza, kuweka misingi ya kwamba mtu keshafanya ugunduzi wake, sasa mambo gani ambayo yakitaka kufanyika na mara nyingi ambayo yanahusiana na ugunduzi kupitia na lile alilolilogundua, kugundua zaidi mambo gani lazima yeye mwenyewe atoe ruhusa, ndio haya kifungu cha 31; ni mambo yanayohitaji yeye mwenyewe atoe ruhusa na akishatoa ruhusa mtu mwengine akigundua anawezekana sasa na yeye akapewa haki ya ugunduzi. Kwa hivyo ile inakubalika kama ni *lawful bound stream invention* kwa Kiingereza, kwamba mmegundua kitu na mwengine kaja kaongezea uvumbuzi katia utaalamu zaidi katika ule uvumbuzi basi ile sheria inaweka misingi, na hayo yanatokea sana inaweka misingi ya namna gani hilo liweze kukubaliwa sasa ndio madhumuni ya vifungu hivi vilivyoweka na mambo mengine, yaani moja ni hilo lakini kuna na mambo mengine ambayo ni ile *economic right* au ni haki ya yule mgunduzi.

Sasa ukija kwenye kifungu hiki anachosema cha 32 (1) (c) hichi kinakataza uvumbuzi ambao umefanywa kwa *down stream* yaani ku-*invent around* kila kilichovumbuliwa isipokuwa kama kimepata ruhusa kwa mujibu wa kile kifungu cha 31 ule utaratibu umekatwa, na mara nyingi haya kunakuwa na makubaliano, yule aliyevumbua awali naye anakuwa ni sehemu ya ule uvumbuzi ambao utakuja baadae. Sasa kama hilo halikufuatwa la kifungu cha 31 ndio mara nyingi inakuwa ile *down stream invention* inakuwa haikubaliki hawezi mtu kupewa. Na hawezi kupewa kwa sababu wanasema kwamba ni kitu kipya, maana upya una *level* yake, tunaweza tukasema hichi kipya lakini kwenye *patent* kwenye mambo haya ya uvumbuzi, ule upya una *level* yake. Sasa kama wewe umegundua *around* kutokana na mtu kitu ambacho alishagundua halafu ukaja ukasema wewe umegundua hiki kitu upewe haki ile *novelty* haipo ndio inayogomba kwamba ule upya unakosekana, kwa sababu wewe ume-*build up* kutokana na mwengine ambaye tayari alikwishafanya ugunduzi, *unless* muwe mumekubaliana na kweli kije kitu ambacho baadaye kitakuja kufuata haya masharti manne ya kupewa haki ya ugunduzi.

Ndio maana nikasema kwamba kusema kweli kwa sababu kwenye hizi *manual* wametoa na mifano, bahati mbaya mimi si mtaalamu wa hii fani ya mimea labda ningeweza kutoa na mifano, lakini ninachosema ni kwamba hichi ni kawaida na misingi yake imewekwa katika kudhibiti zile *down stream invention* ambazo zinatokea katika masuala haya ya ugunduzi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nilipomtaja chechele imesaidia na hasa mimi nimeridhika baada ya maelezo haya kwamba kumbe Mhe. Mwanasheria Mkuu alimfahamu vyema mwalimu wake yule Mjarumani aliyekuwa hakuolewa. Na nadhani elimu na maarifa na maalumati aliyotupa

hapa kwa sababu yeye keshaoa tena mzega zega basi nimemuelewa vizuri zaidi sasa hivi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nimeridhika, nimefurahi kwamba nimejibiwa suali ambalo nadhani sio mimi peke yangu lakini wengi wamefaidika kutokana na jinsi alivyolieleza. Kwa hivyo ninamshukuru sana ninamuomba aendelee kuongeza baada ya mzega mzega uwezo wake wa kufahamu uwe mkubwa zaidi na sisi tuweze kufahamu zaidi kutoka kwake. Ahsante.

Mhe. Spika: Na mimi ninamshukuru maana mtu kufikia kwamba kajua matatizo mpaka ya mwalimu kwa nini hafahamiki, tunaendelea.

Kifungu 32	Mipaka ya hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 33	Uchakavu wa Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 34	Kipindi cha Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina mpya za Mbegu za Mimea
Kifungu 35	Ulinzi na Fidia kwa Ukiukwaji wa Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 36	Ada ya mwaka

Sehemu ya Saba

Ubatilifu, Ufutwaji na Kusalimisha Hakimiliki za Wagunduzi

Kifungu 37	Ubatilifu Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 38	Ufutwaji wa Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 39	Taarifa ya Ubatilishaji na Ufutaji wa Hakimiliki pamoja na marekebisho yake
Kifungu 40	Kusalimisha hakimiliki za Wagunduzi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba mawaziri au serikali kwa jumla wataendelea kunivumilia ili niridhike na kile ambacho tunatakiwa kukipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitaka pia maelezo juu ya nini kimekusudiwa katika kifungu cha 40, na hiki nadhani hakina mazonge sana lakini mimi bado kukielewa, kwa hivyo naomba ufafanuzi kinasema 40(1) hasa ndio nilipo, ‘mmiliki yeyote wa hakimiliki za wagunduzi anaweza kwa notisi ya maandishi kwa Mrajis kusalimisha haki za wagunduzi’. Sasa kifungu hiki cha 40 ukikitizama kinasimama peke yake lakini maelezo ya jumla sehemu hii ya 7 inasema ubatilifu, ufutwaji na kusalimisha haki za wagunduzi. Suala la kusalimisha unalipata katika kifungu hiki cha 40.

Niliuliza hasa katika mchango wangu kwamba vipi mmiliki wa hakimiliki za wagunduzi anasalimisha haki za wagunduzi ambazo mimi nilivyofahamu kwamba si zake, kwa hivyo nikasema kama kuna maelezo mengine ambayo sivyo nilivyofahamu mimi niliomba nipatiwe niweze kujua hasa nini lengo la kifungu hiki. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti labda lililombabaisha Mhe. Jussa ni ile za wagunduzi, lakini ni haki ya wagunduzi ndio hasa kinachosalimishwa. Na sababu za kusalimishwa ziko nyingi, moja inawezekana kwa sababu ya kibiashara kwamba kaombwa kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano mara nyingi zinatokea baadhi ya nchi mbegu iliyogunduliwa inahitajika kwa ajili ya *full security*. Sheria na ule mkataba inaweka utaratibu wa namna gani wa kuzungumza na yule ama akatoa leseni ama ikanunuliwe ile haki yake kwa ajili ya kwamba nchi iweze kuzalisha ile mbegu kwa wingi zaidi, iweze kusafirisha, anaweza akafanya hivyo. Kwa hivyo anapofanya vile maana yake ni ku- *surrender* kwamba anasema jamani mimi nilikuwa na haki hii, na kwa kuwa na haki ya ugunduzi maana yake unakuwa na haki nyengine; *restriction* nyingi inakuwepo kwenye ugunduzi ule. Kwa hivyo unapoi-*surrender* na ndio maana inatakiwa ichapishwe kwenye Gazeti Rasmi la Serikali kwamba hii imekuwa *surrendered* ili sasa inakuwa katika *public domain*, mtu yeyote anaweza akatumia kuzalisha au kusafirisha bila ya zile haki ambazo anazo mgunduzi kuweza kuzingatia ndio madhumuni yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nimemfahamu Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba tuendelee.

Kifungu 40 Kusalimisha Hakimiliki za Wagunduzi

Sehemu ya Nane

Ruhusa na Idhini

Kifungu 41 Ruhusa au Idhini ya Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 42 Vikwazo katika kutumia Hakimiliki za Wagunduzi
Kifungu 43 Maelezo ya Ruhusa, Idhini na Usambazaji

Sehemu ya Tisa

Rufaa

Kifungu 44 Bodi ya Rufaa
Kifungu 45 Rufaa dhidi ya Maamuzi ya Mrajis

Kifungu 46 Maamuzi ya Bodi ya Rufaa

Sehemu ya Kumi

Mfuko wa Maendeleo ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina mpya za Mbegu za Mimea, Mahesabu, Ukaguzi na Ripoti ya mwaka

Kifungu 47

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia niliuliza kwamba kwa nini huu mfuko wa maendeleo ya hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mimea umetakiwa na mswada huu kwamba uanzishwe na Waziri wa Fedha na usianzishwe na Waziri mwenye mwenye dhamana ya sekta hii ambaye ni Waziri wa Kilimo. Na nilisema Mhe. Mwenyekiti kwamba tunayo *experience* ya mifuko mengine ambayo imeanzishwa na Sheria nyengine na tusiende mbali hata mswada huu ambao tutakuja kuujadili baadae wa sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu dhamana imewekwa kwa Waziri mwenye dhamana ya sekta ile. Sasa niliuliza kwa nini kwa mfuko huu upelekwe kwa Waziri wa Fedha. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Nadhani Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi alisema vizuri sana juu ya sheria ile ya fedha ya mwaka 2005, kwamba sheria ile inataka mfuko wowote unaoanzishwa hapa ufanye hivyo. Sasa hili alilolisema ni *challenge* kwetu, na kwamba kuna sheria nyengine inamtambua Waziri mwenye dhamana kuanzisha mfuko, lakini sisi Wizara ya Kilimo na Maliasili tulizingatia zaidi sheria ile ya fedha, kwamba inamtaka au inamtambua Waziri wa Fedha kuwasiliana na Waziri wa sekta husika ili kuweza kuanzisha mfuko wowote ule unaohusu masuala ya fedha, ndicho kilichotupelekea sisi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti zaidi labda mambo mawili; kwamba mifuko hii miwili ni tofauti kidogo. Huu hapa unaanzishwa tunasema kwa *administrative order*, kwa amri ya kiutawala, huu wa ZSTC tayari Baraza hili kwa kupitisha sheria ile moja kwa moja tayari inauanzisha. Kwa hivyo hauhitaji, ni idhini ya Baraza kwa kupitia sheria, maana yake ule unakuwa ni *statutory fund,* huu ni *administrative fund.* Sasa huu *administrative fund* ndio unaohitaji idhini ya Waziri wa Fedha kwa mujibu wa sheria ya fedha, ndio tofauti yake kusema kweli.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimepokea maelezo, ingawa bado nilikuwa nasema anisaidie zaidi Mwanasheria Mkuu. Kwa

sababu kifungu cha 47(1) kinasema, "Waziri wa Fedha atalazimika baada ya kupokea maombi kutoka kwa Waziri kuanzisha Mfuko utakaojulikana kwa jina la "Mfuko wa Maendeleo ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za Mimea" ambao fedha zake zitakazopatikana chini ya sheria hii, zitahifadhiwa katika akaunti maalum".

Sasa baadae kifungu cha 47(2) kikataja vyanzo vya fedha hizo. Lakini pia kinaelezea fedha hizi zitatumika kwa shughuli gani ambazo bila shaka zitakuwepo. Kwa hivyo, hili suala la kwamba waziri mwenye dhamana ya sekta kwa maana ya waziri anayeshughulika na masuala ya kilimo atakuwa na haja ya kuona Mfuko huu, bila shaka kwa madhumuni ya mswada huu na maudhui yake, kwamba haja hiyo ipo tayari. Sasa nilikuwa najiuliza, labda wao maana fani ya utungaji wa sheria kwa maana ya kuandika sheria si fani yangu, watusaidie maana moja kwa moja nimemsikia Mwanasherai Mkuu akisema huu ni *administrative fund*, huu ni *statutory fund*!

Mhe. Mwenyekiti, huu umekuwa *statutory* kwa sababu unaazishwa na sheria, hoja yangu ilikuwa ndio hiyo kwamba kwa nini hapa kwa kufanya marekebisho tusione na huu pia ukafanywa ni *statutory*, ili mswada huu ukatoa dhamana moja kwa moja kwa waziri mwenye kusimamia masuala ya kilimo, kuanzisha Mfuko huu badala yake uzungushwe mpaka kwamba aombwe na Waziri wa Fedha alazimike kuanzisha Mfuko huu. Hebu nimuombe anisaidie maelezo ya ziada kidogo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama ni *reference* ya ule mswada unaoanzisha *statutory fund* unakuwa na sifa mbili kubwa. Sifa ya kwanza *statutory fund* Baraza lenyewe linasema moja kwa moja kwamba kutakuwa na Mfuko huu, lakini hauishii hapo. La pili, unaeleza namna Mfuko ule utakavyoendeshwa na inapoanzishwa maana yake moja kwa moja Baraza linakuwa limeona au limeridhika kwamba ipo haja ya Mfuko ule kuanzishwa. Huu, sifa yake ya kwanza ni kwamba inawezekana usianzishwe *immediate*.

Kwa hivyo ukisema utaanzishwa tu moja kwa moja kutakuwa na tatizo, unaweza ukaanzisha kitu ambacho kusema kweli kuhitajika kwake bado. Kwa sababu mpaka ufikie uwe na huo mfumo wenyewe wa ugunduzi, mpaka ifike kuhitajika huo Mfuko wenyewe, maana yake unahitajika *some mobilization*, baadae ndio unaweza ukaja ukawa huo Mfuko wenyewe ukaweza kuanzishwa.

Lakini la pili ni masharti ya sheria na maelekezo ya serikali kwamba, hii Mifuko mtu mwenyewe asikae akajianzishia kwa sababu ina *implication* ya kibajeti, ni vizuri Waziri wa Fedha ajue ili aweze kuweka *provision* katika bajeti yoyote na ndio maana sheria ika-*regulate* hii Mifuko ya namna hii.

Lakini Baraza hapa lina hiari yake, baada ya mapendekezo ya serikali kwamba linaweza likaanzisha Mfuko huu na ikaweza kuupa kazi zake na kuweka utaratibu wake wa kuendesha. Sasa huu hapa umeanzishwa hivi kwa sababu yale maombi yataeleza pia huo Mfuko wenyewe utaendeshwa namna gani, wakati hii iliyoanzishwa na Baraza tayari kwenye sheria unaeleza ule Mfuko wenyewe utaendeshwa namna gani na kwamba unaanzishwa *immediate* baada ya ile sheria yenyewe kuanza kufanya kazi. Kwa hivyo, tofauti zake ni hizo kwamba sheria inalazimisha kuwa Mifuko ambayo haikuanzishwa *statutory* basi ni lazima ipate idhini ya Waziri ya Fedha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuendeleza mjadala sana, nataka nikubaliane na maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Lakini niseme tu kwamba ni matumaini yangu kuwa hiyo haja ikionekana izingatiwe vyema na serikali. Kwa sababu nilichojaribu kufahamu mimi ni kwamba kama ilivyoelezwa katika madhumuni na sababu, mswada huu umekuja kwa sababu ya mkataba wa kimataifa. Na mara nyingi katika mashirika haya ya kimataifa ni kwamba bila shaka kunakuwa na misaada ya aina fulani ambayo inatolewa kwa zile nchi wanachama.

Sasa ni matarajio yangu ikiwa kuna kitu kama hicho ili isije ikamezwa fedha ambayo inaweza kutoka kwa shughuli maalum, ikamezwa kuwa mpaka ionekane kuna haja ya kuanzishwa Mfuko basi ikitokea fedha kama hiyo huo Mfuko matarajio yangu kwamba utaanzishwa ili fedha ile itumike kwa shughuli ambayo imekusudiwa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nasema nimeridhika na ufafanuzi naomba tuendelee.

Kifungu 47 Mfuko wa Maendeleo ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mimea
Kifungu 48 Mahesabu na Ukaguzi
Kifungu 49 Ripoti ya Mwaka itakayowasilishwa kwa waziri

Sehemu ya Kumi na Moja

Makosa na Adhabu

Kifungu 50 Makosa na Adhabu

Sehemu ya Kumi na Mbili

Vifungu vya Jumla

Kifungu 51	Makusanyo ya ada
Kifungu 52	Utunzaji wa siri
Kifungu 53	Kesi zidi ya serikali
Kifungu 54	Haki za Wagunduzi zinazohusiana na uwepo wa aina za mbegu za karibuni
Kifungu 55	Makubaliano na Serikali za Kigeni
Kifungu 56	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilitoa hoja nyingi sana kuhusiana na suala zima la mswada huu kuhusishwa na Jamhuri ya Muungano. Ingawa Wajumbe wengi kwa sababu ya hamasa na jazba zao walipoteza kabisa msingi wa hoja yangu kwamba ulikuwa ni kuonesha athari gani zinatupata kwa kukosa udhibiti wa Shirika la Kimataifa na kwamba pengine tungelikuwa na hilo tungepelekea Zanzibar kuwa mwanachama kamili wa *UPOV* yenyewe na kufaidika moja kwa moja, badala ya kutegemea mgongo wa mamlaka nyengine.

Lakini yametolewa maelezo sitaki kuendesha mjadala huo, lakini nilikuwa naomba tu nisaidiwe na nadhani katika hili zaidi nitamtegemea Mhe. Mwanasheria Mkuu anisaidie. Kwamba kifungu cha 56(1) kinasema, "Iwapo Mgunduzi si mkaazi au katika hali ya ushirika hana ofisi iliyosajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalazimika kuwa na wakala ambaye ni mkaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Sasa jana katika hoja nilizotoa nilisema kwamba sisi kimsingi Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu cha 78 cha Katiba ya Zanzibar mamlaka yetu ni kutunga sheria kwa mambo ambayo si ya Muungano ndaniya Zanzibar. *References* nyingi zimefanywa ndani ya mswada huu kwa Jamhuri ya Muungano, lakini hapa hasa Mhe. Mwenyekiti, ndipo ninapoona matatizo yake. Kwa sababu inazungumziwa kwamba, huyu ambaye tunataka kumfanya kwa kumtambua anatakiwa kuwa na ofisi katika Jamhuri ya Muungano kama imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungno, ikiwa hana basi awe na wakala ambaye pia ni mkaazi wa Jamhuri ya Muungano.

Sasa nikasema kwamba kilimo si suala la Muungano, tunatunga sheria kwa ajili ya Zanzibar ili manufaa haya yafike kwa Zanzibar, kwa nini isiwe kwamba huyu Mkurugenzi tunaemzungumza hapa awe kama ni ukaazi au kuwa ni ofisi awe mkaazi na awe na ofisi ndani ya Zanzibar. Ikiwa hana basi

awe na wakala wake ndani ya Zanzibar, kwa nini iwe ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hebu Mwanasheria Mkuu naomba anisaidie kidogo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, suala la ukaazi au kuwa na uwakala ni suala ambalo zaidi linazingatia uwezekano wa kumpata yule mtu kwa njia ya urahisi. Kuna nchi ambazo zinachukulia ukaazi ndani ya jumuiya za kikanda, kuna nchi ambazo zinakubali mikataba waliyonayo, yaani *reciprocity* waliyonayo. Kwa mfano, *by literally* kama wamekubaliana kushirikiana baina ya nchi mbili. Kwa hivyo, popote yule mtu anapokuwepo katika nchi zile anaweza kutambulika.

Sasa na sisi ukitizama mfumo wa sheria hii tumekwenda kwa namna ya mashirikiano na wenzetu Tanzania Bara, ndio maana tunasema kwamba tunaposema *United Republic* inategemea nani atavutia mwengine katika sheria zake nyengine, inawezekana ikawa Zanzibar vile vile. Kwa sababu hata kwa wenzetu ni kwamba mtu awe na makaazi katika *United Republic* au awe na *argent* katika *United Republic*.

Kwa hivyo, kikubwa ni kupata urahisi wa yule mtu kupata taarifa zake au linapotokea jambo kuweza kuwasiliana naye, ndio jambo ambalo limezingatiwa. Hivyo akiweko Tanzania Bara ni urahisi wa kuwasiliana naye, akiwepo Zanzibar pia ni urahisi wa kuwasiliana naye kwa sisi ofisi yetu ambayo itashughulika na masuala haya kwa hapa Zanzibar. Sasa hatutungi sheria ambayo itafanya kitu chochote kwa yule wakala akiweko Tanzania Bara, lakini ni kwamba sisi tunachotizama urahisi wetu wa kuweza kuwasiliana naye na ndio maana tukasema akiwa na *registered office* ndani ya *United Republic* tunahisi kwetu sisi ni urahisi wa kuweza kuwasiliana naye.

Lakini kwa sababu hata sheria ya wenzetu ni hivyo hivyo awe na ofisi au wakala ndani ya *United Republic* maana yake mtu yule anaweza akawepo Zanzibar au Tanzania Bara, itategemeana na sisi *aggressiveness* yetu katika kumvutia yule mtu aje awe na uwakala wa Zanzibar badala ya kuwa na uwakala au na makaazi Tanzania Bara kusema kweli. Lakini sidhani kama hilo linaathiri matumizi ya sheria hii, ni kwa njia au kwa madhumuni tu ya kuwasiliana naye si kwa jambo jengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naamini *Inshaallah* kwa sababu siku haziko mbali Zanzibar kuendesha mamlaka yake kamili, basi suala hili litapatiwa ufumbuzi. Kwa sasa hivi nakubali, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 56 Uwakala
Kifungu 57 Mrajisi kuweka muongozo

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imepitisha mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea Zanzibar, ya 2014

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea Zanzibar, wa 2014 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada katika kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi hiyo nzuri mliyoifanya na sasa tunaendelea.

Mswada wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu wa mwaka 2013

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako nisome mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu wa mwaka 2013.

Mhe. Spika, zao la karafuu ni zao lenye tija na umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Zanzibar na wananchi wake, kwani inachangia zaidi ya asilimia 60 ya usafirishaji wote wa bidhaa, *Zanzibar Export Basket*. Takwimu za zao la karafuu zinaonesha kuwa wakulima wa zao hilo wanafaidika na malipo ya ununuzi wa moja kwa moja ambao umefikia shilingi 72 bilioni kwa msimu wa karafuu 2011/2012 kwa uvunaji wa tani 4,900 kutoka tani 2,000 kwa msimu wa mwaka 2010/2011.

Kwa msimu huu wa mwaka 2013/2014 hadi kufikia tarehe 15 Januari, 2014 jumla ya shilingi 64.7 bilioni zimelipwa kwa wakulima baada ya kununua tani 4,630 za karafuu.

Mhe. Spika, licha ya kuwa na mchango mkubwa katika uchumi, uchambuzi wa mwenendo wa ustawi na uuzaji wa karafuu umebaini kuwa, zao la karafuu linakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo uhaba wa ardhi, kuzeeka kwa mikarafuu, teknolojia duni ya uzalishaji, udhaifu katika usimamizi na uuzaji wa karafuu, udhaifu wa sheria katika kuliendeleza zao la karafuu na mengineyo.

Katika kukabiliana na changamoto hizi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshachukua hatua muhimu za kukuza zao la karafuu kwa kuandaa na kutekeleza mpango wa kupanda miche ya mikarafuu laki tano kwa mwaka, kutungwa kwa sheria mpya ya Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) ya mwaka 2011 pamoja na kutekeleza mpango wa mageuzi wa miaka kumi ya shirika hilo na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu.

Mhe. Spika, pamoja na sheria ya *ZSTC* ya mwaka 2011 bado zao la karafuu linaendelea kusimamiwa na sheria ya karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985 ambayo inaonekana kupitwa na wakati, kutokana na hali ya usafirishaji karafuu ilivyo hivi sasa pamoja na ongezeko la ushindani mkali wa kibiashara katika masoko ya kimataifa siku hadi siku.

Mhe. Spika, sheria ya karafuu ya mwaka 1985 inazungumzia mambo machache yakiwemo kuipa uwezo *ZSTC* kuwa mnunuzi wa karafuu pekeyake, kuzuia uondoshaji wa karafuu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine, uzuiaji wa vifaa vya karafuu ndani, uwezo wa kufanya ukaguzi pamoja na adhabu.

Hata hivyo Mhe. Spika, sheria hiyo ina upungufu mkubwa katika masuala ya ukulima na uendelezaji wa zao la karafuu, haikuuliza masuala ya usajili, ukaguzi, uvunaji wala vipindi vya uvunaji na mambo yanayohusiana na hayo. Vile vile haikuwa na ulinzi wa mikarafuu na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya zao hilo. Hali hii imejenga haja ya kuwa na sheria mpya ya maendeleo ya karafuu itakayokidhi hali ya sasa.

Madhumuni

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya waraka huu ni kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi pendekezo la kuimarisha mfumo wa kisheria, wa kuendeleza zao la karafuu kwa kufuta sheria nambari 11 ya mwaka 1985 na kutunga sheria mpya ya maendeleo ya karafuu.

Sababu za Kutungwa kwa Sheria Mpya

Mhe. Spika, mapendekezo ya mswada yametokana na mambo yafuatayo:-

1. Kuwepo kwa vifungu katika sheria ya karafuu nambari 11 ya mwaka 1985 ambavyo haviendani na hali ya biashara ya sasa, kama kifungu Nam. 5, Nam. 6, Nam. 9 na Nam. 10 vya sheria hiyo ambavyo vimeweka masharti ya usafirishaji karafuu kutoka Pemba, vyombo vya usafiri, adhabu ya kifungo cha miaka kumi na kupanda miche mia ya mikarafuu na utozaji wa kodi zisizozidi shilingi tano kwa kilo 50 za karafuu. Utekelezaji wa masharti hayo unaendelea kuwa mgumu siku hadi siku.

2. Haja ya kuanzisha Mfuko maalumu wa maendeleo ya karafuu ili kuendeleza zao hilo na mambo mengine muhimu kwa ajili ya kilimo cha mikarafuu.

3. Uamuzi wa serikali wa kuongeza biashara ya karafuu kwa kutumia tasnia ya mali bunifu na utambulisho.

4. Mchango mkubwa wa zao la karafuu katika uchumi wa Zanzibar ambapo kwa msimu wa mwaka 2011/2012 karafuu imechangia kiasi cha shilingi 72 bilioni kwa wakulima. Mchango mkubwa wa zao hilo

katika uchumi unatoa umuhimu wa kuwa na sheria madhubuti ya kukuza zao la karafuu na kuweka ulinzi maalumu wa mikarafuu ili zao hilo liweze kuendelea kunufaisha taifa kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, utayarishaji wa rasimu ya mswada huu umezingatia uzoefu na taratibu bora za kusimamia mazao muhimu katika nchi mbali mbali duniani, hasa Malasia, Ghana na nchi za Afrika Mashariki katika kuanzia mazao kama vile kahawa, pamba, korosho, chai, mkonge na sukari.

Mapendekezo ya Muda wa Mswada

Sheria mpya inayopendekezwa kutungwa imegawika katika sehemu kuu sita na vifungu 31 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza: Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu vitatu vinavyozungumzia jina la sheria ambalo linaitwa *Clove Development Act*, kuanza kutumika kwa sheria husika, ufafanuzi wa baadhi ya mambo yaliyotumika na utekelezaji wa sheria hiyo.

Sehemu ya Pili: Mhe. Spika, sehemu hii ina jumla ya vifungu sita, vinazungumzia uanzishaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu, kazi zake pamoja na kulipa mamlaka Shirika la *ZSTC* kusimamia Mfuko huo. Lengo la kuanzisha Mfuko huo ni kuendeleza zao la karafuu kwa kukuza uzalishaji, kufanya tafiti, sensa, utambulisho wa zao lenyewe na kazi nyengine zinayohusiana na karafuu. Mfuko huu utaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa *ZSTC* na kusimamiwa na Bodi ya Shirika la *ZSTC*.

Sehemu ya Tatu: Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu kumi na inazungumzia maeneo makuu manne ambayo ni usajili, ukulima, ukaguzi na uvunaji wa zao la karafuu. Katika kupatikana takwimu sahihi kutakuwa na usajili wa wakulima na uuzaji wa karafuu kwa wamiliki wa mashamba ya mikarafuu na ardhi inayooteshwa mikarafuu kwa utaratibu utakaoelezwa katika kanuni au *regulations*. Sehemu hii pia imegusia juu ya suala zima la uoteshaji wa mikarafuu kwa njia ya asili na kudhibiti njia nyengine za ukulima wa karafuu, kutenga maeneo ya mashamba ya karafuu na kuweka ulinzi wa mikarafuu na kuipa hadhi mikarafuu yenyewe.

Sehemu ya Nne: Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu viwili, sehemu hii inaelezea udhibiti wa fedha za Mfuko ambapo umewekwa utaratibu wa kutafuta benki itakayokuwa na majukumu ya kuhifadhi fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu pamoja na kufuatilia mikopo iliyotolewa kwa wakulima.

Sehemu ya Tano: Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu vitatu na inaelezea mambo ya fedha za Mfuko ambazo ni kutoka serikalini na wadau mbali mbali pamoja na kuweka utaratibu wa uandaaji wa bajeti, uhasibu na ukaguzi.

Sehemu ya Sita: Mhe. Spika, sehemu hii ya mwisho ina jumla ya vifungu saba, inaelezea uwezo wa waziri kutoa miongozo ya kisera, adhabu, utayarishaji wa kanuni pamoja na kufutwa kwa sheria ya karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985.

Hitimisho

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupokee na kuujadili mswada huu ili kushauri ipasavyo na baadae kuridhia kutungwa kwa sheria ya maendeleo ya karafuu ya mwaka 2014. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nashukuru, mana kama msingeunga mkono hoja basi tungesema huu mswada uondolewe wajumbe hawataki ujadiliwe. Mswada umeungwa mkono kwa hivyo sasa tuujadili, nimuombe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo aje aanze kutoa mchango wa kamati.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Hija Hassan Hija (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, ifuatayo ni Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu ya mwaka 2014.

Mhe. Spika, kwanza kabisa, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Utukufu na mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kujadili Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam, 11 ya 1985, na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Pia nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada huu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati, viongozi na watendaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na wanasheria wa Baraza la wawakilishi na serikali kwa michango, miongozo na ufafanuzi wao juu ya mambo mbali mbali yaliyojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu.

Mhe. Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa wadau mbali mbali kutoka sekta ya biashara wakiwemo Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima, *ZANOP, AID NET* Zanzibar panoja na MVIWATA. Maoni na mapendekezo yao kwa Kamati yamesaidia kuufanya Mswada huu wa Sheria uwe bora zaidi kwa maslahi ya nchi yetu na wananchi wake.

Mhe. Spika, kutokana na ushirikiano na bidii kubwa ya kazi iliyooneshwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa kamati hii na Makatibu wake wakati wa kuujadili Mswada huu, napenda kuwataja kwa majina Wajumbe hao ili kutambua na kuthamini juhudi zao hizo muhimu.Wajumbe wenyewe na makatibu wao ni kama wafuatao:-

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hijja Hassan Hijja	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Abdu Haji	-	Mjumbe
4.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
5.	Mhe. Hamad Masoud Hamad	-	Mjumbe
6.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
7.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Mjumbe
8.	Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu
9.	Ndg. Fatma Omar Ali	-	Katibu

Mhe. Spika, napenda kuchuka nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na serikali kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kuleta Mswada huu hivi sasa. Ni wazi kuwa Mswada huu utasaidia sana kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika Sheria ya Karafuu ya mwaka 1985 ambayo ilionekana kutoendana na hali ya kibiashara ya sasa.

Aidha, ni jambo la faraja kuona kuwa Mswada huu utasaidia sana katika uimarishaji wa zao hili muhimu katika maeneo mbali mbali yakiwemo ya ukulima, uvunaji, uanikaji wa karafuu, uhifadhi wa mikarafuu, maeneo ya mikarafuu, pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu na kikosi kazi kwa ajili ya uendelezaji wa zao la karafuu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali kuwa, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipata fursa ya kukutana na wadau mbali mbali wa Sekta ya Biashara na Kilimo ili kupata maoni na mapendekezo yao juu ya Mswada huu, hii inatokana na fursa iliyotolewa na Kanuni ya 83(5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Miongoni mwa maoni muhimu ya wadau ni haja ya kuingizwa kwa mkopo katika kifungu cha tatu (3) kwenye ufafanuzi wa neno "Vivutio" kama ni moja

kati ya fursa muhimu ambazo Wakulima wa karafuu wanapaswa kufaidika nazo ili kuweza kuwaendeleza. Aidha, katika kifungu cha 10, wadau waliona haja ya kuwepo kwa ufafanuzi zaidi wa kazi za daftari la usajili wa wakulima wa karafuu, namna litakavyofanya kazi na wakati ambao wahusika watatakiwa kujisajili.

Mhe. Spika, kutokana na kubainika kwa mapungufu kadhaa ya msingi ya rasimu ya mwanzo ya Mswada huu yaliyopelekea haja ya kufanyiwa marekebisho mengi na ya msingi, serikali iliona ni vyema kuuchapisha upya Mswada huu. Katika kufanya hivyo, serikali iliona pia ni vizuri kuyazingatia kabisa maoni ya Kamati na baadhi ya maoni ya wadau katika Mswada huu uliochapishwa upya ili kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi na kurahisisha mjadala wa Mswada huu katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika. hata hivyo**,** baada ya Mswada huu kuchapishwa upya, Kamati ya Fedha, Bishara na Kilimo imekutana tena na wizara kwa ajili ya kuupitia kwa kina mswada huu. Ambapo kimsingi ilikubalina na mapendekezo ya mswada huu.
Hata hivyo, kwa kuzingatia maoni ya Wajumbe wenyewe wa kamati, Kamati yetu ilipendekezwa baadhi ya maazimio ya kimsingi na ya kimaandishi, baadhi ya mapendekezo hayo ni kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza katika jina la Mswada huu, Kamati ilipendekeza marekebisho hayo ya jina la Mswada huu lisomeke. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu namba 11 ya mwaka 85 na kuweka sheria mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo yanayohusiana na hayo.

Aidha, katika kifungu cha tatu kinachoelezea tafsiri, kamati imependekeza kuongeza kwa tafsiri ya neno shirika ambalo halikutolewa tafsiri yake ndani ya mswada huu. Hivyo kamati inaona tafsiri ya neno shirika liwe Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar liloanzishwa chini ya Sheria namba 11 ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, ili kuepusha mgongano wa majukumu katika Bodi ya Shirika la Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lililoongoza mfuko wa maendeleo ya karafuu. Kamati inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 6 na hivyo isomeke:

"Mkurugenzi Mtendaji ndie atakaekuwa mtendaji mkuu wa mfuko"

Mhe. Spika, kwa kuwa kifungu cha 18(2) kimejitokeza tena katika kifungu cha 18(9) hivyo kamati imependekeza kuwa kifungu cha 18(2) kifutwe.

Mhe. Spika, kamati pia imependekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 26(2) kinachotoa uwezo wa fedha zote zinazotakiwa kutoka na malipo ya adhabu kuingizwa katika mfuko wa Maendeleo ya Karafuu, kwa vile sheria haikuweka wazi fedha hizo zitakwenda wapi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 19(1) kinatamka kuwa:

"Mtu atakaetaka kuhamisha karafuu kutoka sehemu moja kwenda nyengine kuomba kibali kwa Sheha kitakachokuwa katika fomu maalumu"

Kamati inaitaka serikali kuhakikisha kuwa vibali vyote vinavyotakiwa viwe kweli vinapatikana kwa Sheha. Kwa kuwa imebainika kuwa baadhi ya Masheha huwa hawana vibali hivyo na badala yake vibali hivyo hutolewa na watu wengine kinyume na utaratibu unavyoekeleza na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 20 ambacho kinatoa uwezo wa Bodi ya Kurugenzi ya Shirika la ZSTC, kuchagua benki kwa ajili ya utoaji wa huduma ya usimamizi wa fedha za mfuko wa maendeleo ya karafuu, zinazotumika kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wa karafuu. Tunasisitiza juu ya haja ya kuwepo kwa umakini mkubwa katika utekelezaji wa suala hili. Kamati inashauri kuwa vigezo vinavyowekwa kwa ajili ya wakulima wa karafuu kupata mikopo hiyo, imelenga kwa ajili ya kuwanufaisha wakulima hao na sio kuwaumiza. Hivyo, ni vyema vigezo hivyo visiwe vigumu ili kuwalinda wakulima waweze kurejesha mikopo hiyo bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yakiwemo ya kimaandishi na uchapaji yameshachukuliwa na wanasheria pamoja na makatibu wetu wa kamati. Inavyoonekana katika karatasi ya mapendekezo na marekebisho ya kamati.
Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaunga mkono mswada huu na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote waungane nasi kwa kutoa maoni kadiri inavyoonekana inafaa na hatimae kuunga mkono na kupitisha mswada huu kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya naomba kuwasilisha na naomba unipe nafasi fupi kabisa nitoe mchango wangu kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Spika, mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani naomba nigusie maeneo yafuatayo:-

Kwanza kabisa nichukuwe nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko, kwa kuonesha nia ya umakini. Mhe. Spika, Wawakilishi wamekuwa wakipima serikali kupitia wizara mbali mbali. Ndani ya kipindi cha miaka mitatu wizara hii chini ya Mhe. Waziri na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wametuletea miswada 5.

Mswada wa mwanzo ambao wizara hii wametuletea ni Mswada wa Sheria ya Viwango ya mwaka 2011, Mswada wa Sheria ZSTC mwaka 2011, Sheria ya Biashara na Sheria ya Leseni ya mwaka 2013 na leo mwaka 2014 tuna Sheria ya Mfuko wa Karafuu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nachukuwa nafasi hii kuipongeza sana wizara na watendaji wote kwamba wamekuwa makini kuleta miswada ambayo inawagusa watu na inaleta manufaa makubwa kwa wananchi wetu wa Zanzibar na hii ni dhahiri kwamba kumbe serikali ikiamua inaweza.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa niende kwenye kifungu cha 5 (j), hiki Mhe. Spika, kazi moja ya mfuko ni kusaidia gharama za matitabu na huduma nyenginezo za Bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shuhuli za uchumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, nachukuwa nafasi hii kuwapongeza sana wizara, leo ukiangalia tafiti takribani kila mwezi si chini ya watu 10 wanapata madhara kutokana na uchumaji wa karafuu. Ama wanaanguka au kufariki. Leo serikali imeona haja sasa ya kuweka huduma za matibabu na bima kwa wachumaji na wakulima wa karafuu kwa ajili ya kuwasaidia.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nawapongeza sana wizara kwamba serikali imeona umuhimu wa hili tunalolizungumza hapa, basi tayari jana, juzi na leo watu wameanguka na kufariki. Kwa hivyo, kifungu hiki cha kulinda Bima na matibabu ya wafanyakazi wa mikarafuu nadhani ni jambo la kupongezwa, na mimi nachukuwa nafasi kuwapongeza sana Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho ninachotaka kuchangia ni cha 13, vitendo vinavyokatazwa katika kilimo cha mikarafuu. Mhe. Spika, kifungu hiki kimeweka adhabu kwa wale ambao watachoma, watakata na kuharibu mikarafuu. Sasa hawa ni watu karibu makundi matatu. Liko kundi ambalo limekata mikarafuu kwa mazoea tu, kwa mfano wananchi wetu vijijini huko wanaona mkarafuu ni nyenzo ya kujengea nyumba zetu, wamekuwa wakikata mikarafuu kwa madhumuni ya majengo na huduma ndogo ndogo.

Sasa niiombe serikali itoe elimu, kwa sababu kifungu cha 13 (5) kimesema wazi kwamba mtu ambae atafanya kosa hili adhabu yake ni jela miaka mitatu au faini milioni tatu. Naomba kuchukuwa nafasi hii Mhe. Spika, kuwanasihi sana Wazanzibari wenzangu kwamba tuondokane na mazoea, sasa mkarafuu ni mali na ni hazina na tabia ya kukata kata basi naomba tuiache.

Pia kwa wale waliokuwa wana tabia ya kuhujumu mikarafu, kuna watu wanakata mikarafuu kwa misumeno wanaona muda wa kuiba karafuu hawana wanaona bora waukate mkarafuu kwa ajili ya kufanya huduma za wizi. Nawasihi waache mara moja.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono sana kifungu hiki kwamba wale wanaohujumu mikarafuu, wanaikata kwa njia ya wizi basi adhabu hizo za miaka mitatu na milioni tatu ni adhabu muafaka na naomba Wawakilishi wenzangu tuziunge mkono. Kwa wale waliokuwa wana mazoea ya kutumia kama nyenzo ya ujenzi basi naomba wizara ichukuwe juhudi za kutoa elimu na kuwaelimisha wananchi wetu kwamba kifungu hiki kimelinda mkarafuu kwa nguvu zote.

Lakini Mhe. Spika, kifungu hiki pia kitaondosha ule udhaifu wa serikali. Serikali wanapoamua kujenga barabara, miundo mbinu ya umeme na maji basi wamekuwa wakikata mikarafuu bila hata fidia. Sasa kwa kifungu hiki Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Nishati, Wizara ya Maji ikiamua kupitisha njia kwenye mashamba ya mikarafuu, watakua na tahadhari.

Mhe. Spika, nataka nitoe maoni yangu katika suala zima la kifungu cha 18(3). Mhe. Spika, kila mkulima, mmiliki na mkodishwaji wa mikarafuu ambae atakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji karafuu atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo:-

Mhe. Spika, sheria hii inavitambua vifaa vifuatavyo kama ni vifaa vya kuanikia karafuu. Kwanza vifaa vya kuanikia, na vya uchumaji. Lakini wananchi wengi wamekuwa wakitumia nyumba za mabati kuanika karafuu. Kwa mujibu wa sheria hii sasa mabati hayatakuwa kifaa halali cha kuanikia karafuu.

Naiomba Wizara ya Biashara itoe taaluma kwa wananchi wetu kwamba sasa mapaa ya nyumba kwa maana ya mabati sio kifaa muafaka cha kuanikia karafuu na hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria hii. Naiomba sana wizara itoe taaluma hiyo na itoe nyenzo kwa wananchi wetu ili wasiingie hatiani pale ambapo watafanya mambo kwa mazoea.

Mhe. Spika, kifungu cha 19(1) mtu yeyote ambaye atakusudia kuhamisha karafuu kavu au mbichi au makonyo ya karafuu kutoka sehemu moja au nyengine anatakiwa kuwa na kibali cha Sheha.

Mhe. Spika, kamati yangu imeeleza wazi na mimi nasisitiza kwamba wako Masheha wanajisahau. Kwa mfano yako maeneo ambayo hayana karafuu, kwa mfano Mwambe, kwangu mimi hakuna mkarafuu. Lakini wakulima wa Mwambe wana mikarafuu yao Ngomeni na sehemu nyengine za Chake Chake. Sasa Sheha wa Mwambe kwa sababu hakuna karafuu anajisahau vyeti au fomu za kuhamisha karafuu hana. Naiomba serikali kila Sheha popote alipo Zanzibar basi apatiwe fomu na vyeti vya karafuu kwa ajili ya kulinda maslahi ya karafuu. Vyenginevyo tukimuachia mtu ambaye hana mkarafuu pengine Tumbatu, na Sheha hana kibali cha karafuu basi wahalifu wanaweza kupeleka Tumbatu karafuu na itakuwa ni mwanya wa kuvujisha karafuu.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho nasisitiza ni usimamizi wa mfuko, kwamba sasa mfuko utachagua benki ambayo itakuwa ni dhamana ya kutoa mikopo kwa ajili ya wakulima wa karafuu.

Mhe. Spika, kifungu cha 20 naiomba serikali itafautishe benki hii iwe ni tofauti na ile Benki iliyotoa mkopo wa JK na AK. Kamati yangu ilipokuwa inafuatilia madeni, wananchi walikuwa wanatwambia kwamba hii ni pesa ya ruzuku.

Sasa naomba Mhe. Spika, benki hii iwe makini na iondeshe upendeleo. Fedha hii isijekuwa fedha ya kisiasa, isijekuwa ni fedha ya kupendelewa na muwaambie wananchi kuwa fedha hii ni ya mkopo na isiwe ni sadaka. Mfuko wa AK na JK kwa kweli ulikuwa ni sehemu ya sadaka na wananchi wengi waliopewa fedha ile ilipotea kwa sababu hatukuwaelimisha wananchi kulinda fedha za serikali.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nishauri kwenye kifungu cha 26-27 kwamba serikali iweke wazi, kwa mfano naomba kunukuu Mhe. Spika:

"Endapo kosa ndani ya sheria au kanuni yoyote iliyofanywa na sheria hii imefanywa na wakala au muajiriwa wakati huo au kiongozi au muajiriwa atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia ataadhibiwa ipasavyo"

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri labda atuweke sawa aadhibiwe ipasavyo vipi, kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria hii au vipi. Maana ipasavyo ni neno ambalo limejifumba, naomba liwe wazi ili lisilete mwanya watendaji wa mfuko kufanya kosa ambalo litaathiri mfuko wetu.

Kwa ujumla Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kiwani, sheria hii ni nzuri na lengo la sheria hii ni kulinda mikarafuu na wachumaji wa karafuu. Lakini nasisitiza kwamba elimu itolewe hasa kwa wananchi ambao wamezoea kutumia mkarafuu kama nyenzo ya kujenga nyumba zao. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kama kawaida yako na mimi kuniona mapema ili niweze kutoa fikira zangu katika mchango huu.

Mhe. Spika, sitofanya dhambi hata siku moja na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atajaalia iwe hivyo.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu na Wakurugenzi wote pamoja na wanasheria wao.

Mhe. Spika, kama kuna medali ya dhahabu basi wizara hii ya mwanzo kabisa iweze kupewa medali hiyo. Kwa sababu mara nyingi sana husema sheria jamani zibadilishwe zimepitwa na wakati, basi kumbe wizara hii Waziri na Naibu wake, katibu wao pamoja na watendaji wao kumbe wananisikiliza sana na wanatuelewa nini tunachokisema Wawakilishi wao humu ndani ya Baraza. Nashukuru sana Mhe. Spika, na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atawapa kila la kheri na wao atawasaidia.

Mhe. Spika, nitoe mifano Mawaziri igeni hapa si dhambi hiyo ukweli tuuseme, ananitizama sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kusema kweli Sheria zenu sasa hivi zibadilishwe. Leo anakamatwa mtu na silaha Zanzibar anatoa laki tano anapewa mtu dhamana. Sasa hiyo si kupitwa na wakati sheria?

Mhe. Spika, *message* imefika nilikuwa na lengo hilo la kumfikishia Mwanasheria kwa sababu inauma sana mtu anakamatwa na bastola anakwenda dhamana ili kesho akatafute bastola nyengine aje hapa Zanzibar. Maana hapa wamefanya kama shamba la bibi sasa hivi.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye mswada wenyewe, tuna nia nzuri ya kutaka kufanya zao la karafuu kulifanya kuwa ni zao la kitaifa. Na ni kweli hasa na nimeamini hivyo kwa mkakati huo ninaamini sasa Zanzibar umasikini huo unapotea, sina wasi wasi.

Mhe. Waziri namuomba sana Mwanasheria huyo aliekutungia hivi vitu basi si vibaya na mimi ukanionesha nikapata kugema kwake, kwa sababu kaweka vitu ambavyo vizuri hata Mhe. Hija Hassan Hija kwa kuwa yeye anasema ndie mchangiaji zaidi leo kachangia vizuri kaikubali, basi nashukuru sana.

Mhe. Spika, nikianza na ukurasa wa 369 katika kifungu ambacho kinasema:

"Kikosi Kazi" maana yake ni kikosi kazi cha watu maalum kilichoundwa chini ya kifungu cha 7 na sheria hiyo"

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nayo sheria hiyo, lakini ningeomba ikiwezekana sitaki nitoe kasoro kama nilivyosema na mimi nataka nitoe ziada yangu tu. Mhe. Spika, kikosi hiki kiwe kinapewa motisha kila baada ya muda fulani na mara nyingi sana wanafanya kazi nzuri sana kikosi hiki, kwa sababu hawa ndio wakombozi.

Mhe. Spika, ukurasa huo huo kifungu cha 4(1) kinasema:

> "4(i) Kuanzishwa kwa Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu."

Mimi nakubaliana nalo, sina tatizo kabisa na nakiri kukubali mfuko huo uwe chini ya dhamana ya bodi, kwa sababu bodi ndio itakayokuwa na mamlaka hiyo kwa mujibu wa sheria hii ya kusimamia mfuko huo. Lakini twende vizuri mfuko wetu, tuuenzi vizuri asijeakaingia panya akaudokoa.

Lakini vile vile kifungu 5(a) kinaseama:

> "5(a) Kuimarisha na kueneza upandaji, uzalishaji, majaribio na uchunguzi unaohusiana na maendeleo ya karafuu."

Mhe. Spika, kuimarisha ni suala ambalo ni muhimu sana. Lakini Mhe. Spika, tutumie *modern step* kwa kuwa sasa hivi tumekwisha kusudia hasa si vibaya tukafanya *special day.* Naomba sana Mhe. Waziri tenga bajeti yako wala usione tabu tuwakusanye wazalendo wa Kizanzibari aliyekuwa na shamba, asiyekuwa na shamba twende tukapande hii mikarafuu.

Si vibaya ndio lengo tulilolikusudia hilo. Hapa ndio tutakuwa na lengo zuri sana Mhe. Spika, tuwashajihishe vijana na askari wetu wa vikosi na kila aina ya mtu anaemjue yeye ambae zao hili litakuja kumsaidia mbele ya safari.
Kutoa misaada ya kifedha ili kuwahamasisha wakulima, hili hapa ndio umeuwa. Hapa sasa si mchezo mkulima leo anapewa mpaka motisha ya fedha. Mhe. Spika, hii furaha yangu nitashindwa hata kuuchangia kwa sababu ni suala ambalo kweli sasa hivi tumekusudia si kitu cha mchezo.

Vile vile Mhe. Spika, kifungu cha 5(f) kinasema:

> "5(f) Kusaidia shirika kama ni mnunuzi wa mwisho wa karafuu endapo bei ya karafuu itaanguka katika soko la dunia."

Sasa huyu mkulima hapati shida tena anakuja bei yake ni ile ile. Sasa hapa nani atakubali kubeba mzigo. Lakini nyinyi mmekubali kutokana na mazingira ya kumsaidia mkulima. Hili mimi nakubaliana nalo sina pingamizi nalo kabisa.

Lakini 5(g) kinasema:

> "5(g) Kutoa usaidizi katika vipaumbele vya shughuli za uzalishaji wa karafuu."

Haya ni mambo ambayo Waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi walikuwa wakiyasema. Lakini hapa mimi naongeza langu dogo tu. Ongezeko langu sasa hivi tufanye kama vile mechi, ili tuwe tunatoa *special* zawadi au *certificate* kubwa ya mkulima wa karafuu kwamba amefika viwango vya uoteshaji au vya uvunaji. Ili aweze kutambulika ndani ya ulimwengu huu na kuoenesha jinsi gani wizara inavyowajali watu wake.

Mhe. Spika, hapa ndio zaidi kifungu cha 5(i) kinasema:

> "5(i) kuweka daftari la usajili wa wakulima."

Lakini mimi nataka kushauri hapa, katika daftari hili mkodishwaji asiwemo, yule mpita njia tu kwa nini umsajili. Mimi naomba yule yule mwenye shamba aendelee kuwa ni msajili.

Hii 5 (j) inasema:

> "5(j) Kuwasaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu".

Hapa natoa rai, kulikuwa na vituo maalum kwenye mashamba kwa mfano kama shamba la Kinduni, kulikuwa na mabwana shamba tena wataalamu na watibabu, kwa hivyo naomba warejeshwe, isijekuwa huyu yuko mjini mkulima akamtafute.

Nakwenda ukurasa wa 371 katika kifungu 10(2) kinasema:

> "10(2) Kila mkulima wa karafuu, mmiliki, mkodishwaji, muuzaji au watu wengine wanaohusuka na karafuu watapaswa kusajiliwa na mfuko"

Mkodishwaji atapata kusajiliwa kwenye mfuko ndio maana nikakwambia tizama huko tunakwenda mbele ina maana huyu mwenye mali amekwisha kwa sababu yule anamkodisha mtu kwa muda, akimaliza zao ndio anapata ile

haki yake. Sasa hapa ndipo niliposema tutoe elimu na tusione tabu. Hili sasa tunakwenda kwenye utajiri na katika utajiri kwenye sheria lazima tuwe makini sana hapa. Mhe. Spika, kuna wajanja humu wanasoma sheria vichochoroni. Sasa mimi naomba sana Mhe. Spika, isije kuwa sheria yako nzuri baadae ikageuka ikawa mbaya.

Nikiendelea Mhe. Spika, nakubaliana nae Mhe. Waziri, zamani walikuwepo hawa watibabu. Lakini walikuwa labda wamekosa hii taaluma ya uchunguzi wa kuujua na kutoa kinga ya hayo maradhi yaliokuwemo kwenye mikarafuu. Ilikuwa zamani hakuna maradhi na nashukuru sana kuwa sasa umetuwekea hiyo, kutakuwa na uchunguzi na kinga ndani yake. Hili mimi nakubaliana nalo kabisa.

Lakini sasa zoezi hili tuwachukuwe wananchi kwa kila wenye mashamba, kwa hiari, twende tukawape taaluma na wao wajue kuwa tatizo hili la mkarafuu ukiona unasinzia, haraka sana tuweze kufanya uchunguzi kwa kupitia taaluma fulani ili kuweza kuukinga baadae asije kula hasara.

Mhe. Spika, ukurasa wa chini yake wa tatu, huo mfuko utaendelea na bajeti yake kila mwaka. Mhe. Waziri tunaomba sana mfuko wako huo uwe mkubwa, kama unaingia kwenye Baraza letu mfuko huo au bajeti hiyo, itakuwa ni *special* kwa wizara yako tu. Ukija kwetu tuko tayari kukupigia debe uwe mfuko mkubwa. Kwa sababu lengo lako ni zuri sana kuliko watu wanavyolitizama.

Mhe. Spika, nikiingia ukurasa huu wa 373 hapa inasema hii:

> "Inakatazwa mtu yoyote kufanya jambo lolote kati ya yafuatayo kwenye shamba ya mikarafuu
> (a) Kuchoma au kutengeneza makaa "

Mhe. Spika, hapa tutengeneze sheria kali, wako watu waharibifu nakubaliana nalo hilo. Zamani karafuu watu walikuwa wanaficha kwenye mapolo, watu wakivuusha kimagendo. Mhe. Waziri usikubali kibali cha aina yoyote cha kumpa mtu aweze kwenda kukata mkarafuu, ukitoa na ukiridhika na kuambiwa mkavu basi itakatwa mibichi mitano.

Naomba hapa sheria yako iwe kali sana usimuone haya mtu sasa hivi utajiri huo, tunakosa mafuta tunapata karafuu, si jambo la mchezo hilo.
Nikingia hapa kifungu cha (3)

> "(3) Mtu yeyote ambaye anakusudia kukata mkarafuu kwa madhumuni ya shughuli za maendeleo atatakiwa kuomba kibali".

Hiki kikatae wewe Mhe. Waziri, kibali cha nini, neno kibali futa, ukiridhia hii itakuwa hatari. Tamka sheria mtu hakuna ruhusa kukata mkarafuu, eka hiyo ni sheria.

Mhe. Spika kifungu cha 14(1)

> "14(1) Kwa masharti ya Sheria hii, na kwa sharti mpango wa matumizi wa ardhi"

Sasa hapa kidogo nataka nijiulize huku tuna sheria ya ardhi na wewe unaingia katika ardhi hebu tuelezeni sasa zile heka zote au mashamba yote utakabidhiwa wewe. Mimi naomba jibu kwa Mwanasheria niweze kufahamu vizuri.

Wewe unaitaka karafuu, lakini karafuu imo ndani ya ardhi, lakini na wewe unaitengenezea sheria hii kwenye ardhi iwe una mamlaka hapo. Sasa ningeomba sana Mheshimiwa wangu hebu hii niweke sawa utakapokuja kunisaidia ili na mimi niweze kukuchangia vizuri sana.

Lakini kifungu cha 18 kutakuwa na msimu wa zao la mwaka, msimu wa zao la vuli, kwani misimu ya uchumaji wa karafuu wa kila mwaka, kila mkulima mmiliki anakodishwaje mkarafuu ambaye anakusudiwa kuchuma au kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji wa karafuu na atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri, labda twende na *models* sasa hivi, kwanza tumrahisishie kama kutakuwa na mashine ya uchumaji ambayo wewe utachagua pevu. Mimi naomba sana Mheshimiwa twende na wakati. Kama sheria unavyozibadili Mheshimiwa na tubadili na mfumo wa uchumaji. Hapa ukichuma watu wengine wanaiharibu wanaiua. Basi tuwatafutie wananchi wetu mashine ambazo zitaweza kuchagua hii changa, hii pevu na zipo sana, nipe tenda mimi uone kama sijakuletea.

Mhe. Spika, hiyo ningeomba sana kuwa Waziri aangalie kwa sababu watu wengine wanakuwa na kingoe kirefu, sasa akikata ile inakuwa inakufa. Kwa hivyo, tuwatafutie *model.*

Lakini vitu ambavyo vya kukaushia Mhe. Spika, mara nyingi sana inakuwa yale majamvi niseme sehemu nyengine za mashamba huko wanakuwa hawapati kwa wakati wanachelewa. Mimi ningeomba sana wapatiwe kwa wakati vile vifaa, zamani wakipata majamvi, karabai.

Mhe. Waziri, nataka ujiandae kweli si kitu cha mchezo sasa hivi, maana yake ujiandae hasa, *serious* kabisa. Kwa sababu hili zao ambalo ndilo lililotupatia

uchumi wa Zanzibar, ndio uchumi wetu hasa, hawa wengine wote wanajaribu tu, lakini sisi ndio tuna *quality* ya karafuu yenyewe ya Zanzibar. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri, kwamba tujaribu kufanya njia hizi ili kuweza kuwasaidia wananchi.

Kifungu cha 19 kimezungumzwa na mwenzangu, hapa Mhe. Wazir, ndio unapoanza kunyang'anywa mali na ndio maana nikasema kuwa tungekuwa na kituo maalum maana yake unajenga nyumba ambayo hiyo itaweza kuwakusanya watu wa Shehia ya Kinduni mfano. Ungekuwa na uwezo huo Mhe. Waziri, najua sasa hivi uwezo huo huna, lakini *inshaallah* Mungu atakupa uwezo, iwe hapa tena asitafutwe mtu wa Mahonda, zikatwe katwe zikapimiwe Mahonda hapo ndio tunaponyang'anywa.

Mimi nafikiri tungejaribu kutafuta mbinu mbadala ili uweze kufanikisha hili lengo lako ulilokusudia vizuri zisiibiwe zisichupe chupe hizi karafuu. Mhe. Spika, zikichupa chupa ndio tunapoibiwa hapa ukweli tuseme huo. Ukiruhusu tu karafuu ikaanikwe Mahonda kutoka Kinduni, Mheshimiwa wewe sema hapo gunia mbili tatu unakwenda kuzihesabu kule unakuta pungufu watu wameshachukua. Naomba sana Mhe. Waziri, uangalie sana hapo kukubali kutoa kibali cha kwenda mji hadi mji kwa kwenda kuanika. Ujanja tu nao ule Mheshimiwa, popote jua lipo la Mwenyezi Mungu asikudanganye mtu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 375 hapa kidogo naomba Mhe. Waziri, anisaidie anasema "Inakatazwa kwa mtu yeyote isipokuwa Shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala na sehemu nyengine".

Mheshimiwa, kwa muda gani? Tunaomba sheria uiweke sawa hapo kwa sababu mimi naweza nikaweka karafuu mwaka hadi mwaka ndani. Sheria inaniruhusu hivyo? Ndio mapungufu ya sheria sasa hapo inapoanzia. Hebu liangalie Mhe. Waziri hili, tutoe *deadline*, tunasema msimu ukisha tu mtu tukimkuta na punje ya karafuu tia ndani usifanye mchezo.

Naomba sana Mhe. Spika, hili kwa sababu wamejitahidi kuongeza bei kubwa wala hawatozwi kodi, wao walete karafuu zao tu halafu ndio wakae ndani Mheshimiwa. Naomba hapa anitafutie *space* ya kuongeza Wanasheria.

Mhe. Spika, ukurasa huo huo kifungu cha 20 hapa mimi nakubaliana nalo sana, benki itakuwa na majukumu hayo. Lakini sasa Mhe. Spika, hapa nataka nikwambie hasa, hebu tuwatafutie njia mbadala pamoja na kuwa nyinyi benki ambazo zitakuwa kwenye *control* ya bodi ili kuwasaidia wakulima wetu. Sasa hapa ndio maana nikasema mfuko ule ikiwa utamkuta mkulima hakodishi tena.

Sasa mimi naomba tujaribu sana katika kuwajengea uhai kwa kuwapatia fedha za mikopo hawa wakulima, basi iwe mara moja kwa sababu asishawishike tena kukodisha. Kwa sababu kuna wengine wanakodishwa waharibifu, wanataka mpaka kileleni waipopoe kwa jiwe ile. Sasa utakuta anamuulia mwenzake mkarafuu. Kwa hiyo, kampeni iwepo Mhe. Waziri, ili mtu aweze kukubaliana na suala hilo.

Lakini chini hapa kifungu cha 22 (1) (b) michango kutokana na wakulima, wadau wengine wa karafuu ili kutunga sheria hii. Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo ruzuku ya michango yote itakayotolewa kwa mfuko ndio kama nilivyosema mwanzo nilisifu sana kutokana ruzuku hizi zitatoa changamoto nzuri sana. Lakini fedha zozote zinazotokana kwenye soko la mali na ubunifu na mirahaba au haki nyengine zozote, mapato yatakayotokana na vitega uchumi na mambo mengine. Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kuwa haya mambo kweli mwaka huu wamekusudia kuwa karafuu iwepo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ukurasa wa 26, mtu atakwenda kinyume na masharti ya sheria atafichua siri na utaratibu wa mfuko kwa asiyehusika atawekwa hifadhi kwa kumzuia. Mhe. Spika, hii mimi nakubaliana nayo, lakini kwa hukumu yake milioni moja bado ingali tunatania sheria. Ningeomba nayo hii tuweke mkazo sana, kisia Mhe. Waziri, si mchezo kwa sababu ni lengo la kutaka kuweka sheria yako iwe nzuri na ulinzi wa hizo karafuu zenyewe.

Mhe. Waziri, naomba sana hilo suala ulikubali na uangalie vipi hizi athari, lakini kwa kosa la shilingi milioni moja ni utani hili tukubaliane nalo. Kwa sababu si mchezo wewe umekusudia kutaka kuuondoa umaskini, basi usione tabu hata kuweka sheria kali kwa kuwa ni zao ambalo linatakiwa.

Mhe. Spika, nimalizie eka zinauzwa sasa hivi za mikarafuu na watu wanakuwa na namna mbili, aidha wanataka kujenga kitu cha maendeleo ni sawa. Lakini je, tuulize hii karafuu si ya maendeleo, si ya kuleta uchumi. Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri, haraka sana ashirikiane na Mhe. Waziri wa Ardhi azuie. Sasa mle watu hawauziani sehemu ambayo iliyokuwa na minazi mitupu, wanauziana ndani ya mikarafuu sasa hivi.

Naomba sana Mhe. Spika, eka zile sasa hivi zizuiliwe wapewe wenyewe wananchi waliouza, ndio bahati mbaya wameshauza wameshakosa neema hii, maana yake hii neema hawaijui, sheria hii kama sasa hivi itawasaidia. Naomba sana Mhe. Spika, sasa hivi *full stop* mtu yeyote kuuza eka tunataka kupanda mikarafuu, tuwe *serious* nalo suala hilo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia Mhe. Waziri, alitunga sheria ya masuala ya vyakula. Mhe. Spika, sheria ile ni nzuri sana, lakini iko *very slow.* Mhe. Spika, vyakula tunakula vibovu, tusifichane Mhe. Waziri, sheria uliileta wewe na niliiunga mkono sana. Kama sheria hii nakuunga mkono wala sikupunguzii senti hapo, nakuunga mkono tu. Lakini naomba Mhe. Waziri, sheria zao zinakaa kitako, sheria zinataka mtendaji. Hebu tuone yale makeke yako kama unavyotuletea hizi sheria, sheria hazikai ndani ya *briefcase.*

Tatizo tunatunga sheria, lakini hatimae zinakaa kwenye mkoba, wananchi wanateketea sasa hivi kwa vyakula vibovu. Naomba sana Mhe. Waziri, sheria yako hii ifanye kazi wasituharibie watu, hawawezi wakae pembeni wapo watu wanaweza kufanya kazi, watoto wapo kibao wanazurura mijini huko, wana diploma, wana *form VI* wachukueni hawa waingizeni watafanya kazi.

Naomba sana Mhe. Waziri, hii ni *message* nimekuwekea maalum ya kumalizia kuwa sheria zako ni nzuri, lakini watendaji wana-*delay time* kuzifanyia kazi. Sijasikia hata siku moja mtu ambaye kakamatwa na magunia kumi ya michele mibovu, imezamishwa. Hata kama wapo,lakini anakuwa ni mmoja tu, ni wale wale wa siku zote. Mhe. Waziri, usikubali kabisa sheria zako zikachezewa.

Mhe. Spika, naunga mkono kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa kuwa tuna mikarafuu mingi kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inaturuhusu.

Mhe. Spika, vile vile, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika sheria hii ya kuanzisha Sheria mpya ya Maendeleo ya Karafuu.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu hautakuwa mkubwa nitajikita katika maeneo manne, lakini ambayo yanakidhi haja.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na Naibu Wazir na watendaji wake kwa kutuletea sheria hii ambayo niseme ni mkombozi wa wakulima wa karafuu pamoja na wachumaji wa karafuu na watu wengine wanaojishughulisha na mambo haya.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nianze katika kifungu cha 4 (1) naomba kunukuu kinasema kunaanzishwa mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Maendeleo wa Karafuu. Mhe. Spika, mimi kifungu hichi nakipongeza kwa

nguvu zangu zote kuweza kuanzishwa mfuko huu ambao utakuwa ni mkombozi kama alivyozungumza kwa wakulima wa karafuu pamoja na wachumaji wa karafuu.

Lakini nikiendelea na mchango wangu, niende katika kifungu cha 5 ambacho kinasema kazi ya mfuko itajumuisha shughuli zifuatazo. Sasa nitajikita katika kifungu (c) naomba nikinukuu kwa ruhusa yako kinasema;

"Kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu"
Mhe. Spika, katika uchumaji wa karafuu kama alivyozungumza Mhe. Hija Hassan Hija, pale kunatokea madhara sana ndani ya wachumaji wa karafuu ikiwemo kuanguka mkarafuu siku hadi siku ambapo zao hili linaendelea kuchumwa.

Naomba nitoe mfano ulio hai, juzi tarehe 14/12/2013 kuna kijana mmoja mwanamke kaanguka mkarafuu sehemu za Piki, kwa bahati mbaya kaumia vibaya sana na akapelekwa hospitali ya Wete akafanyiwa uchunguzi wa *x-ray*, baadae kahamishiwa Mkoani. Kufika Mkoani kalala siku moja, siku ya pili yake kahamishiwa kwenda hospitali ya Muhimbili kwa matibabu. Lakini jambo la kusikitisha na la huzuni huduma kubwa aliyoipata ya bure ni kutoka pale hospitali ya Mkoani kwenda bandarini kuingia ndani ya boti kwa ajili ya usafiri kwenda mbele ya safari Muhimbili. Hata si vibaya kama nitamtaja kwa jina, nisimtaje.

Mhe. Spika, kama alivyozungumza mwenzangu pale Mhe. Hija Hassan Hija, kuwa siku hadi siku watatu, wanne wanaanguka mkarafuu. Na kwa sababu ya mfuko huu ulioanzishwa itakuwa ni ukombozi, kama ni ukombozi basi sheria iweke wazi namna gani mtu anayeanguka mkarafuu atahudumiwa. Bila ya hivyo, basi itakuwa madhara kama hayo yanatokea ni kuwakatisha watu tamaa. Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri, awe makini sana katika mfuko huu. Na huu mfuko watu wanaweza kuumia, lakini kama mtu hana mtu wake anayefanya kazi pale atakosa huduma zinazopatikana na wakapata wengine ambao hawana madhara makubwa.

Hili liangaliwe kwa kina, hii tumezoea hata ukiangalia kule kwenye mambo ya uvuv, basi kuna wavuvi wanaosaidiwa kwa kujuana tu ambao si wavuvi. Na sheria hii isije ikawa hivyo lazima iangaliwe vizuri sana.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nasema kama hapa wajikite sana katika eneo hili. Si huyu tu hata juzi Mwambe, mtu mmoja kaanguka mkarafuu nae kaumia vile vile. Sasa nataka Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atufahamishe huko nyuma ilikuwa watu wanaoanguka mikarafuu na kupata

maumivu makali, walikuwa wanahudumiwa vipi kabla ya mfuko huu toka kuanzishwa au ilikuwa vipi. Aje atupe maelezo zaidi ili tufahamu. Kama kulikuwa na huduma, basi hawa walioanguka wapatiwe huduma ili tupate kuendelea na baadae wanufaike na mfuko huu ambao utaanzishwa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu naelekea katika ukurasa wa 373 kifungu cha 13 (1).

Mhe. Spika, naomba uniruhusu ninukuu kifungu hichi kama kinavyosomeka"Inakatazwa kwa mtu yeyote kufanya jambo lolote kati ya yafuatayo kwenye mashamba ya mikarafuu;

(a) Kuchoma au kutengeneza makaa,
(b) Kuchimba mawe, udongo au mchanga, na
(c) Kuangusha, kung'oa, kukata, kuharibu au kuathiri mkarafuu na mambo mengineyo.

Mhe. Spika, kifungu hiki ni kizuri sana, haya makatazo ni mazuri sana. Kwa sababu tunapokata miti kwa ajili ya kufanya mkaa wa mkarafuu tunaumiza mkarafuu, hatima yake hata hatutoiona tena hiyo mikarafuu. Lakini vile vile, katika kuichimba ni kuiathiri vibaya sana. Kwa hivyo, mimi naunga mkono kifungu hiki kitiliwe mkazo zaidi na hukuma iliyopangwa,basi atakayejulikana anakata mkarafuu, mimi nasema iwe adhabu ya milioni tatu au kifungo cha miaka mitatu ni kidogo kiongezwe, ili kila mtu awe ni fundisho kwa jambo hili la zao la kitaifa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu naelekea katika kifungu cha 19 (1) ukurasa wa 374 kinasema "Mtu yeyote ambaye atakusudia kuhamisha karafuu kavu au mbichi au makonyo ya karafuu kutoka sehemu moja kwenda nyengine, atatakiwa kuomba kibali kwa Sheha kitakachokuwa katika fomu maalum. Na kifungu hiki nasema ni kizuri. Katika misimu ya karafuu iliyopita tulikuwa tunapata tabu sana kwa wananchi wetu hasa wanaochuma karafuu mbichi.

Mhe. Spika, katika uchumaji wa karafuu kuna namna mbili, kuna wale watu wanaojenga kambi katika eneo la mkarafuu, lakini vile vile, kuna watu wanaokwenda kuchuma na kurudi. Sasa hawa wanaokwenda kuchuma na kurudi wanapata tabu sana. Kwa hiyo, kifungu hiki kilichowekwa katika kutoa kibali, basi tunaomba kibali kitolewe kwa wale wanaokwenda kuchuma karafuu na kurudi.

Mimi katika eneo langu la Kojani hakuna mkarafuu hata mmoja, lakini nakumbuka zamani ilikuwa karafuu inaanikwa Kojani kisiwani. Unakuja

ng'ambu unachuma karafuu unavuka tena unakwenda kuanika karafuu Kojani. Hii ilikuwa inasababishwa tajiri aliyekuwepo Kojani kwenda kukodi mikarafuu, lakini vibarua kutoka kule kule lazima wawe wanakwenda kuvuna karafuu na kuja kuchambua kwa tajiri kule kisiwani Kojani kwa sababu hawawezi kujenga kambi. Kwa hivyo, huu usumbufu umekuwepo mkubwa wa kutosha tunaomba Mhe. Waziri, alizingatie sana. Tunaomba kibali kitoke kwa Masheha na kisiwe tatizo hali mradi uzingatiwe utaratibu wa kisheria uliotumika.

Mhe. Spika, hii nyengine ya mtu anayeomba kibali kwa karafuu kavu ni wakati wa kwenda kufanya mauzo hakuna jambo jengine. Kama naitoa karafuu yangu Pandani na kwenda *ZSTC* Wete kwenda kuuza ndie huyu anachukua kibali, lakini sidhani kama anachukua kibali kwa kwenda kufanya mambo mengine, anachukua kibali kwa kwenda kufanya mauzo. Kwa hivyo, hii izingatiwe sana. Hili linakuwa ni jambo zuri kwa kufuata utaratibu wa kisheria ambao leo hapa tunaichangia.

Lakini vile vile, niende katika kifungu cha 18 (3) kinasema "Kila mkulima mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu ambaye atakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji karafuu, atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo vinathibitishwa na mamlaka husika;

(a) Vifaa vya kuhifadhia karafuu,
(b) Vifaa vya kuanikia karafuu,
(c) Vifaa vya upimaji, na
(d) Mahitaji mengineyo yoyote ambayo mfuko utayaona yanafaa.

Nasema kifungu hiki na mimi nakipongeza vile vile kwa sababu inafikia wakati wakulima wa karafuu hawana vifaa hivi vilivyotajwa. Lakini vifaa hivi kama vitakuwa japo wenyewe watakwenda kununua, lakini wakipatiwa mapema ni matayarisho ya uchumaji wa karafuu na karafuu yetu itakuwa bora. Mtu leo anachuma karafuu vibarua tayari wameshachambua hana hata pishi ya kupimia ni matatizo.Ukifika msimu wa karafuu vifaa hivi vyote vimekamilika na wenye karafuu wamevipata mapema ili kujiandaa na msimu wa uchumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, mimi nilisema uchangiaji wangu umejikita katika maeneo manne haya, lakini nimeshayazungumza kwa kina naomba Mhe.Waziri, ayachukue na ayafanyie kazi. Nasema ahsante nakushukuru sana na naunga mkono mia juu ya mia mswada huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naanza kwa kumhimidi Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima wa afya na

leo hii tukiendelea na mkutano wetu huu wa chombo hiki muhimu cha wananchi wa Zanzibar.

Pili, Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa na mimi kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985 na kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nitakuwa sitendi haki kama sikumpongeza na kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Waziri makini na mahiri Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, na timu yake yote kwa kuleta mswada huu muhimu sana kwa maslahi ya Zanzibar na watu wake.

Mhe. Spika, natamani Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, ingelikuwa Mawaziri wake wote ni kama Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, ambaye ubunifu wake na kujituma kwake kunaonekana wazi wazi na ndio maana tunaona kila siku kunapatikana mafanikio katika sekta anazosimamia.

Mhe. Spika, mwenzangu kasema na mimi naona si vibaya kurejea kwamba katika kipindi hichi kifupi tangu alipoteuliwa kuwa Waziri ametuletea miswada mitano ya sheria. Na si miswada tu kwa ajili ya kuongeza sheria, lakini yote ikiwa imejikita katika kufanya marekebisho ya mfumo ambayo yataleta ufanisi zaidi katika sekta ambazo anazisimamia.

Mhe. Spika, alituletea Mswada wa Sheria ya Viwango, yaani sheria inayoanzisha *Zanzibar Bureau of Standard* mwaka 2011, Sheria ya Kuanzisha Rasmi Shirika la Biashara ya Taifa *(ZSTC)* ya mwaka 2011, Sheria ya Biashara ya mwaka 2013, Sheria ya Leseni mwaka 2013 na leo hii Sheria ya Maendeleo ya Karafuu.

Mhe. Spika, mswada kwa jumla ni mzuri na umejitahidi sana kuandaliwa vizuri na kujikita katika yale malengo ambayo yamekusudiwa kama yalivyo katika maelezo ya madhumuni na sababu.

Mhe. Spika, kabla sikuingia katika mswada wenyewe nilikuwa na tahaadhari ndogo, naomba kuielekeza katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusu hii miswada ambayo inachapishwa upya.

Mhe. Spika, taratibu za kuchapisha magazeti rasmi ya serikali zinaeleweka na hata nambari za kurasa za magazeti yale ya serikali zina utaratibu wake. Lakini nimegundua kwamba miswada inapochapishwa upya kila mswada unapokuja katika gazeti rasmi la serikali, nambari zinakuwa ni zile zile. Kwa mfano mswada tuliokuwa tumeumaliza kuujadili na kuupitisha asubuhi ya leo

unaanza na ukurasa wa 367 na huu tunaoujadili sasa wa Sheria ya Karafuu nao umeanza na 367.

Si hasha na ule ambao uliokuwa wa asili ambao ulikuwa na miswada yote una 367. Kwa hivyo, nadhani hili kidogo linapaswa lizingatiwe kwa sababu kuna taratibu ambazo zinaongoza masuala haya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sasa niseme mapema kabisa kwamba mimi nauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Na nauunga mkono kwa sababu mswada huu unarekebisha na kuleta mambo mapya mengi sana ambayo yatakuwa na faida kwa nchi yetu na wananchi wake, lakini hasa wale ambao wanahusika na zao la karafuu.

Mhe. Spika, ukitizama kifungu cha 5 kina mambo ya msingi sana ambayo yanakusudiwa kuletwa na mswada huu. Kwanza kuna huduma ambazo zitatolewa kwa wakulima wa karafuu. Lakini vile vile, kuna suala la fedha zitatokana na mfuko huu kutumika kuendeleza miundo mbinu katika maeneo ambayo yana mikarafuu.

Pia kuna suala zima lile la ubunifu wa *branding* ambao utatumika katika kuziwekea alama maalum karafuu za Zanzibar. Isitoshe itakapokuwa inaathirika, basi kifungu hichi pia kimejielekeza kwamba fedha za mfuko huu zitumike kufidia shirika la *ZSTC* ili liweze kuwalipa wakulima wa karafuu bei ile pengine ambayo imezoeleka. Lakini vile vile, imejikita katika utafiti.

Mhe. Spika, si hayo tu, kifungu cha 12 kinazungumzia Mpango wa Maendeleo wa Karafuu ambao ni dhana nzuri sana ya kibiashara. Na kujua kwamba Mhe. Waziri wa Wizara hii, hii ni sekta yake unaliona katika kifungu cha 12 kwamba panazungumziwa kuwa na tathmini za upembuzi na uchambuzi wa uchumi unaotokana na mabadiliko mbali mbali ambayo yatakuwa yanatokana na suala hili la karafuu. Kwa hivyo, haya Mhe. Spika, yanaonesha umakini ambao umetumika katika kuleta mswada huu.

Mhe. Spika, kabla sikuingia katika vifungu ambavyo nataka kuvichangia naomba niseme kwamba naungana na Mhe. Hija Hassan Hij, aliyesisitiza haja ya kutolewa elimu ya kina kuhusiana na mabadiliko ambayo mswada huu unayaleta kwa wakulima na wananchi kwa jumla, ili wasije wakaingia katika mkumbo wa kukumbwa na adhabu mbali mbali kutokana na makosa ambayo yanaanzishwa, pengine kutokana na mazoea tu hawana maarifa nayo. Nadhani hilo ni muhimu sana.

Sasa Mhe. Spika, baada ya hayo niende katika mswada. Mhe. Spika, mimi kwanza nilikuwa naomba nitoe maoni kuhusiana na kifungu cha 3 cha

mswada huu cha tafsiri hasa katika neno "ofisa wa umma". Na baadae nitakapokuja kukichangia kifungu cha 13 (4) nitaeleza kwa nini ninasema hivyo.

Mhe. Spika, mimi kwa maoni yangu namuomba Mhe. Waziri, akubaliane na mimi kwamba katika ofisa wa umma orodha ile iwaondoshe Sheha na Diwani. Sababu zangu nitakuja kuzieleza kwa kina nitakapofika kifungu cha 13 (4).

Mhe. Spika, ninasema hivyo, kwa sababu hata hii sheria ambayo inafutwa huko nyuma katika masuala ya kusimamia sheria iliwataja Polisi. Sasa sioni shida kuwajumuisha mkaguzi, ofisa misitu na ofisa yeyote anayeshughulika na karafuu. Lakini kidogo nina mashaka na kumuingiza hapa kama ofisa wa umma katika usimamizi wa sheria hii, Sheha na Diwani ambapo nitakuja kueleza hapo baadae Mhe. Spika. Hilo moja.

Mhe. Spika, la pili, nilikuwa naomba vile vile, nikichangie kifungu cha 10. Mhe. Spika, kifungu hiki kinasema:

> 10 (1) "Kutakuwa na daftari la usajili la wakulima wauzaji wa karafuu na wadau wengine wa karafuu ambayo mambo yote yanayohusiana na uendelezaji wa karafuu yaliyoelezwa chini ya sheria hii yataingizwa"

Sasa sina matatizo na kifungu, lakini hawa ambao wametajwa kidogo Mhe. Spika, kuna tofauti na orodha kama hii ambayo ipo katika kifungu cha 5 (1) (i). Mhe. Spika, kifungu cha 5 (1) (i) kinasema katika kazi za mfuko;

> 5 (1) (i) "Kuweka daftari la usajili wa wakulima wamiliki wakodishwaji na wadau wengine wanaojishughulisha na shughuli za uzalishaji wa karafuu kwa madhumuni ya kurahisisha shughuli za ulimaji wa karafuu huduma za kifedha bima na shughuli nyenginezo zinazohusiana na karafuu"

Sasa utaona kwamba huku kumetajwa wakulima wamiliki wakodishwaji na wadau wengine, lakini kifungu cha 10 kinataja wakulima na wauzaji wa karafuu na wadau wengine, kuna baadhi ya makundi hapa yameachwa. Mimi nilikuwa ninadhani ni muhimu kifungu cha 10 hiki, kwa sababu kinazungumzia daftari lile basi likajumuisha wote, kuwe na *constant*, kuwe na usawa baina ya wale ambao wametajwa katika kifungu cha 5 (1) (i) ambacho sasa kinakuwa kifungu cha 5 (i) baada ya marekebisho yaliyofanywa na Kamati na hiki ambacho kipo katika kifungu cha 10 (1).

Mhe. Spika, hivyo hivyo kwa hoja hiyo hiyo, kitazamwe na kifungu cha 10 (2) yale makundi ambayo yaliyotajwa pale yawe yote ambayo yametajwa katika kifungu cha 5 (i). Mhe. Spika, kifungu kile ambacho nilikuwa naomba nikitolee maoni ni kifungu cha 12 katika kusaidia kuufanya mswada kuwa bora zaidi.

Hapa Mhe. Spika, kuna mpango wa maendeleo wa karafuu. Mimi ninapongeza kwanza hii dhana nzima ya kibiashara kabisa, *concept* ya kibiashara kabisa Mhe. Spika, kwamba kuwe na mpango tusiwe tunakwenda tu, kuwe na *close development plan*. Na ninapongeza yale ambayo yametajwa kwenye kifungu cha 12 (2) kwamba yatakuwemo katika huo mpango. Lakini kuna suala moja ambalo naona Mhe. Waziri, limesahauliwa na kama nipo sahihi ningependekeza kwamba liingizwe, nalo Mhe. Spika, ni suala la kufikiria usarifu wa karafuu na bidhaa zinazotokana na karafuu.

Miaka mingi tafiti mbali mbali zilizofanywa, hata ukisoma majarida ya nje zinazozungumzia karafuu za Zanzibar, Zanzibar imetajwa sana katika karafuu, visiwa vyetu vimefika kuitwa *Spices Island,* si kwa sababu ya hiliki au mdalasini ni kwa sababu wa karafuu. Lakini wengi waliokuwa wakiandika wameandika kwamba Zanzibar imeshindwa karne na karne katika uvumbuzi wa kuja na njia za kusarifu karafuu ili kutafuta kuuza bidhaa nyengine zinazotokana na karafuu badala ya kuuza karafuu tu na mafuta ya karafuu.

Hao wanaonunua karafuu na mafuta ya karafuu Mhe. Spika, kuna bidhaa wanatengenezea. Sasa je, bidhaa hizi haziwezi kutengenezwa Zanzibar hapa hapa zikauzwa *product* bidha zenyewe badala ya kuendelea kuuza karafuu. Sasa ninafikiri katika ule mpango wa maendeleo suala la usarifu wa karafuu na bidhaa zinazotokana na karafuu, basi nazo zingeingizwa pale, kwa sababu sikuona popote kuanzia (a) mpaka (h).

Lakini jengine Mhe. Spika, ni kifungu 12 (3) (a). Hapa kifungu cha 12 (3) panazungumzwa mfuko wa kuandaa bajeti ya kila mwaka katika uendeshaji wa mpango wa maendeleo ya karafuu ambao utategemea, (a) imesemwa idadi ya wakulima walioomba na walio na sifa za kupewa vivutio kutoka kwenye mfuko.

Sasa hoja yangu Mhe. Spika, hapa na ninamuomba Mhe. Waziri, aizingatie ni kwamba kule kwengine kumetajwa makundi mbali mbali; kuna wakulima, wauzaji, wakodishwaji na pengine kuna wachomaji, lakini hapa pametajwa wakulima tu na tafsiri ya mkulima iliyoekwa katika kifungu cha ufafanuzi inamtaja mkulima kwa maana hususan ni *specific*.

Sasa nilikuwa naomba kwamba na wale wengine pia watajwe hapa ili wote wale waweze kufaidika ikiwa wale wenye mfuko ambao usimamizi wake ni bodi ikiwa itaridhika kwamba kuna tija itapatikana, basi wote waweze kuzingatiwa. Nilikuwa naomba hilo pia lionekane katika kifungu cha 12 (3) (a).

Mhe. Spika, sasa nije katika kile kifungu ambacho katika ufafanuzi nilikataa kwamba Sheha na Diwani waondolewe katika tafsiri ya ofisa wa umma kwenye kifungu cha 13 (4). Mhe. Spika, kifungu cha 13 (4) kinasema hivi na ninaomba nikinukuu;

> "Kwa madhumuni ya kusimamia masharti ya kifungu hiki, ofisa yeyote wa umma anaweza kuingia katika jengo au sehemu kwa ajili ya kuchukua au kukamata mkarafuu uliofikiriwa kuwa umetumika kinyume na masharti ya sheria hii"

Sasa Mhe. Spika, hapa kuna suala la kutekeleza sheria *law enforcement*. Kuna watu, kuna vyombo kama Polisi kwa mfano ambavyo vina majukumu haya, lakini kuna maofisa wengine ambao wana dhamana kama hizi, lakini Mhe. Spika, Sheha na Madiwani sisi sote tunajua mara nyengine wao wenyewe wametuhumiwa kushiriki hayo makosa yanayohusu usafirishaji wa karafuu na uharibifu wa mikarafuu.

Sasa leo tunawapa wao pia dhamana ya kuingia katika jengo au sehemu yoyote kwa ajili ya kuchukua au kukamata, hatukaribishi matatizo Mhe. Spika? Mimi kule kunakotolewa kibali Mhe. Spika, sina matatizo Sheha kubakia, lakini katika kumpa mamlaka Sheha na Diwani. Kwa mfano, Diwani Mhe. Spika, ni mwanasiasa anachaguliwa kama anavyochaguliwa Mwakilishi.

Sasa tunapompa dhamana hii ya kuingia katika jengo lolote au sehemu yoyote kwa ajili ya kuchukua na kukamata, mimi kidogo hii ninahisi inaweza ikaja ikatumika vibaya ikapelekea kuwanyanyasa hawa wakulima na wananchi kwa jumla. Mimi nilikuwa naomba kwa nia njema kabisa kwamba Sheha na Diwani angeondolewa. Mhe. Spika, rejea yangu ni sheria hii ambayo tunaifuta.

Sheria ambayo tunaifuta Mhe. Spika, kifungu chake cha 8 kwa sababu ipo kwa Kiingereza naomba nikisome kama kilivyo. Kifungu cha 8 (1) inasema;

> "*Any Police officer above the rank of Sub Inspector shall have power to enter upon and inspect any premises where he has reasons to suspect that the provision of this Act have been or are being*

contravened provided that such a police officer has a valid search warrant"

Sasa Mhe. Spika, hiki ni kifungu kimeandikika vizuri mno katika kuzingatia misingi ya sheria. Huyo Polisi si Polisi yeyote tu, katajwa mwenye *rank* inayozidi *Sub inspector*, tena katakiwa awe na *search warrant.*

Sasa ninajiuliza tunapotaka kufuta sheria tufute ni sawa, lakini kwa nini yale mazuri ya sheria ya zamani tusiyabakishe? Kifungu hiki kimekaa vizuri zaidi Mhe. Spika, kuliko hiki ambacho umekiona hapa. Kama nilivyosema kumetajwa kule katika tafsiri ofisa wa misitu na wengine, pengine hawa angalau wana madaraka ambayo tunaweza kusema ni sawa sawa na ya Polisi, lakini kidogo ninapata mashaka unapoingiza Masheha na Madiwani. Mhe. Spika, nilikuwa naomba hili tulitazame vizuri sana.

Jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 14 (1). Hapa Mhe. Spika, imesemwa uwezo wa Waziri kutangaza sehemu ya ardhi kuwa ni ya kilimo cha mikarafuu. Sina pingamizi na hicho kifungu kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana ya kusimamia suala la karafuu. Lakini nilipokuwa na matatizo, ukikisoma kifungu chenyewe kinasema kwenye 14 (1);

"Kwa masharti ya sheria hii na kwa sharti la mpango wa matumizi ya ardhi, Waziri baada ya kushauriana na taasisi ya ardhi anaweza kuitangaza kwenye gazeti la serikali ardhi yoyote ndani ya Zanzibar kuwa ni eneo la mashamba ya mikarafuu"

Tatizo langu Mhe. Spika, taasisi ya ardhi haikufafanuliwa ni nini. Katika ufafanuzi huku haikusemwa, sasa taasisi ya ardhi ni wizara ndio atakuwa Waziri anapaswa kushauriana naye au ni idara, ni chombo gani? Mhe. Spika, kwa sababu taasisi ya ardhi kuna taasisi zaidi ya moja katika viwango tofauti nilikuwa ninafikiri kuna haja ya kutajwa au kama kifungu kinabakia hivyo hivyo, huku kwenye ufafanuzi iongezwe taasisi ya ardhi, ni ipi inayokusudiwa hapa ambayo waziri atashirikiana nayo.

Kifungu cha 15 Mhe. Spika, hichi ninamuomba Mhe. Waziri, aharakishe tu uundwaji na ukamilishwaji wa mamlaka ya viwango Zanzibar (*ZBS*), kwa sababu inatajwa hapa. Tunavyojua mpaka leo kateuwa na kishateuwa viongozi wake na yeye ameshachagua wajumbe wake, lakini utendaji kazi mpaka leo ni wa mashaka kwa sababu mambo tele yanayohitajika yapatikane ili mamlaka hii iweze kufanya kazi hayapo. Kwa hivyo, nilikuwa ninamuomba hili alisimamie likamilike ili sheria iweze kufanya kazi inataja tena kwamba mamlaka hiyo lazima iwepo.

Mhe. Spika, kifungu chengine ni cha 16 ninaomba ufafanuzi vile vile, kinazungumzia sifa za mkaguzi. Hapa imesemwa mkaguzi aliyepewa mamlaka chini ya kifungu cha 8 (i) cha sheria hii atakuwa na sifa kama zilivyoelezwa katika sheria zilizopo. Hoja yangu ipo hapa sheria zilizopo ni zipi? za ukaguzi au zipi hakuna maelezo yanayojitosheleza katika kifungu hiki. Nilikuwa naomba Mhe. Spika, pia majibu.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho naomba univumilie kwa sababu kuna vifungu kidogo vingi ingawa ninasema kwa ufupi sana ili nipate kuvijumuisha vyote, kwa sababu sheria hii ni muhimu sana kwa maslahi ya Zanzibar na wananchi wa Zanzibar, ni kifungu cha 17.

Hapa Mhe. Spika, ninazungumzia kifungu cha 17 (c). Kifungu cha 17 kwa ujumla wake ni uwezo na majukumu ya wakaguzi. Sasa kifungu cha 17 (c) kinasema;

> "Kuchunguza au kukagua kibali chochote cha usajili, leseni, madaftari au hati nyengine na kwa madhumuni hayo, anaweza kufanya shughuli nyengine ikijumuisha kuchukua nyaraka ambayo inamilikiwa na mtu huyo"

Mhe. Spika, mimi tatizo langu ni hii ikijumuisha kuchukua nyaraka ambayo inamilikiwa na mtu huyo. Kwanza haikufafanuliwa ni waraka upi. Inawezekana waraka huu ndio ushahidi wa mtu kumiliki mali yake. Sasa anapokuwa mkaguzi anaweza kuchukua waraka huo, baadae huyo ambaye ananyang'anywa atakuwa na uthibitisho upi. Nilikuwa naomba nisaidiwe.

Mhe. Spika, hofu yangu kwamba kifungu hichi kisije kikaleta *arbitrariness* katika utekelezaji wake, yaani kikavuka mipaka na hivyo kumuathiri badala ya kumlinda yule ambaye anayekusudiwa kumlinda ni mwananchi wa Zanzibar.

Jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 18 (3) ambacho sasa baada ya marekebisho ya Kamati ikiwa kitapitishwa kitakuwa ni cha 18 (2). Hichi Mhe. Spika, kinazungumzia mambo ambayo kila mkulima mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu anapaswa kuwa nayo kabla ya kuanika au kuchuma, hapa imetajwa vifaa vya kuhifadhia karafuu, kuanikia, upimaji na mahitaji mengine yoyote ambayo mfuko itaona yanafaa.

Sasa hoja yangu ni kwamba kule mwanzo kwenye kifungu cha 5, mfuko umesema kuna haja ya kutoa motisha, lakini haikusema kwamba mfuko utalazimika kuwapatia wakulima mahitaji haya au hawa wengine ambao wanaoshughulika na kazi ya uchumaji na uanikaji. Sasa tunapoweka sharti

Mhe. Spika, kwamba mtu hatoweza kufanya hii mpaka ahakikishe kapata vifaa hivi na huku mbele inasema kwamba ikiwa huna vifaa hivi ni kosa la kisheria, kama serikali yenyewe haikuweka mazingira ya kumpatia mkulima kama huko zamani ilikuwa ikifanya kwa mfano kwa mikopo. Je, itakuwa ni halali kumtia mtu katika adhabu kwa kutokuwa na vifaa hivi.

Nilikuwa naomba hapa Mhe. Spika, akija Mhe. Waziri, tusaidiwe. Nilikuwa ninadhani tukiwa tumeweka kifungu cha kuwawezesha kuwapatia hivi kupitia mfuko huu, halafu wakawa hawana, hapo itakuwa ni sahihi kwamba liwe ni kosa.

Mhe. Spika, jengine linahusu uhamishaji wa karafuu kifungu cha 19. Wengi wamechangia hapa kifungu cha 19 (2) kinasema; kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hakitotumika kwa wachumaji wa karafuu ambao watakuwa katika majukumu yao ya kawaida kurejea majumbani mwao kutoka sehemu za uchumaji wa karafuu. Ninakiunga mkono sana Mhe. Spika, lakini hoja yangu na ninaomba Mhe. Waziri, akija anisaidie ni kwamba utawekwa utaratibu gani wa kumtambua huyu ambaye anarudi katika sehemu yake anayokaa ya kawaida na yule ambaye anahamishwa.

Pametajwa kwamba atachukua kibali kutoka kwa Sheha, lakini tunasema katika kijifungu cha (2) kwamba huyu halazimiki kuchukua hicho kibali. Sasa je, akija akikamatwa akisema anarudi katika sehemu yake, tuna uthibitisho gani. Nilikuwa naomba pia hilo niweke vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho kimenipa mashaka ni kifungu cha 19 (4). Hichi kinasema inakatwa kwa mtu yeyote isipokuwa shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala au sehemu nyengine yoyote. Mhe. Spika, mimi si mkulima wa karafuu, sijawahi hata kuzichuma, lakini tunawasikia wazee, tunasoma maandiko katika ripoti mbali mbali, tunafanya utafiti kwamba maumbile ya Pemba na hata pengine na wakulima wa karafuu kwa ujumla, lakini tunaambiwa hasa Pemba, ilikuwa ni kawaida kwa wazee kubakisha karafuu kavu kama ni akiba badala ya kuweka pesa yeye anaweka karafuu. (*Makofi*).

Siku anapozidiwa anakwenda kuuza karafuu yake, wanaposema wenyewe siku za masika. Sasa leo inapoondoshwa hii *tradition*, mazoea yaliyojengeka ya njia ya wananchi wenyewe kujiwekea akiba zao kwa njia zao Mhe. Spika, kidogo ninapata mashaka. Kwa sababu moja katika sheria za nchi lazima ziakisi utamaduni wa watu ambao eneo lile. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa naomba hili litizamwe tena. (*Makofi*).

Na kwa sababu kijifungu cha 5 kinazungumzia Waziri kuweka taratibu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kifungu hiki, labda inaweza ikaweka taratibu, lakini nilikuwa ninadhani hichi kifungu cha 19 (4) hasa kingeondoshwa Mhe. Spika, au kingeandikwa upya kwamba ikiwa anaweka kwa madhumuni ya kufanya uhalifu ni suala jengine, lakini kama anatunza kwa ajili kama akiba yake, mimi nilikuwa ninadhani ni utamaduni ambao umezoeleka ungeendelea ukabakia Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hee! muda unanikimbia, lakini naomba niende kifungu cha 20. Kifungu hichi kinahusu uteuzi wa benki. Kiujumla mimi nimefahamu malengo yake kwamba ni kutafuta ushindani wa kibiashara katika kutafuta benki ambayo itatoa kivutio kikubwa zaidi. Lakini Mhe. Spika, Zanzibar tunayo benki ya kibiashara ambayo inamilikiwa na wananchi wa Zanzibar, benki ya serikali ya *PBZ* na imafanya kazi kubwa sana kujiimarisha.

Na nilikuwa ninadhani tunahaja sisi kama benki ya nchi kuilinda na kuipa kila msaada ambao utapelekea kuongeza mapato yake. Sasa nilikuwa ninajiuliza kwa nini kwa madhumuni ya kifungu hiki, isiwe benki hii ikawa ni Benki ya *PBZ*, kwa nini tutoe fursa ya kutafuta benki nyengine ambazo zinazokuja hapa kuja kutengeneza faida tu, lakini si kuleta maslahi kwa wananchi. *PBZ* Mhe. Spika, ikifanya faida, faida yake inarudi kwa wananchi wa Zanzibar, watakaokopeshwa ni wananchi wa Zanzibar kutokana na faida zake. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili litazamwe hasa likizingatiwa katika kifungu cha 3 chenye tafsiri ya benki ambayo ilikuwa imetajwa.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba nilitolee maoni ni kifungu cha 22 (2). Mhe. Spika, kifungu cha 22 (2) kinazungumzia vyanzo vya fedha vya mfuko. Sasa kifungu cha 22 (2) inasema;

"Fedha za mfuko zitatumika kwa kazi na madhumuni ya mfuko tu kama itakavyoidhinishwa na uongozi wa shirika hautokuwa na uwezo wa kutumia fedha za mfuko kinyume na masharti ya kifungu hiki"

Sasa Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba kifungu cha 5 cha mswada tayari kimeeleza fedha za mfuko zitatumika kwa kazi zipi. Sasa kwa nini hapa tufanye ugumu na madhumuni ya mfuko tu kama itakavyoidhinishwa na bodi na uongozi wa shirika, wakati tayari kazi hizo zimeshatajwa ndani ya sheria yenyewe, kwa nini tena tuwape mwanya bodi kuja kuamua mambo mengine nje ambayo tayari yametajwa ndani ya kifungu cha 5 cha mswada huu.

Mhe. Spika, haraka haraka kifungu cha 24 (2), hapa panazungumziwa ukaguzi wa hesabu. Nimeona siku hizi wamekuja na *trend* hii ya sheria zote zinasema kwamba ukaguzi wa mahesabu ya mfuko utafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali au na mtu aliyeidhinishwa na yeye, sina tatizo na hilo, lakini ninaona kwamba sheria zote kwamba sasa zinakiuka kuweka sharti jengine la kwamba kuwe na ukaguzi wa nje kwanza wa mkaguzi wa kawaida kabla ya kuja Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Naona tumekuwa tukiliacha. Nilikuwa naomba nielezwe kwa nini hatuweki kifungu kinachohusu kwanza mkaguzi wa nje wa mfuko wa kufanya ukaguzi au wa shirika kufanya ukaguzi kabla ya kuja Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, sasa niende katika kifungu cha 26 kinachohusu makosa na adhabu. Hapa Mhe. Spika, bado ninamkumbusha Mhe. Mwanasheria Mkuu, tuliwahi kuzungumza ninafikiri tangu mwaka 2011 kwamba kuna haja ya kuwa sera juu ya adhabu, kwa sababu kama si hivyo, yaani *policy on penalties*, kwa sababu kama si hivyo, kila mswada ukija unakuja na vifungu vyake na adhabu zake ambazo nyengine haziowani.

Kwa mfano kuna nyengine hapa kwenye faini angalau imetajwa kima cha chini na cha juu, lakini kwenye kifungo kimetajwa cha chini tu, kisichopunguo miaka mitatu. Haielezi kikomo cha kifungo ambacho mtu anaweza kufungwa. Kwa hivyo, kimeachiwa wenyewe Majaji na Mahakimu waamue. Nilikuwa ninadhani Mhe. Spika, kuna haja ya serikali kuikumbusha tena kuja na hii *policy* ikifika miaka mitano, bado sheria tuliahidiwa kuwa itafanyiwa kazi ndani ya Baraza ikawa haijafanyiwa kazi. Ninajua kuwa Mhe. Mwanasheria Mkuu, ana mambo mengi, lakini ninafikiria na hili alitazame.

Mhe. Spika, kifungu cha 27. Hapa kidogo nimepata mashaka kuhusu makosa ya shirika. Kifungu cha 27 (1) kinasema; "Endapo kosa lolote chini ya sheria hii au Kanuni iliyotungwa chini ya sheria hii imefanywa shirika, mtu yeyote ambaye wakati utekelezaji wa kosa alikuwa kama mkurugenzi au afisa wa uongozi wa mambo ya shirika, itakuwa amefanya kosa na endapo akipatikana na hatia ataadhibiwa ipasavyo." Hii Mhe. Spika, tunamtwika dhamana binafsi kama likitokea kosa ndani ya shirika atakuwa kama amelitenda yeye binafsi.

Sasa kuna sheria nyengine tunazoletewa hapa zinakuwa na kifungu kinachosema kwamba ikiwa amefanya kosa ametenda au ameacha kutenda jambo kwa nia njema hatohesabika kuwa ametenda kosa. Hicho kimekosekana kwa Shirika la *ZSTC*, tunasema tu kwamba mtu yeyote atakayefanya kosa atahesabiwa kwamba yeye binafsi kafanya kosa lile na ataadhibiwa. Nilikuwa naomba maelezo kwa nini tumefanya hivyo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni kifungu cha 30 kinachohusu kanuni. Hili Mhe. Spika, ninataka nisisitize tu kwamba mswada ni mzuri na tukiupitisha na *Inshaallah* tutaupitisha utaweka sheria moja nzuri sana. Lakini mambo yake mengi yanahitaji yafafanuliwe kwenye Kanuni iweze kufanya kazi.

Pale mapema kuna mtu ametoa maoni Mjumbe mmoja, mimi ninafikiri kama alikuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alitaja mambo ambayo alisema yafafanuliwe, hayawezi Mhe. Spika, yale mambo yatajwe ndani ya sheria, yanapaswa yatajwe ndani ya Kanuni. Kwa hivyo, Kanuni ni muhimu sana zikamilishwe na nimuombe Mhe. Waziri, huyu makini mahiri wa kupigiwa mfano asimalizie tu tukampigia mifano kwa sheria, lakini vile vile, aoneshe uwezo wake kwa kutunga Kanuni kwa wakati ili sheria zake hizi ambazo amezileta ziweze kufanya kazi vizuri na ziweze kuleta tija na manufaa yaliyokusudiwa kwa wananchi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema tena ninauunga mkono mswada kwa asilimia mia moja, ninamtakia kila la kheri Mhe. Waziri, na ninamuombea apande zaidi na zaidi kwa sababu ni mmoja wa watu ambao akipewa dhamana Zanzibar itafika mbali sana.
Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kuwashukuru kwa mashirikiano makubwa ambayo munanipa katika kuendesha shughuli zetu. Muda uliobaki ninafikiri ni mdogo mno kiasi ya kwamba hatuwezi tukampa Mhe. Mjumbe, akachangia kwa utulivu. Kwa maana hiyo, basi tusitishe shughuli zetu na ninaahirishe kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni ambapo ninategemea wafuatao ndio watapata nafasi ya mapema kuja kuchangia.
Nao ni:

1. Mhe. Asha Bakari Makame
2. Mhe. Panya Ali Abdalla
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said
5. Mhe. Marina Joel Thomas

Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote tufike mapema kama kawaida, lakini msisitizo mkubwa ni hawa ambao nitawaita kwa ajili ya kufanya mchango wao.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe ninaahirisha kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 6.55 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa kuwa mtu wa mwanzo jioni hii kuchangia suala zima ambalo naweza kulihesabu kuwa ni uti wa mgongo wa serikali hii ukiacha kilimo.

Lakini Mhe Spika, kabla sijachangia nichukue nafasi hii adhimu nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake ambazo anazichukua kwa dhati kabisa na usimamizi mzuri kabisa katika zao hili la karafuu. Pongezi hizi kwa kweli niseme tu kwamba aendelee nazo kwa sababu ya kupandisha bei ya zao la karafuu toka utawala wake mara mbili. Kwa kweli watu wameingiwa na imani kubwa sana na niseme tu kwamba hata serikali kama inaingia hasara, basi kwa kweli inalipia fidia ile.

Mhe. Spika, baada ya kumpongeza Mhe. Rais, sasa nichukue nafasi hii niwapongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri, kwa kutuletea mswada huu ambao ndio kiini na uti wa mgongo wa zao la karafuu. Pia niwajumuishe na watendaji wao, ambao walikaa kwa makini na kuzingatia, wakaona kwamba sasa kuna haja ya kuuleta mswada huu ili sheria ikamilike kwa ajili ya zao letu la karafuu.

Sasa Mhe. Spika, kabla sijaenda kwenye dondoo moja moja, lakini kwanza mimi nataka Mhe. Waziri aje anifahamishe kwa kina katika haya nitakayoyazungumza. Katika ukurasa wa 372, kifungu cha 12(1);

Kifungu cha 12(1)

"Bodi itaandaa mpango wa muda mfupi, kati na wa muda mrefu na maendeleo ya karafuu ambao utaidhinishwa na Waziri kwa ajili ya kuongoza shughuli zote za maendeleo ya karafuu kwa kila mwaka".

Sasa sijui katika bodi hii kuna mtu wa kilimo humu. Mhe. Waziri aje anielimishe katika bodi hii, kama kuna mtu wa kilimo basi mimi sitokuwa na matatizo, lakini kama hakuna mtu wa kilimo, kwa kweli mimi kidogo nitagatigati hapa mpaka nielewe vizuri, hilo moja.

Lakini la pili, limeelezea mtiririko hapa. Mhe. Spika, hili zao la karafuu mimi niseme ni la *ZSTC* au ni la kilimo. Maana Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mujibu wa mtiririko huu Mhe. Spika, hapa kwamba upembuzi na uchunguzi

wa kiuchumi utakaojumuisha ubinafsishaji na athari zinazotokana na utekelezaji wa mpango na kuimarisha mikakati ya kuzuia athari hizo.

Kifungu cha 12(2)(b) "taratibu za uwekaji, usimamizi na uendeshaji wa vitalu na mashamba ya mikarafuu;

Kifungu cha 12(2)(c) “Mapendekezo ya uanzishwaji na uendeshaji wa mashamba ya mikarafuu”;

Kifungu cha 12(2)(d) “Mapendekezo ya mfumo wa vivutio na usaidizi kwa wakulima wa mikarafuu katika maeneo yanayohusu vifaa, usafishaji, upandaji, uoteshaji, uchumaji, uanikaji”;

Samahani Mhe. Spika, kwa sababu nataka nielimishwe.

Kifungu cha 12(2)(e) “mapendekezo ya tafiti za kuimarisha zao la karafuu katika maeneo yanayohusiana na mbegu, usimamizi wa vitalu, usimamizi wa uwekaji wa mbolea na usimamizi wa maji na teknolojia”;

Ni mtiririko mkubwa Mhe. Spika. Sasa mimi hapa nitamuomba Mhe.Waziri aje anielimishe vizuri. Najua kwamba *ZSTC* ndio inayoshughulikia mambo yote ya uuzwaji wa karafuu, lakini je haya pia ni ya *ZSTC*, najiuliza mimi mwenyewe. Sasa namuomba Mhe. Waziri akija aje anieleze vizuri hapa, maana naona kama kilimo kimemegwa kidogo na kimeletwa hapa. Kwa hivyo, naomba nije kupata ufafanuzi mzuri na wa kina.

Vile vile nikiendelea na uchangiaji wangu Mhe. Spika, ni kwamba karafuu Zanzibar kama tunavyoelewa kuwa visiwa vyetu hivi viwili ni nzuri kuliko zile ambazo zinazalishwa katika nchi ambazo zinazalisha karafuu. Hilo naona kuwa ni moja ambalo linatoa bei kubwa kwa ajili ya karafuu zetu za Zanzibar, lakini hata ukiangalia baina ya karafuu za Pemba na Unguja, basi wanasema watu kuwa karafuu za Pemba ni kali zaidi na ni nzuri kuliko karafuu za Unguja, kutokana na rutuba ambayo kule Pemba kwa zao hili la karafuu inaonekana kama ni mashamba maalumu ambayo yanazalishwa karafuu.

Mhe. Spika, mimi niiombe wizara ambayo imetutungia sheria hii kwa makini, lakini kwanza niiombe wizara kwamba tunatunga sheria nyingi sana Mhe. Spika, lakini usimamizi wake ni mdogo au usimamizi wake sisi tunaotunga sheria, basi saa nyengine tunafanya kuwa sheria ile isitumike kwa namna moja au nyengine, kwa maslahi ya wale ambao wanajitakia ruzuku kutoka kwa wale wakulima wa karafuu.

Mhe. Spika, sitaki nizungumze mengi kwa sababu hii karafuu ina miko yake, lakini miko hiyo ya karafuu saa nyengine inawapa shida hawa wakulima wa karafuu. Toka kuchumwa, kuanikwa, kuchambuliwa na mengineyo, kwa kweli ina mizengwe ndani yake. Sasa niiombe wizara, kwa sababu tunatunga sheria hii Mhe. Spika, basi sheria itumike kama ilivyoelezwa humu. Hilo moja.

Lakini la pili Mhe. Spika, usimamizi ndio muhimu. Suala la tatu Mhe. Spika, wenzangu waliotangulia wamesema elimu hasa kwa wakulima wetu wa mikarafuu, kutoa taaluma na kumuhakikishia mkulima yule unamfahamisha mpaka ahakikishe hatoingia katika dosari ndogo ndogo za makosa, halafu baadae tukawalaumu wakulima wetu wa karafuu. Naiomba sana wizara suala hilo litiliwe nguvu, kwa sababu mkulima wa karafuu ni tofauti na mkulima wa mwani, tofauti na mkulima mwengine yeyote. Mkulima wa karafuu kwa kweli ni mtu ambaye anahitaji taaluma kubwa sana, hasa kwa mujibu wa sheria hii tunayoizungumza sasa hivi.

Jengine Mhe. Spika, niwaombe wananchi wote kwa jumla ambao ni wakulima wa karafuu, kwamba tunapitisha sheria hii na nimeshaiomba wizara itoe taaluma, kwa kweli ukataji ovyo wa mikarafuu nawaomba wananchi jambo hili walitahadhari, kwa sababu sheria itachukua mkondo wake. Mimi naunga mkono Mhe. Spika, kwamba yeyote ambaye atakamatwa anakata mikarafuu kwa ajili ya ujenzi au kwa ajili ya shughuli nyengine. Nasema hata ile fidia ya Shs. 3,000,000 sijui na miaka 3 ni kidogo. Kwa sababu karafuu sasa hivi ukiangalia, mikarafuu mingi sana imekufa na mikarafuu mingi sana imeshazeeka, hata hicho kibali mimi nasema pia kinakaribisha rushwa, kama tutapewa vibali basi tunakaribisha rushwa Mhe. Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naiomba sana wizara kwamba sheria hii tuhakikishe kuwa tunaitendea haki yake ya kuisimamia na utekelezaji wake. Pia nije hapo hapo Mhe. Spika, zamani mchumaji karafuu, nilisema kwenye sheria, lakini sitaki nieleze kifungu cha (a), (b),(c) na (d). Mhe. Spika, naiomba wizara hii kwamba turudie yale mambo kama ya zamani, mchumaji wa karafuu mwenye mikarafuu hasa mkulima wa karafuu, basi akopeshwe majamvi, magunia ya kutia karafuu na akopeshwe vile vifaa vyote ambavyo vitamfanya yeye aingie mori na kuhakikisha kwamba karafuu hizi zina muelekeo mzuri, kwa sababu karafuu ni kwa jamvi, karafuu sio kwa kitu chengine chochote, wala sio kwa bati na wala sio kwa gunia. Karafuu ni kuanikwa kwa jamvi ndio unapata karafuu nzuri.

Mhe. Spika, cha kushangaza utakuta sasa hivi karafuu zinaanikwa barabarani, ukipita barabarani utakuta watu wameanika karafuu barabarani, nyengine zinapondwa na gari. Kwa hivyo, hizi haziwi karafuu nzuri. Ni namna gani

zamani walikuwa wanakopeshwa watu wetu vifaa vyote vile ambavyo vinamuhusu mkulima wa karafuu, wataweka sheria ndogo ndogo ambazo zinaweza kumshika yule ambaye amekopeshwa au kama imo hiyo sheria humu, basi watajua ni namna gani ya kumdhibiti yule mtu ambaye anakopeshwa vifaa vyote ambavyo vinahusika kuiweka karafuu katika hali yake ya kawaida na nzuri.

Mhe. Spika, nikiendelea na hapo hebu tujiulize hawa wenzetu huko nje hizi karafuu wanazichumaje, maana yake husikii mtu kaanguka kavunjika mikono, kichwa, kiuno. Je, wanazichumaje, hebu tutafiti. Siwezi kusema kama nina uhakika, lakini kuna baadhi ya nchi ambazo wanafanya mambo yao, kuna vitu ambavyo wanakua kama kuna ngazi hivi wanachuma karafuu, na mikarafuu haikatwi na wala haifanywi chochote inachumwa vizuri tu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri tubadilike katika uchumaji wetu wa karafuu, kusema kweli watu wetu wengi sana wanakuwa na vilema vya viuno, mtu hazai tena na anakuwa na kilema cha miguu, mtu hawezi kushughulika na shughuli zake nyengine. Namuomba Mhe. Waziri katika mambo haya tufanye utafiti, ili tubadilike hapa tulipo kuchuma karafuu kwa kujifunga kamba ya kiuno na huku unaning'inia, na nyimbo unazoimba wewe unaona zinakuchombeza kumbe zinataka kukuua.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika ugonjwa wa mikarafuu. Mhe. Spika, zamani wakati wa Mhe. Aboud Jumbe, mikarafuu ilipata maradhi mengi sana. Kulikuwa na maradhi yakiitwa sadande na daibo. Hebu sasa Mhe. Waziri akija atufahamishe, sasa hivi hakuna tena maradhi yale na mikarafuu inaendelea tu. Siku nyengine ukipita juu ya anga huko unaiona hasa mikarafuu kama kizee wa miaka 100 mvi tupu juu ukitizama chini, mikarafuu imepiga weupe. Kwa hivyo, aje Mhe. Waziri atufahamishe je, suala hili hajaliona kama kuna utaratibu wa kuhangaika na kutizama namna gani mikarafuu yetu tuweze kuienzi ili isitokezewe na hali hii na ile, kwa sababu ilikuwa inaambukiza maradhi yale. Kwa hivyo, na suala hili pia nataka aje atuambie Mhe. Waziri kuwa atalifanyia kazi vipi.

Lakini vile vile niwapongeze sana wizara katika fidia na Bima, lakini nitazungumza fidia kwanza halafu nitazungumza Bima. Mhe. Spika, hizi fidia basi *wallahi* mtu mpaka siku nyengine atatoka hospitali ameshatumia fedha zake nyingi sana kwa kujitibu yeye mwenyewe, lakini bado. Hapa ndio linapokuja lile suala la rushwa Mhe. Spika, hivyo namuomba sana Mhe. Waziri kwamba fidia ya mtu anayeanguka kwenye mkarafuu, basi ifanyiwe haraka.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani katoa mfano hapa. Kwa kweli ni mifano ambayo ipo hai. Mimi niishukuru kwanza Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutandika njia nzuri, njia mwanana kwa Jimbo la Mtambwe na hasa Mtambwe yenyewe, niipongeze sana serikali na nimpongeze sana Mhe. Rais, maana tulikuwa tunapiga kelele humu ili kuhakikisha kwamba njia ile inatengenezwa, lakini sio kutengenezwa tu kuburuzwa buruzwa, imekolea na imetengenezwa hasa, ahsante sana Mhe. Rais.

Natoa pongezi hizi kwa dhati kabisa, kwa sababu ni sehemu kubwa sana ambayo magendo ya karafuu yako kule. Kilichobakia nimuombe Mhe. Waziri, sasa zile njia za ndani ndani zile za kukimbiza karafuu, basi zile muzifanyie ukarabati ili mnapotaka kwenda huko muweze kufika bila ya matatizo.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema nimpongeze Mhe. Rais kwa njia ya Mtambwe, kwa sababu kuna siku nilikwenda Mtambwe Makoongeni, miaka mingi kidogo ya nyuma, basi mwanamke alianguka kwenye mkarafuu akiwa na mimba, lakini namna ya kumchukua na kumfikisha hospitali ilikuwa mashaka, basi mwanamke yule alikufa pamoja na mtoto ndani ya tumbo. Kwa hivyo, nasema napongeza kwa dhati hasa.

Mhe. Spika, na mimi nataka niseme hasa kwamba naipongeza serikali hii maana huo uchumaji wa karafuu kama hakuna maji, kama hakuna umeme ni bure, lakini sasa hivi watu *alhamdulillah*, jamaa wangu wa Mtambwe wako kwenye raha mustarehe, maji yapo, umeme *alhamdulillah,* na barabara ndio hiyo. Kwa hivyo, nachukua nafasi hii Mhe. Spika, kwa makusudi na mimi nasema, maana mimi huwa sifichi. Barabara ya Mtambwe ina maji na umeme, kabla hatujahamia hapa niliomba mimi katika lile jengo la zamani la Baraza la Wawakilishi. Umeme nilimuomba aliyekuwa waziri wa Nishati Mhe. Burhan Saadat Haji, akaniambia nitakutilia *Phase IV*.

Mhe. Spika, Umeme ule ni *Phase IV* niliouomba mimi Asha Bakari Makame kwa upande wa Mtambwe. Maji leo ndio nataka kusema. Maji nilianzisha mimi pale kwa baba yangu Bwagamoyo, kwamba hatuna maji, tukatafuta vianzio, lakini haikuwa, hawakupata wale niliowaanzishia, tukaenda Mtambwe Daya sijui Sichoko, maana usichoke huko hayo maji huko yaliko Sichoko, maana usichoke. Kuna mlima mrefu umesimama hata ukipandisha doo au hando basi uko taabani, na sijui kama unaweza kufika nayo juu kama hujaporomoka nayo.

Mhe. Spika, vile vile naishukuru Wizara ya Ujenzi kwa kupitia Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, walihakikisha kwamba maji yanapatikana. Yakaanza maji Hidaya kuliko kule Bwagamoyo niliokusanya watu kutaka kupatiwa maji, lakini baadae naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba

maji yale sasa hivi yanapatikana. Kuna maji, umeme na barabara ndio hiyo *alhamdulillah*. Mwenyezi Mungu atupe kila la kheri Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili tuwaletee wananchi wetu maendeleo wafaidike na Mapinduzi yao matukufu ya mwaka 1964.

Sasa Mhe. Spika, nikiendelea kuchangia niseme naishukuru wizara, maana kwanza kusema kweli Shirika la *ZSTC* lilikaa kama lilokufa mwanzo, lakini sasa mmelifufua, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa kufufuliwa shirika hili na nimpongeze sana Mhe. Waziri baada ya kuingia na Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wao pale waliona kuwa kuna haja ya kufanya marekebisho ya Shirika hili la *ZSTC*.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, palizungumzwa hapa kuhusu habari ile ya kutoa Madiwani na Masheha. Jamani tusikatae, kama utaingia kwenye nyumba ya mtu basi Sheha ndiye mwenye kujua nyumba. Mimi hao Madiwani saa nyengine hata sio lazima, lakini Sheha ndiye mwenye kujua mwenye shehia yake, tusikatae kitu ambacho kitatusaidia sisi wenyewe.

Mhe. Spika, ninavyoelewa ni kwamba hata huyo polisi akija na *warranty* hatoingia tu katika nyumba na hatomjua, ni mpaka afuate taratibu. Kwanza mpaka amfuate Sheha, aulize jina maana majina yetu Faki zinaweza kuwa Faki 20 katika mtaa mmoja. Fatuma yanaweza kuwa Fatuma 50 katika mtaa mmoja. Mhe. Spika, labda diwani, lakini kwa sheha naona tusimtoe kwa sababu Sheha ndiye mwenye shehia ambaye anajulikana kuwa yeye ndiye mwenye shehia.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 19 alikizungumza sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mimi naungana mkono na yeye. Jamani enzi za zamani Mhe. Spika, mimi nimeshawahi kuona babu yangu anachuma karafuu kama magunia 50 au 60, maana wao wenyewe walikuwa wanachuma karafuu halafu wanaziweka, za mwaka huu zinakutana na za mwakani. Walikuwa wanazipandisha juu ya dari wanaweka, likitokea tatizo la kutojiweza la njaa au la kitu chengine chochote, basi mwenyewe anapachua magunia mawili mawili juu ya dari kisha anapeleka kuuza anapata chochote cha kumsaidia yeye, watoto wake na wajukuu zake na familia yake.

Kwa hivyo, suala hili na mimi naunga mkono, kama litaleta matatizo Mhe. Spika, basi tumsajili na yeye huyu ili tujue tu Bakari Makame kachuma magunia mangapi na kauza magunia mangapi, atakayoyaweka ni mangapi, hapo hapatatokezea tatizo, ili kuweza mwenyewe kuja kufidia wakati atakaposhikwa na shida, lakini ukisema kwamba zichukuliwe karafuu na ndio maana ukaona wakati wa karafuu za enzi hizo za zamani Mhe. Spika, harusi iko hapo, watoto kutiwa jandoni iko hapo, kununuliwa masufuria hapo,

kununuliwa vitanda ni siku hizo za karafuu, kwenda Tanga au Mombasa kwenda kuchukua mahando ni wakati huo wa karafuu. Jamaa zetu ambao wanachuma karafuu basi kila kitu chao wanakifanya wakati wa karafuu, sasa tuwarudishie ile hadhi yao ya zamani. Pemba mpaka leo mahando yapo, wazee walikuwa wakienda Mombasa kuchukua mahando, kwa sababu ni toka jadi na enzi vitu hivyo vipo.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri suala hili waliangalie upya, isipokuwa waliwekee taratibu za kwamba mtu hatokuja kuweza kuuza karafuu kwa magendo au kuzisafirisha kwenda kwengine.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu sera. Kama alivyosema mwenzangu hapa ya adhabu. Mimi nadhani tuwe makini katika mambo haya, kwa sababu ni lazima tukubali, kuna sheria nyengine tunazitunga lakini tunakosea katika mambo yetu kutizama ile sera inatuambia nini. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, tusije kumtia mtu hatiani ambaye tutadhania tu, kama hakuna sera au kama imepitwa na wakati basi ni vizuri sera ile tukaiangalia upya, ili kuhakikisha kwamba tusije tukampa adhabu mtu ambaye anajitahidi katika kuleta uchumi kwenye suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu vituo vya karafuu. Kwanza niwapongeze wizara kupitia shirika lao la *ZSTC* baadhi ya vituo wamevitengeneza upya, lakini niombe kwamba watizame ni sehemu gani ambayo inahitaji vituo vile, ili kutowapa shida wale ambao wanaouza karafuu zao. Kama vituo vikiwa mbali Mhe. Spika, basi ndio hapa karafuu zinazoambiwa nakwenda kuuza kituoni, kumbe zinapitishwa njia nyengine zinapelekwa baharini.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri afanye utafiti wa Pemba nzima, ni sehemu gani na gani ambayo inahitaji vituo ili kuwarahisishia wakulima wetu wa karafuu kuuza karafuu zao kwa ufasaha.

Baada ya kusema hayo Mhe Spika, niseme kwamba atakapokuja kunifafanulia vifungu hivi vya kilimo, anayepanda mwenyewe kitalu na akaulea mkarafuu mpaka ukazaa. Pia nilisema kwamba je katika bodi hizi kuna mtu wa kilimo, maana huyu ndiye anayemtengenezea huyu *ZSTC* kupata ule uchumi. Sasa ikiwa yule anayetengeneza kuleta ule uchumi wewe hukumtia popote, itakuwa hujamtendea haki.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, basi nichukue nafasi hii niwapongeze sana Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwa kutuletea mswada huu ingawa umechelewa, lakini tutafanya nini. Naomba nisisitize tu kwamba mswada huu unatakiwa usimamiwe na utekelezwe na tufuatilie, tusije tukakaa kwenye viti tukapitisha mswada huu, tukasahau kwamba kuna malengo ambayo

mmeyapanga nyie wenyewe katika Mswada huu, ili kutekeleza hii karafuu iweze kunufaisha taifa letu.

Baada ya kusema hayo nikishapata sina matatizo na mswada, lakini nataka nipate maelezo tu. Nikishapata maelezo mswada sina matatizo nao, maana nikiupinga utakuwa hauwezi kufanya kazi huu mswada na yale matakwa ya wananchi yatakuwa bado hayajapatikana.

Baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kwa imani kabisa, kwa sababu ni tegemeo la wananchi. Niwaambie tu wananchi tutumie mswada huu tutakapopata elimu, tuelimishwe na tuulize kama hatukuufahamu vizuri ili tuufahamu tusije tukaingia makosani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia hazina ya uzima na afya njema pamoja na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu hadi hapa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, nadhani nitumie fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe. Pamoja na kwamba asubuhi uliniruhusu kuuliza swali langu la msingi na lile la nyongeza, na sasa nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada iliyopo mbele yetu. Kwa hivyo kwa niaba yangu na wapiga kura wangu wa jimbo langu la Wawi tunakushukuru sana kwa wema wako huo.

Mhe. Spika kwa kweli mchangiaji aliyepita mama yangu, mkwe wangu, mama Asha Bakari Makame, yeye ana uzoefu sio tu katika masuala ya kuchangia katika Baraza hili, lakini hata katika masuala ya uchumaji, masuala ya uanikaji na hata katika masuala ya uuzaji karafuu. Kwa sababu yeye anatokea Mtambwe ambapo ni sehemu ambayo karafuu zinapatikana kwa wingi. Kwa vile yeye anasema ameshachangia na mimi natokea Vitongoji kwa hali ambako hakuna mkarafuu hata mmoja Mhe. Spika. Mimi nadhani atakuwa kanifilisi sana huyu mama, lakini pamoja na hayo nitalazimika kutiatia nyalio tu baadhi ya maeneo.

Sasa kwa mnasaba huo Mheshimiwa kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu mno, naomba kidogo nianze na historia fupi ya huu mswada.

Kwanza Mhe. Spika, niishukuru serikali kwa kuleta huu mswada. Nasema hili kwa dhati kabisa niishukuru na serikali kupitia Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwa kuweza kutuletea huu mswada. Kwa kweli mti wa mkarafuu ambao unaendelea kupotea siku hadi siku. Mti huu umeingia hapa tangu karne

ya 17 na mfanyabiashara wa Kiomani bwana Saleh Buharumeili Hii ni kwa sababu hakukuwa na sheria makini na madhubuti zinazosimamia mti huu.

Mhe. Spika, tuna kila sababu ya kuutunza sio katika minajili ya kwamba ni mti wa biashara, lakini hii wataalamu wanaita kwamba huu ni urithi wa nchi na hadhi ya taifa letu. Leo kuendelea kuuacha mkarafuu ukapotea na kukatwa na kujengewa nyumba na watu kuendelea kukata kuni na kupikia, hii ni hasara kubwa. Sasa kwa dhati kabisa napenda niipongeze serikali kwa kuuleta huu mswada ambao mimi sina tatizo nao, baada ya kuuboresha na kuvitilia nyalio baadhi ya vifungu.

Mhe. Spika, juzi nilipata nafasi ya kwenda China, nilifanyiwa mipango na Mwenyekiti wangu wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma. Nikaenda China pale Guangzhou nikaenda Shangshan, nikatembea kidogo. Kwa bahati mimi siwezi kuzikosa karafuu, popote ninapokwenda japo mbili tatu niwe nazo kwa ajili ya kumung'unya wakati wa usiku, hasa nikiwa katika maeneo ya baridi kama vile China. Kwa bahati kule nilipata kuonana na wajumbe wenzangu wa mataifa mbali mbali. Kila mmoja akaja na mambo katika taifa lake. Mimi ikafika pahali nikawaambia katika taifa langu nina zao moja zuri sana la biashara ambalo kwa kweli katika nchi zilizopo kule Kusini mwa jangwa la Sahara tunatamba sana kwa zao hili. Nikaanza kuwagaia punje tatu tatu za zile karafuu. Walikuwa wanataka kunichukua nikaishi kwao kwa jinsi zile punje tatu tu za karafuu walivyozipenda.

Mhe. Spika, wenzetu karafuu wanazipenda na wanaihitaji sana, sisi hizi karafuu tunazidhalilisha, mikarafuu hatuitunzi, inatiwa moto, inachanjwa kuni, inakatwa miti kwa kujengewa, huku serikali inaangalia tu. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa lakini kwa sasa inaonekana mnaanza kujali baada ya kutuletea huu mswada.

Mhe. Spika, niende kwanza katika kifungu cha 7(1) cha mswada cha kuanzishwa kikosi kazi naomba nikinukuu.

> Kifungu cha 1(1) "Kitaanzishwa kikosi kazi chini ya Waziri chenye jukumu la kuzuia magendo ya karafuu na vitendo vyengine vinavyoathiri biashara ya karafuu."

Mhe. Spika, hapa nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo, kwa sababu hivi vikosi kazi vitakuwa vingapi, nikitaka nijue. Wakati nakuja huku Unguja natokea Vitongoji mpaka nilipofika Mkoani Bandarini nilipita mageti karibu manne hivi, na kila nnapopita nasimamishwa naangaliwa katika gari na kuna polisi, KVZ na KMKM. Sasa hivi vikosi kazi baada ya hivi kumbe pia vinataka kuanzishwa na vikosi kazi vyengine. Waziri utakapokuja katika hili uje

unifanyie ufafanuzi. Kwa sababu sisi ni lazima tuwe makini Waheshimiwa katika kupitisha hizi sheria.

Mhe. Spika, sisi katika nchi hii ndio *watchdog* wa kuangalia matumizi mazuri ya *public fund*. Sasa kama itaendelea kuundwa kwa vikosi kazi tu sisi itakuwa kila kukicha tunaunda vikosi kazi tu na tukasema viundwe na tukaidhinisha fedha. Hayo sio matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi wa nchi hii. Kwa vyovyote vile, kwanza Mhe. Waziri aje atoe maelezo, hichi kikosi kazi ni *excluding* ya lile jopo la mapolisi, KMKM na wengine waliokuwemo barabarani na kwenye maji, nitakuja kuhitaji ufafanuzi huo.

Mhe. Spika, niende katika Sehemu ya Tatu, uchumi wa karafuu katika ukurasa wa 371. Uimarishwaji wa kilimo cha karafuu. Kwanza niishukuru serikali, kwanza nataka nizungumzie mambo ya kitaalamu juu ya kuimarisha hili suala la karafuu. Nadhani wanasiasa wenzangu hawatoweza kunifahamu vizuri, lakini nadhani hili jopo la wataalamu waliopo hapo juu nafikiri wanaweza wakanifahamu.

Mhe. Spika, hivi sasa sisi tuna mabadiliko ya tabia nchi. Kwa ninavyofahamu mimi karafuu inahitaji udongo wa *loamy soil*, mara nyingi hii inakuwa *slightly alkaline or acidic*. Mkarafuu kwa siku za nyuma ulikuwa ukihitaji udongo uliokuwa hamirojo sio ule wa *acidic* lakini kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kumekuwa na ongezeko la hewa mkaa katika nchi. Ambapo hewa mkaa hii huoshwa na maji ya mvua na hatimaye kutiririka katika udongo na kufanya ule udongo wa *loamy* kuwa *acidic* badala ya kuwa hamirojo uwe na sumu sasa. Jambo ambalo mti wa mkarafuu haupendi udogo wa aina ile.

Mimi nilikuwa nawashauri tu hawa wataalamu kwa sababu sheria tumeshaipitisha jana na naamini iko kwenye meza ya Mhe. Rais ile Sheria ya Hakimiliki kwa ajili ya wagunduzi, ile tuliyoipitisha juzi kwa mimea. Naomba sana katika hili wataalamu wanisikilize na ingawa Waziri siku moja alinambia kwamba tukileta *variety* nyengine ya karafuu, mkarafuu tutaupoteza. Hii *existing species* ya mkarafuu, imekutana na mabadiliko ya tabia nchi sasa, uzalishaji sio mzuri, mmea wake si mzuri tena.

Mhe. Spika, naomba ili mazao yapatikane ya kutosha, wataalamu wetu kwa sababu sheria tumeshaipitisha jana ya wagunduzi wa mambo ya mimea na Rais wetu naamini ile sheria ataitia zaini karibuni basi mshirikiane nao hawa, kusudi watutafutie *variety* ambayo itaoana na mabadiliko haya ya tabia nchi. Mvua zimekuwa ndogo sana sasa, mikarafuu imeanza kusinyaa badala ya kutoa matawi unakutia kuna majiti tu na majani kidogo. Hii ni kwa sababu haipati maji ya kutosha, haya aliyokuja nayo Saleh Buharumeilu katika karne ya 17 inahitaji maji mengi, lakini kutokana na mabadiliko ya tabia nchi mvua

zimekuwa ndogo. Sasa tunaomba mu -*work hard* wataalamu kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo ili mtupatie *species* hii tusiiondoshe lakini mtupatie *variety* nyengine ambayo itakuwa *well equipped according to environment*.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika suala zima la hichi kikosi kazi. Kikosi kazi kisiangalie magendo ya karafuu tu. Hivi sasa kuna watu ambao sijui kama wafuaji nyuki wale, mimi sidhani kama *forest fire,* kwa sababu miti yetu haijisugui sugui kama ile ya ki- Bara, lakini kuna watu maalumu wanashughulika na mambo hayo, halafu mikarafuu inaungua sana. Hivi karibuni katika njia ya kuelekea Kiwani mkono wa kulia, lile shamba lililokuwepo karibu liliteketea sana kwa moto. Sasa Kikosi kazi nacho kiwe na kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba mambo ya moto katika miti yetu au mikarafuu yetu inapungua.

Aidha, wauzaji kuni za mikarafuu, miti inakatwa kwa wingi, zinawekwa barabarani na tunanunua. Vijijini huna vya kuwaambia kwamba wapikie muembe au wapikie mshelisheli, wanasema hauwaki, lazima wapate mkarafuu. Sasa mimi nadhani wizara katika hili wajitahidi sana kwa kushirikiana na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kile kitengo cha mazingira waweze kuwa *turn* watu *mindset* zao kwa kupitia elimu, kwamba jamani na mshelisheli nao ni kuni, mkamasi nao ni kuni na muembe nao pia ni kuni, lakini mkarafuu msiutegemee sana. Ikiwa watu hawana uwezo wa kutumia nishati nyengine basi mtumie na hii miti mengine, pamoja na kwamba ni kuharibu mazingira lakini sasa tutafanyaje, tusile?

Mhe. Spika, nije katika suala zima la mfuko wa karafuu. Katika suala hili tumeambiwa kutakuwa na daftari, litakuwa na taratibu na kuingiza wadau wote wa karafuu. Mimi naanza kupata tatizo hapa. Daftari hili uanzishwaji wake utakuwaje na kutakuwa kunaingia na kutoka katika hili daftari. Maana mkulima wa karafuu anaweza akawa ana shamba lake la mkarafuu lakini akatokewa na mashaka akaliuza na akafilisika akaamua kuondoka nchini, akawa hana shamba hata moja la mkarafuu au huyu mtu akafariki na akajileta mtu mwengine kwa kutumia jina lile la maiti. Hautokuja kutokea utapeli wa huu mfuko wetu? Sasa sijui mtatumia utaratibu gani nyinyi katika kuona mnalihakiki vipi hili daftari la hawa wakulima wa mkarafuu.

Mhe. Spika, nikija katika ibara ya 18(2) naomba nikinukuu:

Kifungu 18(2) "Kila mkulima, mmiliki, au mkodishwaji wa mikarafuu ambaye anakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji wa karafuu atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo vilivyothibitishwa na mamlaka husika"

Baadhi ya vifaa hivyo alivitaja kama magunia, majamvi, pishi na vifaa vyenginevyo.

Mhe. Spika, hapa mimi kipengele hichi napata wasiwasi, tusije tukawakumbia watu sheria kandamizi. Wewe Mheshimiwa una karafuu zako chungu nzima zinaharibika, ushakwenda zako Tanga kwa mashua umeshapata majamvi, halafu wewe utoke Konde, pia na karafuu zako zikonde na wakati umeshapitia huko kwa mashua, halafu uje Chake Chake uje uthibitishiwe. Huu si unyanyasaji wa wakulima kwamba majamvi umeyatoa Shimoni Mombasa unateremka Msuka kwa mashua, halafu uje Chake Chake uje uthibitishiwe majamvi yale. Mimi nadhani kipengele hichi kitolewe. Tunataka kuwafanya watumwa wakulima wetu wa karafuu.

Mimi nadhani mtu akishapata majamvi yake kama kayapata Tanga au Shimoni, yasijekuthibitishwa lolote, aende kwenye kambi yake akayaanikie. Tusiwafanye watumwa hawa wakulima wetu, kabisa kabisa. Mambo kama haya tuyaepushe na hawa na wao wana kazi, aende akatafute karabai, haya na hiyo karabai nayo pia ithibitishe, keshanunua karabai Mombasa 20 azilete ZSTC zije zithibitishwe, si utumwa huo? Hapana bwana, kipengele hichi hakifai katika mswada huu, mimi nadhani kiondosheni hiki.

Mhe. Spika, sasa twende katika ibara ya 18(4) naomba Mhe. Spika, nikinukuu vile vile.

> Kifungu 18(4)"Kila Mkulima, mmiliki au mkodishwaji wa mkarafuu atahakikisha kwamba karafuu zake zipo katika hali nzuri na hazijaharibika au kuchanganyika na vitu vyengine wakati wa uchumaji, uanikaji au uuzaji."

Mhe. Spika, sasa unataka kututia wasiwasi huu wa mpeta kwamba tukiwa na karafuu za mpeta, maana mpeta ni karafuu zilizoharibika. Nilimwambia Mhe. Waziri wa Biashara siku zile kwamba leteni *another alternative* ya kufanya *drying* ya hizi karafuu kuzikausha, akasema ni lazima zikaushwe na jua. Haya sasa msimu wa masika mvua utakwenda kuzianikia wapi weye? Ukitizama huku una marunda ya karafuu, huku mvua inanyesha, karafuu huna pa kuziweka, utaziweka wapi karafuu hizo, hata zisiharibike zikawa mpeta.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nafikiri ananifahamu zivuri. Katika uchumaji wa karafuu kunakuwa na mvua, matope, yatazuia majani, mataka taka, yatakuwa yanaburutwa, yakiingia kwenye chungu za mikarafuu. Ndio utakapokwenda kuuza kuna madongo, kuna madude mbali mbali, kwenye mkeka, Yailahi Yarabbi Toba vijumba tunavyoishi sisi ni vidogo vidogo na ukienda huko kambini ni vibanda vitupu kama labda tutazizoa tuzitie kwenye nyumba zetu, hatuna uwezo huo. Matokeo yake tunaziacha

pale pale vishungu vishungu na zinapigwa na mvua. Leo mnakuja kutwambia kwamba tuhakikishe tutakapokuja kuziuza zisichanganyike na jambo jengine. Labda muizuie mvua isinyeshe katika huo uchumaji wa karafuu au sisi wakulima mtujengee majumba kama hili holi, ili zikinyesha mvua tukimbilie kuja kutia mbio karafuu zetu, lakini kinyume na hilo hichi nacho tuondosheni mtakuja kutufunga au tutakuwa hatuziuzi karafuu.

Mhe. Spika, jengine twende katika ibara ya 19(4) naomba nikinukuu kwa idhini yako.

Kifungu cha 19(4) "Inakatazwa kwa mtu yeyote isipokuwa Shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala au sehemu nyengine yoyote"

Mhe. Spika, sikiliza nikwambie, hii serikali isitufanyie mambo haya. Hizi karafuu ni zetu sisi wakulima, si zao wao, kabisa kabisa. Leo kutulazimisha kwamba siye karafuu tukishakuzichuma tukimbilie ZSTC kuziuza. Aaa! hizi karafuu si zenu bwana. Nyie mmekuwa wakiritimba tu kuhodhi hili zao. Lakini tulikuwa tuna uwezo siye wa kwamba tuuze sehemu nyengine yoyote tunayoitaka ilimradi bei inaridhisha. Leo tumeshakubali ya kwamba nyie mu-*monopolise* hili zao, leo mnatutaka tukishakuzichuma tuziuze, huo ni utumwa mnaotwambia ya kwamba mnatukaanga kwa mafuta yetu wenyewe, msitukaange kwa mafuta yetu wenyewe.

Mhe. Spika, kuna usemi unasema wa kiarabu "*milatul biladi, sheria"* kwa maana ya kwamba mila za jamii ni sheria. Sisi tangu zamani na hadi sasa na hata baadaye, Wazanzibari, tuna khulka na tabia ya kuhifadhi mambo yetu haya kwa mfano ng'ombe wetu, karafuu zetu, mpaka pale tutakapofikwa na mashaka ndio tunakwenda kuuza. Leo ukitwambia kwamba tukaziuze papo kwa papo, watoto wetu wanataka kusoma, tunasubiri *semester* ifike tukauze karafuu. Tukiziuza kabla ya *semester* haijamalizika tutazitumia pesa kwa kuzinunulia mpunga. Kwa hivyo ndio inatupasa tuweke karafuu kwa sababu karafuu hailiki, lakini pesa tukizipata tutazitumia. Hizi karafuu ni zetu siye msitunyanyase jamani serikali!

Mhe. Spika, mimi napendekeza tuweke muda kwamba mtu asikae na karafuu ndani kavu zaidi ya mwaka, lakini kwa kusema tuziuze hapo kwa hapo, mtatufunga wengi kwa hili hatukubali! Karafuu ni zetu, hamtusaidii kulima, hamtusaidii kupalilia, kwa hili mtupe muda.

Mhe. Spika, mimi mtoto wangu alipotaka kwenda kuoa nilikwenda kwa Gopal Samji, nikamuonesha karafuu changa, unachuma karafuu ile changa unamwambia mzee nataka unipatie shilingi elfu 10, mtoto wangu anataka kuoa. Anakukopesha, unamwambia ikishakupea tu karafuu nitakulipa pesa

zako. Gopal Samji anakupatia pesa zile, unakwenda kuozesha mtoto wako kama unakwenda kusomesha watoto wako, wanasoma. Leo serikali kazi yenu kututungia masheria kwamba tukishakuzivuna tuziuze, ama kwa hili hatuziuzi!

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba suala hili tuwekeeni muda, kinyume cha hivyo mtakuwa mnatunyanyasa, hamtukopeshi. Au mtwambie tukitaka kusomesha watoto wetu tuje tukope mfuko huu. Mimi hivi sasa hivi nina watoto watatu wapo chuo, mwengine ana watoto wanne. Halafu unanambia nikishakuchuma karafuu nije niziuze pesa nizitumie. Siziuzi, nitaziweka ndani mpaka ikiingia *semester* nyengine nikaziuze nije niwasomeshee wanangu.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena niiombe sana serikali kwamba mkarafuu huu umefika zamani, una haja ya kutunzwa. Pia ni vyema tutafuteni na *variety* nyengine ambayo itakayoendana na mabadiliko ya tabia nchi. Ingawa tusiachane na huu mkarafuu wa karne ya 17 lakini tuendeleze na huku tukiwa na *variety* nyengine ambayo inaweza kupambana na haya mabadiliko ya tabia nchi, kusudi mazao ya karafuu yapatikane kwa wingi ili tuweze kupata tija kwa taifa letu.

Mhe. Spika, nimalizie na hili suala la usafiri wa karafuu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Mimi nakaa Vitongoji nina mikarafuu yangu Chonga, nikitoka Chonga niilete Vitongoji. Nyie mliokusudia ni hilo, lakini kuna tatizo la wale wakulima wakubwa wa karafuu wanaoishi maeneo ya Mgelema, Ng'ombeni, Mkoani kwa akina Mhe. Abdalla Moh'd kwao mvua hazipiti. Sasa huamua kuchukua karafuu kwa malori zikapelekwa Vitongoji, kulikokuwa hakuna mvua sana, au sehemu ya Kangagani kwao Mhe. Hamad Masoud, sehemu za Muwambe kwao Mhe. Hija Hassan kuja kuanika. Sasa mtakapowaona kina Mhe. Abdalla Moh'd Ali na waheshimiwa wengine huwa wanaleta karafuu zao na huwa hawazileti kwa magendo, wanaamua kuleta huku kwetu kuja kuanika, zikishakauka wanazirudisha tena kwenda kuziuza au kuzihifadhi majumbani mwao kwa ajili ya kuwasomesha watoto wao.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, ikiwa nitapata ufafanuzi wa kutosha katika hoja zangu nilizozitoa, nitaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mia kwa mia. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache. Kwanza nikupe pole kwa kufiliwa na mtoto wako na mimi nawashukuru wote wale walioungana na mimi katika msiba wa mtoto wangu wa kwanza ambaye ilitokea tarehe 13 na Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema Peponi. Vile vile nimuombe Mwenyezi Mungu

amjaalie afya njema Mhe. Haroun Ali Suleiman aweze kurudi tena hapa Barazani.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Waziri kwa kuleta mswada wake huu. Kama unavyosema Mswada huu ni Kufuta Sheria Nam. 11 mwaka 1985 na kuweka Sheria mpya ya Maendeleo ya Karafuu na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba sheria hii ni nzuri na vile vile niungane na Kamati kwa yote na mchango wao wa kamati ile tunaupokea vizuri sana. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Amani na mimi haitakuwa vyema kama sikuchangia mswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja kwenye vifungu, kwanza madhumuni ya sheria hii ni mazuri sana na ina malengo au ina misingi mikuu mitano ambayo yameelezwa hapa. Pamoja na mchango mkubwa unaotolewa na karafuu katika uchumi wa Zanzibar ambapo kwa msimu wa mwaka 2011/2012 karafuu zimechangia kiasi cha shilingi sabiini milioni. Hali hii inaridhisha. Umuhimu wa kuwa na sheria madhubuti ya kukuza zao la karafuu ili iweze kunufaisha taifa kwa kiwango kikubwa zaidi ni la msingi.

Mhe. Spika, nasema sasa umefika wakati wa kutunga sheria madhubuti kwa zao la karafuu, mwenzangu amesema hapa alityepita, karafuu ni zao wenyewe wakulima na kwa hivyo tuwaachie wenyewe wauze kule wanakotaka. Lakini hili niseme kwamba ni zao la taifa, kwa hivyo taifa lenyewe liwe na mikakati yake ya kulilinda zao hili la karafuu.

Mhe. Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 370 kuna uongozi wa mfuko ambao Mkurugenzi Muendeshaji wa Shirika ndie atakayefanya kazi ya mfuko huo. Napenda Mhe. Waziri aniambie Mkurugenzi huyu atafanya kazi hizo za mfuko namna gani?

Kuanzishwa kwa kikosi kazi, kwa kweli Mhe. Spika, sisi kama wananchi wa nchi hii tunahitaji mambo mengi kupitia serikali. Kwa hivyo kikosi kazi hiki mimi kwa kweli naungana na wenzangu wale waliochangia sehemu hii ya kikosi kazi. Tumeona kwamba ni pesa nyingi ambazo zinatumika kwenye *task force*, ambapo vikosi vyote vya SMZ pamoja na vyombo vya habari kwa wakati ule wa msimu wa karafuu vinakuwa vinafanya kazi kwa kulilinda zao lile.

Kama sisi tunaitegemea serikali itulipe mishahara na kila kitu, kwa hivyo kila mtu atakuwa na kazi ambayo anawajibika nayo, ni kwa nini sasa tusifanye zile kazi zetu kwa mujibu wa utaratibu. Lakini unazikuta pesa nyingi sana zinatumika, hata lile shirika lenyewe linashindwa kupata faida kinyume chake

ile faida yote inakwenda kwenye *task force.* Kwa hivyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri ni lazima na sisi katika hii *task force* kama walivyosema wenzangu tuna nafasi ya kulipangia mikakati ili zao hili liweze kutumika vizuri na tukaipatia faida serikali yetu.

Mhe. Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 371 kuna kifungu cha 9 kinasema Bodi itaanzisha Idara itakayoshughulikia majukumu yote ya mfuko. Lakini kuna huu mfuko umekwenda kwenye sehemu nyingi, kwa nini tusiweke kwenye kifungu kimoja kama hapa kifungu cha 8, bila ya kuathiri uwezo wa Bodi uliopewa chini ya kifungu cha 15 ambapo kwenye uwezo wa majukumu ya Bodi kifungu cha 15 cha sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar namba 11 ya 2011 itakuwa na uwezo kwa mfuko.

Mhe. Spika, kuna maeneo mengi yametajwa mfuko mfuko! Kwa nini tusiweke pamoja mambo yote yanayohusiana na mfuko zikiwemo kazi zake. Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba tufanye hivyo.

Vile vile kwenye kifungu cha 13 ukurasa wa 373 vitendo vinavyokatazwa katika kilimo cha mikarafuu ni kuchoma au kutengeneza makaa, kuchimba mawe, udongo au mchanga hili Mhe. Spika, ni jambo zuri kwa sababu ukianza kwenda kuchimba kwenye maeneo yale kwa kweli hali ya uharibifu wa mazingira inaweza ikatokezea.

Mhe. Spika, kuna mikarafuu mingi kwa kweli imeshakuwa mikongwe, kwa hivyo kuwe na mkakati wa kuitoa ile mikongwe na kuotesha mipya. Na kazi hii jana tulipitisha sheria moja hapa ya mswada wa kuanzisha sheria ya hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu.

Mhe. Spika, ukurasa huo huo wa 373 kifungu namba 14 kwa masharti ya sheria hii na kwa sharti na mpango wa matumizi ya ardhi Waziri baada ya kushauriana na Taasisi ya ardhi, anaweza kuitangaza kwenye gazeti la serikali ardhi yote ndani ya Zanzibar ni eneo la mashamba ya mikarafuu. Kwa kweli Mhe. Spika, hapa naona kama kutakuwa na mgongano, waziri gani sasa hapa tumpe mamlaka ya kutangaza.

Kwa sababu kuna Waziri wa Ardhi anayeshughulika na ardhi na vile vile kuna Waziri anayeshughulika na kilimo, utaona kwamba unampa fursa au unampa kazi ya mtu mwengine, kazi ya ardhi basi awe ni Waziri wa Ardhi tu, wakae pamoja labda kuona ni kituo kimoja ambacho ni nani atakuwa na mamlaka ya kutangaza kwamba ardhi hii itakuwa ni kwa kazi gani. Kwa sababu sheria za ardhi nazo vile vile zinamtaka Waziri wa Ardhi ndio awe na fursa zaidi ya kugawa ardhi na vile vile kuna ardhi ambazo zimetengwa kwa mashamba, majenzi na kwa uwekezaji. Tukisema kwamba ya huyu tunampa

huyu nafasi ya huyu au haki ya huyu tunampa huyu, sasa tukienda hata kwenye mambo ya uwekezaji ni Waziri wa ardhi ndio anayehusika na kutoa ardhi ile kwa wawekezaji.

Mheshimiwa kuna kifungu namba 18 kinasema kutakuwa na msimu wa zao la mwaka na msimu wa zao la vuli kama ni msimu wa uchumaji wa karafuu wa kila mwaka. Na kutakuwa na vifaa, ni kweli kama alivyosema Mhe. Asha Bakari kwamba sasa hivi unakuta ule uanikaji wa karafuu kwa kweli si nzuri. Karafuu zinaanikwa barabarani, juu ya mapaa ya nyumba n.k. Na hii inasababisha kutokupata karafuu zenye *grade* nzuri ingawaje zao hii la karafuu sasa hivi limekuwa ninavyosikia bei ni moja tu. Karafuu utakayoipeleka wewe haina *grade* kama zamani. Kwa hivyo ni lazima kuwe na uanikaji uliokuwa nzuri. Zamani mimi ninakumbuka niko mdogo ilikuwa wakati wa uchumaji wa karafuu kunakuwa na kambi.

Na vile vile vifaa vya upimaji, nimesikia hivi karibuni kwamba karafuu hizi kuna watu wanafanya ujanja pale wakati wa upimaji. Yeye anapimia pishi kubwa kutoka kwa wachumaji (vibarua) lakini yeye anapokwenda kuuza anapimiwa kwa pishi ndogo. Kwa hivyo hii ni dhulma na tujue kwamba Mwenyezi Mungu hatokuachia kufanya dhulma ya namna hii.

Kifungu 20 (1) kwa madhumuni ya kifungu cha 8 cha sheria hii Bodi itazingatia taratibu za ushindani na itachagua benki kwa ajili ya utoaji wa huduma ya benki, huduma ya usimamizi wa fedha za mfuko zilizotengwa kwa ajili ya kuwakopesha wakulima. Bodi kuchagua benki gani kwa sababu watu wanasema *charity begins at home,* sisi tuna benki yetu kwa nini tusichague benki yetu moja kwa moja hapa, Benki ya Watu wa Zanzibar ambayo vile vile inatoa mchango wake wa fedha nyingi kulipa wauzaji wa karafuu. Ningeomba kwamba hiyo Bodi basi itoe fursa kwa benki hii.

Mhe. Spika, vile vile niende ukurasa 377 ambao kifungu cha 30 (1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa utekelezaji nzuri wa masharti na madhumuni ya sheria hii. Ni vizuri kwa waziri kutunga kanuni kwa sababu sheria bila ya kanuni hakuna ufanisi mzuri.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, kwa sababu wenzangu wameshachangia mengi niseme na mimi naunga mkono sheria hii na ninashukuru kwa kunipa fursa hiyo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia mswada wa kuanzisha sheria ya kufuta sheria ya karafuu namba 11 ya mwaka 1985. Mhe. Spika, pia naipongeza serikali kwa kuanzisha mswada huu. Mimi nitachangia katika kifungu namba 8 (b) kifungu ambacho

kinasema, ‘kusimamia mipango ya urejeshaji wa mikopo na ulipaji wa madeni ya mfuko’.

Mhe. Spika, hapa mimi nataka nitoe indhari tu kwa Wizara iwe makini katika kusimamia suala hili la ulipaji wa mikopo na madeni. Nasema hivyo kwa sababu serikali ilianzisha mifuko mbali mbali ikiwemo JK na AK kwa nia ya kuwasaidia wananchi wake kuweza kujishughulisha na shughuli mbali mbali za maendeleo. Lakini kiuzoefu inaonesha kwamba mifuko mingi ulipaji wake ulikuwa wa kusua sua na kwa baadhi ya wananchi wengine kutolipa kabisa mikopo hiyo.

Lakini hapa ninachoomba kwa Wizara itoe elimu ya kutosha kabisa kabla haijanza kutoa mikopo hiyo, ili waelewe kwamba mikopo si sadaka, wala si msaada. Mikopo unakopa, unafanyia shughuli zako na unarejesha ili fedha hizo ziweze kuwasaidia wengine katika kuendeleza shughuli zao mbali mbali za kujiletea kipato.

Nitakwenda katika kifungu namba 18(3), kifungu hiki kinasema kila mkulima, mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu ambae atakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji karafuu atatakiwa atimize masharti yafuatayo kwa mamlaka husika.

(a) Vifaa vya kuhifadhia karafuu, vifaa vya kuanikia, vifaa vya upimaji na mahitaji mengine yote ambayo mfuko itayaona yanafaa.

Mhe. Spika, hapa nilikuwa ninaiomba Wizara ifuatilie kwa kina suala hili ili ionekane kwamba vifaa hivi vinapatikana, kwa sababu wakitumia vifaa hivi vitasaidia karafuu zetu kuwa katika hali nzuri na hatimae kwa ubora na hata na bei inakuwa nzuri.

Ninakwenda katika kifungu namba 10(1) kinasema kutakuwa na daftari la usajili wa wakulima, hapa tu nilikuwa naomba maelezo kwa Mhe. Waziri, naomba nimuulize kwamba daftari hilo litakuwa wapi na litasimamiwa na nani. Nilikuwa naomba hapa Mhe. Waziri anipe maelezo.

Mhe. Spika, kifungu namba 13 (4) kinasema, ‘kwa madhumuni ya kusimamia masharti ya kifungu hiki Ofisa yoyote wa umma anaweza kuingia katika jengo au sehemu kwa ajili ya kuchukua au kukamata mkarafuu unaofikiriwa kuwa umetumika kinyume na masharti ya sheria hii. Katika tafsiri ya mswada huu Mhe. Spika, imeeleza ofisa wa umma inajumuisha Sheha, Diwani, Polisi na kadhalika.

Hapa kuna baadhi ya waheshimiwa wenzangu wamechangia kwamba labda sheha asiwepo lakini mimi naomba nitoe maelezo haya. Mhe. Spika, sheha ni kiongozi wa serikali na ameteuliwa na serikali. Sheha ana majukumu mengi tu katika shehia yake. Sheha anatekeleza sheria, sera miongozo mbali mbali ambayo wanapewa na serikali. Sheha pia anatunza kumbukumbu mbali mbali za vizazi, vifo, kuhama, kuhamia, talaka na kadhalika. Kwa hivyo sheha katika chombo hiki naona Wizara haikubahatisha wala haikumpendelea ni moja ya majukumu yake.

Mimi nitatoa mfano tu, kuna baadhi ya wananchi pengine kiutaratibu inavyotakiwa unakaa katika shehia fulani, mfano mimi ninakaa katika shehia ya Tomondo lakini nataka kuhamia katika shehia ya labda Kiembesamaki. Kiutaratibu unatoka na barua ya Sheha ambae huku unakotoka anakupa barua na unapeleka kule unakokwenda, yeye anakupokea na anajua katika shehia yangu kaingia mwananchi mpya.

Lakini kuna baadhi wa wananchi hawafuati taratibu hizo, matokeo yake linatokea jambo la maana anakwenda kwa Sheha kutaka msaada, sheha anamwambia mimi sikutambui na hamtambui kweli, kwa sababu kaingia kinyemela. Matokeo yake anasema kwamba sheha huyu hafai, sheha anabagua, lakini kiufupi bwana na sisi tuna matatizo. Tufuate zile taratibu ambazo zinawekwa na sheria hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashkuru kunipa fursa kwa wakati huu sijui laasiri au sijui ni magharibi kuzungumza chochote kuhusu mswada huu. Kiujumla nafikiri na mimi nimelelewa au nimezaliwa ndani ya mikarafuu na nimelelewa kwa fedha za karafuu na nimesoma kwa fedha za karafuu. Sasa isingelikuwa busara kuuwacha mswada huu ukapita tu bila ya mimi kusema chochote. Na Mhe. Saleh pale alisema yeye alitaka kuweka nyalio, lakini bahati nzuri kaweka na nyama na boriti kabisa. Sasa fursa kaichukua yeye lakini kwa vile na sisi tunatoka katika sehemu hizo hatutokosa cha kusema, hasa kwa vile kanitaja kwamba sisi ndio wahusika wakuu wa zao la karafuu. Na ukiangalia kiukweli takwimu zinasema Wilaya ya Mkoani ndio inayozalisha karafuu nyingi kwa Visiwa vyetu hivi viwili.

Mhe. Spika, kiujumla ukiangalia kwa maneno utaiona sheria hii ni nzuri sana lakini ukiingia ndani kwa *practice* utakutia imekuja kidogo kuleta kero kwa wakulima wa zao la karafuu. Kwa nini ninasema hivyo, kwa sababu Mhe. Spika, haya mengi tunayoyaona hapa yatakuwa kidogo kama yanakuja kubadilisha tabia zetu za uchumaji wa karafuu. Sasa nina wasiwasi tukiya-*practice* huenda yakaleta kero kwa sababu kwetu sisi yatakuwa ni mapya

kabisa. Sasa sijui kukubalika kwake kwa jamii kutakuwa kwa mara moja, haraka haraka au kutakuchukua muda mrefu.

Mhe. Spika, nilikuwa kwanza mimi nipendekeze katika utangulizi wa mswada huu kuna kipengele kinasema Ofisa wa Umma, sasa kipengele hiki kinasema kinajumuisha Ofisa wa Umma, Mkaguzi, Polisi, Ofisa wa Misitu, Sheha, Diwani na Ofisa yeyote anayehusika na karafuu. Mhe. Spika, nilikuwa nataka nipendekeze kipengele hiki kiondoke kwa sababu *best practice* hasa katika Kisiwa cha Pemba inaonesha kwamba masheha wetu wamekuwa ni lalamiko kubwa kwa wanaohudumia karafuu, hasa ule wakati wa utoaji wa vyeti na mengineyo.

Lakini nilipokwenda mbele nilikutia kipengele cha 9 kinasema mtu yoyote ambaye anakusudia kuhamisha karafuu kavu au mbichi au makonyo kutoka sehemu moja kwenda nyengine atatakiwa kuomba kibali maalum kwa sheha. Sasa sheria hii Mhe. Spika, imemtaja Ofisa wa Umma akiwemo Mkaguzi, akiwemo Polisi, Ofisa Misitu na Diwani. Lakini huku kutoa kibali kwa ajili ya kuhamisha karafuu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine hawa wote wameachwa, amepewa mamlaka mtu mmoja.

Sasa mimi ninajiuliza, kwa nini hawa wengine waliotajwa kwamba na wao ni Maofisa wa Umma na wao wasipewe mamlaka ya kutoa kibali, ili kama lengo ni kurahisisha uchumaji, uanikaji wa hizi karafuu na uuzaji wake basi kukamilika kwake kutahitaji hawa maofisa wote. Lakini leo sheha anapewa mamlaka peke yake ya kufanya hivi, hiki kipengele Mhe. Spika, kitaleta kero. Kwa hivyo mimi ningemshauri Waziri ili kufanikisha sheria hii basi na hawa Maafisa wa Umma waliotajwa katika sheria hii na wao wakapewa ruhusa. Sheha peke yake anaweza akakwamisha maendeleo ya sheria hii.

Mhe. Spika, niendelee kidogo kuchangia tena kipengele kinachosema kwamba kuwahudumia wanunuzi wa mwisho katika hali ya kuanguka kwa bei duniani. Sijui hapa Mhe. Spika, mswada huu unamkusudia nani. Kwa imani yangu hapa linakusudiwa lile Shirika la ZSTC ambalo ndio mtu wa mwisho anayenunua karafuu kutoka kwa wakulima. Sasa ninajiuliza ina maana tunaweka fungu kwa ajili ya kui-*compensate* iwapo Shirika litakula hasara katika ununuzi wa karafuu, kama ni hivyo biashara hii itakuwa inafanyika vipi.

Mimi ninafikiria haya yangelikuwa ni mambo mawili, kama Shirika tumelipa kazi ya kununua karafuu basi linunue karafuu kupata hasara na kupata faida itokane na mfuko wake yeye mwenyewe. Mfuko huu kusudio lake ni kuwasaidia wachumaji, wakulima na watakaoanguka mikarafuu, si hivyo mfuko huu nina wasiwasi utatumika vibaya.

Kulisaidia Shirika kwa ajili ya kulipa fidia litakapopata hasara hiyo ni kazi yake yeye, Shirika tusililee, tulipe kazi yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, lakini katika kile kipengele cha mwanzo nilichosema kwamba mtu hatakiwi au aombe kibali kutoka kwa Sheha na wale niliopendekeza na wao waingizwe katika kutoa vibali, pale patakuja mgogoro mkubwa. Ninafikiri sheria ingetuainishia eneo ukubwa wake hasa ni eneo gani ambalo mtu atatakiwa aombe kibali kwa kuchukua cheti. Kwa kuiacha hivi hivi tutakuja kamatana humo na baadae tutapelekana Polisi na baadae tufungane au tutoleane faini. Kwa hivyo bora ingekuwa wazi, ikasema eneo fulani, lenye ukubwa fulani, utatakiwa uchukue kibali si hivyo, matatizo yatatokea katika jamii yetu ambalo si jambo tunalolipendelea.

Lakini Mhe. Spika, kipengele cha 13 kinasema tunakatazwa, kuchimba mawe, udongo na mengineyo. Kimazoea yetu wakati wa uchumaji wa karafuu au wakati wa upandaji wa karafuu kunajitokeza kipindi ambacho huwa tunafanya usafi, aidha huwa tunakata miti midogo midogo au tunaondoa hayo mawe ambayo yatakuwa yapo chini ya mikarafuu.

Ninavyofahamu mimi sehemu ambayo inaota mikarafuu basi mawe huwa hayapo. Sasa ili kulisafisha shamba langu mimi nitahitaji yale mawe niyaondoe ili kupata wigo zaidi wa kupanda ile mikarafuu. Sasa hapa ukija ukiniambia kwamba siruhusiki kuchimba mawe, hicho kitakuwa ni kinyume na ile taratibu niliyosema, ndio nikasema baadae inaweza ikaja ikawa ni kero kwa wale wanaojua upandaji wa mikarafuu. Haya mawe nafikiri tungeyaondoa, tungeruhusu watu wachimbe mawe kwa usalama wao.

Kwa sababu wakati wa uchumaji inawezekana chini kuna mawe, ukianguka ikawa ni hatari zaidi na hilo ndilo tunalofuatilia. Kwa hivyo, tunataka tuyaondoe ili kuwa na usalama wa yule ambaye pengine atadondoka katika mkarafuu, au kunipa fursa mimi ya kupanda mkarafuu mwengine katika eneo lile.

Mhe. Spika, lakini pia sheria hii kama walivyosema wengine inakataza pia kuhifadhi karafuu. Wamesema kwamba ni sheria ambayo labda inapingana na taratibu zetu za huko nyuma. Ni kweli, lakini je, huo muda umewekwa? Kwamba wewe hutakiwi uhifadhi karafuu katika muda fulani ni muda gani? Labda pia sheria ingetueleza kwamba muda ambao wewe hutakiwi kuweka karafuu zako ni muda fulani. Kwa sababu sisi tuna mazowea ya kwamba wakati wa uchumaji karafuu wengine hatupendelei kwenda kila wiki au kila siku kuuza karafuu. Tunapendelea zaidi mpaka tunakunja majamvi yetu ndio siku ile tunakuja na gari tunapeleka kituoni moja kwa moja. Ukienda pale

unauza kwa *lump sum* kama ni kulipa unakwenda kulipa, hatuna mazowea ya kwamba kila siku twende na kigunia kimoja.

Mhe. Spika, kwa maelezo hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi jioni hii kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu ya mwaka 2013. Mhe. Spika, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake kutuletea mswada huu.

Mhe. Spika, kwani huu mswada hautokuwa wa mtu mmoja tu au kwa wakulima wa karafuu tu, bali kwa wananchi kwa ujumla na taifa zima. Mhe. Spika, niseme kwamba huu mswada ni habari njema ambayo Mhe. Waziri katuletea hapa, kwa sababu hata Waswahili husema kwamba, "Inapoingia neema huwa haiingii kwa mtu mmoja, huingia kwa watu wote".

Lakini pia niseme kwamba Mhe. Waziri baada ya kutuletea huu mswada kikubwa zaidi kwanza ni kuhamasisha upandaji wa mikarafuu. Kwa sababu hivi sasa mikarafuu hiyo inayotungiwa mswada inakufa kwa wingi sana.

Pia niseme kwamba, hii sheria isiwe kuwa ya kuwadhalilisha watu. Kwa mfano, kipindi kile cha mikarafuu hii inapozaa kwa kule kwetu huwa watoto wanakwenda kuokota mpeta na wakifika kule wale matajiri ambao wanachumiwa zile karafuu na watoto wanaokota, basi wao huanza kuwadhalilisha watoto na wakasema kwamba, unataka kuokota karafuu zangu hapa ukiondoka hapa tuelewane. Hili namuomba Mhe. Waziri alipigie kelele sana kuhusu watoto wetu ili waweze kuwa wanahifadhiwa na udhalilishaji huo.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 18(2) kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma hapa na mimi kidogo nataka nifafanuliwe. Aidha, kifungu hiki kitawavunja moyo wakulima na wavunaji wa karafuu. Lakini naomba kwanza nikinukuu.

Kifungu 18(2) kinasema kwamba: "Kila mkulima, mmiliki, au mkodishwaji wa karafuu ambaye anakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji wa karafuu atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo vilivyothibitishwa na mamlaka husika".

Mhe. Spika, niseme kwamba kama ni vifaa vilivyothibitishwa, hili litawavunja moyo sana wakulima wetu, la ikiwa vifaa hivi itakuwa wanakopeshwa hapa Mhe. Waziri nitamuunga mkono sana. Kwa sababu

wanapochuma karafuu ikiwa vifaa vile wanavyo, naamini watu watakuwa na furaha.

Mhe. Spika, kwanza ufahamu karafuu ni kuwa na vifaa na vifaa vyenyewe kwa mfano kama majamvi. Sasa unapowadia msimu wa karafuu ikiwa watu hawana majamvi ya kuanikia ni tatizo kubwa, la ikiwa hivi vitathibitishwa au vitakopeshwa itakuwa si tatizo. Kwa sababu tatizo kubwa la karafuu kuharibika ni kukosa vifaa. Kwa mfano, ikiwa vitathibitishwa hivi itakuwa watu wanaanika karafuu pale pale chini hatakwenda mtu kununua jamvi wala kifaa chengine.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 20 ukurasa wa 375 kinachosema, kwa madhumuni ya kifungu cha 8 cha sheria hii, Bodi itazingatia taratibu za ushindani na itachagua benki kwa ajili ya utoaji wa huduma ya usimamizi wa fedha za Mfuko zilizotengwa kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wa karafuu.

Mhe. Spika, hili nampongeza sana Mhe. Waziri, ni jambo kubwa sana na ni zuri. Kwa sababu hata mtu awe tajiri ikiwa anayo mikarafuu hana fedha itakuwa ni tatizo kubwa. Lakini ikiwa kutakuwa na fedha za kukopeshwa naamini hata mkulima ataweza kupata kulipwa pale anapochuma.

Nikiendelea nije katika kifungu cha 370(j) kinachosema kwamba, kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, hili nalo pia ni suala kubwa sana kwa sababu watu wetu wanapoanguka mikarafuu wanapofika hospitali wanakaa kama wiki moja bado mtu hajatibiwa. Kwa hilo nimuombe Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Afya anapokuwa mtu kaanguka mkarafuu tu akipelekwa hospitali apewe kipaumbele cha kutibiwa. Kwa sababu huyu mtu anakuwa ni muokozi wa taifa hili na ni muokozi wa zao letu hili la karafuu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hilo alizingatie.

Lakini pia nije katika ukurasa wa 371 kifungu cha 11, Mfuko utasaidia mamlaka inayohusika kwa kuidhinisha aina tofauti ya karafuu zinazopandwa Zanzibar. Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kuna aina ngapi za karafuu Zanzibar ambazo zinazooteshwa?

Kwa hayo Mhe. Spika, naomba uniruhusu nikae kitako ahsante.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii

kuwepo katika Baraza kwa ajili ya kuwatumikia wananchi kama vile ambavyo wametutuma.

Lakini la pili nachukua nafasi hii ya kukushukuru wewe binafsi kunipa nafasi hii ya kuchangia angalau mawili matatu katika mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 na kuweka Sheria mpya ya Maendeleo ya Karafuu na mambo yanayohusiana na hayo.

La tatu, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake uliokuwa mfupi lakini ulikuwa na ufasaha, pamoja na kumpongeza kutuletea mswada huu kama ni ukombozi wa wakulima wa zao la karafuu visiwani petu Zanzibar.

Mhe. Spika, mchango wangu nianze kwenye Sehemu ya Pili kifungu cha 5(1)(j). Hiki kimechangiwa na wawakilishi wengi, lakini pia na mimi nitakuwa mchache wa fadhila kama sikukichangia kipengele hiki. Kipengele hiki kinasema, kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, kipengele hiki ni muhimu sana, tulikuwa tunazungumza mara nyingi zamani kidogo, wachumaji wa karafuu wanapopata madhara katika machumo ya karafuu walikuwa wanapewa fidia, lakini kwa muda mrefu kidogo uliopita suala hili kwa kweli lilisahauliwa au lilidharauliwa kabisa. Jambo ambalo linahuzunisha sana kutokana na madhara wanayoyapata wakulima wa karafuu.

Kwanza nitoe pole kwa mchumaji wa karafuu wa Jimbo langu la Chambani katika kijiji cha Zawadini aliyeanguka mkarafuu juzi na siku ya pili akafariki. Nawapa pole wafiwa wote na namuomba Mwenyezi Mungu awape subira na amlaze mahala pema peponi muhanga huyu wa mkarafuuu.

Mhe. Spika, suala hili ni muhimu na ni muhimu sana kama ambavyo karafuu ni muhimu kwa Zanzibar. Hivi sasa tuna walemavu wengi ambao wamepata ulemavu kwa kuanguka mikarafuu. Kwa hivyo, nalishajihisha sana suala hili lakini kama walivyochangia wenzangu kwamba suala hili anapotokea muhanga wa mkarafuu basi lisicheleweshwe kufanyiwa utaratibu wa kutibiwa. Huyu ambaye ameanguka mkarafuu urasimu wa aina yoyote tunamuomba Mhe. Waziri asiufanye, ili mhusika atibiwe mapema. Watuwake waepukane na kuuza ng'ombe au chochote kwa ajili ya kumtibu mtu huyu ambaye amepata madhara ya kuanguka mkarafuu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika kifungu cha 7, kuanzishwa kwa kikosi kazi. Mhe. Spika, kwa kweli kipengele hiki kinasema kitaanzishwa kikosi kazi chini ya waziri chenye jukumu la kuzuwia magendo ya karafuu na vitendo vyengine vinavyoathiri biashara ya karafuu.

Mhe. Spika, hofu yangu ni kwamba kikosi kazi hiki kinaweza kikatumia fedha nyingi zaidi kuliko hata huo uzuiaji wa magendo. Sasa hapa niseme kwamba waziri awe makini sana kwa sababu kuna wakati mwingi tunapata taarifa kuwa pahali fulani imekamatwa mashua, ina gunia 80 za karafuu lakini aliyekamatwa na gunia hizo hapatikani. Kwa hivyo, hapa namuomba Mhe. Waziri awe makini sana katika kikundi hiki cha *Task Force*. Kwa hivyo hili linatakiwa angalizo la kutosha.

Mhe. Spika, niende katika kifungu nambari 11(a) alizungumza hapa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, lakini kwa sababu ni *point* muhimu nimeiweka na mimi nitahitaji ufafanuzi. Kifungu hiki kinasema kuidhinisha aina tofauti za karafuu zitakazopandwa Zanzibar. Mimi nipo katika eneo ambalo jimbo langu limezungukwa na mikarafuu katika sehemu za barabarani, lakini najua aina moja tu ya mkarafuu. Sasa hizi aina tofauti za mikarafuu namuomba Mhe. Waziri atufafanulie kwa sababu inawezekana kwamba kuna aina nyengine za mikarafuu ambazo mimi sizijui.

Mhe. Spika, nikienda katika kifungu hicho hicho 11(d) kinachosema kwamba, kuchunguza sababu, tukio, kinga, kudhibiti na kuondosha maradhi yoyote ambayo yanaelekea kuhatarisha maslahi ya zao la karafuu.

Mhe. Spika, zamani miaka ya 1970 kulikuwa na watibabu wa mikarafuu tukiwaita madebeki kwetu sisi. Hawa waliihujumu sana mikarafuu, walikuwa wakiitia dawa sijui ilikuwa ni lami au masinzi. Lakini pia mkarafuu kama umenyauka kidogo tu wanauchimba, yaani wanaung'oa, kumbe ile mikarafuu ilikuwa ni mizima katika utaratibu wa ukulima wa mikarafuu. Lakini hawa walikuwa wanaiondoa kabisa na mikarafuu mingi sana kipindi kile ilitoweka.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aangalie kwa makini sana wataalamu hawa wa mikarafuu wasije wakatuondolea mikarafuu kwa sababu ya utaalamu wao tu wa hivi hivi, wakitoa utaalamu basi uwe ni utaalamu tosha, isijekuwa ni utaalamu wa kubahatisha wakaing'oa mikarafuu baada ya muda tunataka mikarafuu hatuioni kumbe imeondolewa kwa sababu ya utaalamu usiokidhi haja.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 13 kinaeleza hapa kwamba, inakatazwa kwa mtu yeyote kufanya jambo lolote kati ya yafuatayo kwenye mashamba ya karafuu; kuchoma au kutengeneza makaa. Kwa kweli hili ni

jambo muhimu sana, kuchoma moto katika mashamba ya mikarafuu ni tatizo na ni athari kubwa sana. Kuna mikarafuu mingi sana imekufa kwa sababu ya kuchomwa moto.

Lakini Mhe. Spika, sababu nyengine zinazosababisha kuchomwa moto hapa ni wafugaji wa nyuki, wafugaji wengi wa nyuki miongoni mwao wanafuga nyuki katika maeneo ya mashamba ya mikarafuu. Kuna miti tofauti wanategа nyuki wakati wa kufua asali moto ule unapoanguka unaweza ukateketeza shamba zima la mikarafuu. Lakini na wafugaji wa nyuki ni muhimu kwa sababu pia na wao wanapata riziki zao, tufanye nini? Ushauri wangu kwa Shirika hili la *ZSTC* litoe taaluma kwa wafugaji wa nyuki ndani ya mashamba ya mikarafuu, lakini pia wawape vifaa vya kisasa vya kufulia nyuki badala ya kutumia moto, kwa mfano iwe kuna mavazi maalum ya ufuaji wa nyuki ili mikarafuu hii iepukane na kuteketea kwa moto.

Mhe. Spika, nikienda katika kipengele cha 13(3) kinasema hivi, "Mtu yeyote ambaye anakusudia kukata mkarafuu kwa madhumuni ya shughuli za maendeleo atatakiwa kuomba kibali kwa waziri na atapaswa kulipia fidia kwa kila mkarafuu ambapo waziri ataitangaza katika Gazeti la Serikali".

Hili kwa kweli ni zuri, mikarafuu mingi inateketea kwa shughuli za kimaendeleo, tunajenga barabara, tunapitisha mitaro ya maji na mengineyo. Kwa hivyo, ninachosisitiza hapa bei ya karafuu tunaijua ni kubwa na mkarafuu mmoja unaweza ukachumwa zaidi ya pishi 50 za karafuu. Sasa thamani ya mkarafuu ilingane na thamani ya hii fidia itakayotolewa na huyu atakayepeleka maendeleo katika eneo lile, usikatwe mkarafuu ambao thamani yake kwa zao moja la karafuu unaweza ukapata shilingi laki tano, sita au zaidi lakini mwenye mkarafuu huyu akalipwa shilingi elfu 20 au 30. Kwa hivyo, bei ya mkarafuu ilingane na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, kipengele namba 4. Kwa madhumuni ya kusimamia masharti ya kifungu hiki Ofisa yeyote wa Umma anaweza kuingia katika jengo au sehemu kwa ajili ya kuchukua au kukamata mkarafuu unaofikiriwa kuwa umetumika kinyume na masharti ya sheria hii. Mhe. Spika, suala la kuikata mikarafuu kwa kweli suala hili ni baya na mimi nakubaliana nalo moja kwa moja. Kwa sababu hali ya uchumaji tunajua kwamba mkarafuu unaweza ukakatika matawi, lakini kuna watu wanakata matawi ya mikarafuu kwa ajili ya ujenzi au kwa ajili ya mambo mengineyo. Hata hivyo, nimuulize Mhe. Waziri, nini hukumu ya mkarafuu mkavu ambao umekufa katika shamba na mkulima anataka kuutumia mkarafuu ule.

Mhe. Spika, niende katika kipengele cha 18(3). Hapa kuna aina ya vifaa ambavyo anatakiwa mchumaji wa karafuu awe navyo, vifaa vya kuhifadhia

karafuu, vifaa vya kuanikia, vifaa vya kupimia na mahitaji mengine yoyote ambayo Mfuko itayaona yanafaa.

Mhe. Spika, kupatikana kwa vifaa hivi ndio uchumaji wa karafuu na ndio karafuu zenyewe zinapatikana katika hali iliyo nzuri kabisa. Mimi ningeiomba serikali vifaa hivi ijitahidi kwa asilimia mia moja iwatafutie wakulima na wachumaji wa karafuu ili waepukane na tabu ya kwenda huku na kule kutafuta vifaa hivi.

Lakini pia ningemuomba Mhe. Waziri hivi vifaa vya kuanikia karafuu kuna maeneo kama kule Jimbo la Chambani, Kiwani, Pujini, Chonga, Vitongoji, kuna aina nyingi za miti ya mivumo ambayo inasukiwa majamvi. Hivyo watoe taaluma kwa wale watu wanaoishi maeneo yale ili Shirika la *ZSTC* liwashajiishe wasuke majamvi kwa wingi ikiwezekana *ZSTC* inunue majamvi haya ili iwapatie wachumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, nikiendelea niende katika kipengele cha 19(4). Hiki kinasomeka hivi, inakatazwa kwa mtu yeyote isipokuwa shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala au sehemu nyengine yoyote. Kipengele hiki kimesemwa na watu wengi, lakini kwa sababu na mimi ni miongoni mwa waliolelewa na karafuu basi ni wajibu wangu nikitetee kwa nguvu zangu zote. Kwa niaba ya wakulima na wachumaji wa karafuu wa Jimbo la Chambani kipengele hiki kwao ni kero.

Mheshimiwa, kule kwetu sisi Pemba kuna msimu maalum tunauita masika, msimu wa masika hatuufahamu kwetu sisi kama ni muongo tunaufahamu kama ni msimu wa dhiki. Sasa wakulima wengi waliotangulia wanahifadhi karafuu zao mpaka unafika msimu wa mahitaji yao wanauza kiporo, gunia au pishi mbili, pishi nne inategemea namna gani ya mahitaji yake na namna gani ya karafuu alizonazo.

Naliomba Shirika la *ZSTC* iliangalie vizuri hili na wakulima wa karafuu wapangiwe muda. Wenzangu wengi walisema wapangiwe muda, lakini mimi nataka niseme kwamba wapangiwe muda usiopungua mwaka mmoja ndani ya zao lile, au wapangiwe muda kutoka zao mpaka zao iwe karafuu hizi wameshaziuza. Lakini kuziuza karafuu hizi papo kwa papo, mbichi mbichi hili litakuwa ni tatizo gumu kwa wananchi wanyonge ambao wamezowea kuuza karafuu mbili mbili kwa mujibu wa mahitaji yao.

Mhe. Spika, nikiacha kipengele hicho niende katika Sehemu ya Nne kifungu cha 20(2). Benki itakuwa na majukumu ya kusimamia fedha zilizotengwa kwa ajili ya wakulima wa karafuu na yanayofuatia. Lengo langu kubwa hapa ninalokusudia kuzungumza Mhe. Spika, kwamba benki itakuwa inaweka

fedha kwa ajili ya maslahi ya wakulima na wachumaji wa karafuu. Ninachozungumza hapa ni kimoja tu, kwamba fedha hizi zitumike pasiwe na ubaguzi wa aina yoyote katika upatikanaji wa fedha hizi. Baada ya mtu kukamilisha masharti yanayostahiki kwamba ni mkulima wa karafuu, mchumaji au mkodishwaji basi asiangaliwe rangi yake, sura yake, chama chake, mji wake, aangaliwe tu kwamba yeye ni mhudumu wa karafuu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kuna suala ambalo nataka nimuulize Mhe. Waziri. Kuna mashamba ya mikarafuu ambayo imepandwa miti mingine ya biashara kama vile mipira, kule Pemba Kaskazini, mfano Maziwani. Je, tuliite vipi shamba lile ni la mipira au shamba la mikarafuu? Nini tunahitaji, tunahitaji mipira au tunahitaji mikarafuu? Tufanye nini katika kuokoa aidha mpira au kuokoa mkarafuu? Kuna mikarafuu mizuri yenye thamani kubwa lakini imedhikika kwa ajili ya upandaji wa mipira.

Mwisho nizungumzie kuhusiana na miundombinu inayofikiwa katika maeneo ya mikarafuu. Alisema Mhe. Abdalla Moh'd Ali, hapa inasadikiwa kwamba wilaya ya Mkoani inakuwa na uzalishaji mwingi wa karafuu kisiwani Pemba kuliko wilaya nyengine.

Lakini pia, kuna eneo moja maarufu sana Ngomeni. Eneo hili lina mikarafuu mingi na takribani ya wilaya yetu inatunza mikarafuu katika eneo la Ngomeni. Lakini miundo mbinu ya barabara ni michafu, migumu na mibaya sana. Pamoja na mswada huu na kwa umuhimu wa zao la karafuu na kwa umuhimu wa Ngomeni kulivyo tunaomba bila ya kuchelewa mfuko huu ushughulikie barabara ya Ngomeni angalau kwa kiwango cha kifusi kwa hatua ya kwanza na hatua ya pili ifuate baadae.

Mhe. Spika, Ngomeni kwa kweli kuliacha eneo lile kuwa halipitiki kwa gari wakati wowote, kwa kweli si kuwatendea haki watu wa Ngomeni. Kwa sababu asilimia kubwa ya karafuu zinatoka katika mji ule wa Ngomeni.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda wako na natoa pongezi zangu kwa shirika hili kwa kutuletea mswada huu muhimu. Nasema nitaunga mkono pale ambapo nitapata ufafanuzi juu ya yale ambayo nimeomba ufafanuzi. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi Magharibi haya kupata nafasi ya kutoa mawazo yangu kuhusu mswada huu ulio mbele yetu, ambao ni mswada muhimu wenye lengo la kulinda na kuokoa mikarafuu

Kabla ya maelezo yangu Mhe. Spika, nikushukuru na nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wote kwa ujumla kwa kazi kubwa waliofanya kwenye kutayarisha mswada huu.

Mhe. Spika, karafuu zinatokana na mkarafuu, lakini Mhe. Waziri, yeye yake ni karafuu, mkarafuu si wa kwake ni wa mtu wa kilimo. Sasa sijui yeye na Wizara ya Kilimo wanaukaribu gani wa kuhudumia mkarafuu ili yeye apate hiyo karafuu. Mhe. Spika, isijekuwa yeye anataka maziwa tu, lakini ng'ombe kumchunga na kumlisha ikawa hamshughulikii. Sasa maziwa anayoyahitaji yatakuwa machache.

Kwa hivyo, ningetaka kujua kuna uhusiano gani baina ya mmiliki wa mkarafuu ukiacha mwananchi yaani Wazira ya Kilimo ambao mkarafuu ni zao la kilimo. Lakini karafuu ni zao la biashara na ndio maana likaingia katika mswada huu.

Mhe. Spika, takribani wachangiaji wote wamechangia maeneo ambayo na mimi nilikusudia nichangie. Sasa kurudia mara kwa mara yale kwa yale ambayo yameshasemwa na wengi, itakuwa si mzuri. Lakini kwa kuwa hii nafasi nimeiomba nimeipata nami nitalazimika kusema machache sana juu ya mswada huu.

Mhe. Spika, nianze mwisho kidogo kabla sijaja mwanzo nilipokusudia. Mhe. Spika, juu ya uhifadhi wa karafuu baada ya kuchumwa. Mimi mwaka niliofanya mtihani wa kuingia kidato cha kwanza, baada ya kutoka matokeo nilimwambia babu yangu kuwa nimefaulu na nimechaguliwa kwenda kusoma Vitongoji. Babu yangu aliingia kwenye kijighala chake akapima pishi tano ya karafuu kavu akaenda kuziuza. Kama babu angelikuwa hana akiba ya karafuu, basi mimi kidato cha kwanza nisingekwenda.

Kwa hivyo, suala la kuhifadhi karafuu wakulima baada ya kuchuma lina umuhimu wake katika mila zetu na desturi zetu za wachumaji wa karafuu. Sasa Mhe. Spika, hili mimi nilikuwa naliona ni jambo muhimu la kulizungumza.

Mhe. Spika, katika majimbo yetu wameanzisha vitalu vya kupanda karafuu ili hatimae wanawauzia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Kilimo hatimae wanawapa watu mikarafuu ile ili waweze kuendeleza mashamba ya mikarafuu.

Mhe. Spika, ningeliomba na wizara hii iwaunge mkono hizi jumuiya ambazo zina vitalu vya mikarafuu. Kwa sababu karafuu inatokana na mikarafuu. Na sasa watu wengi wameshajihika hata katika jimbo langu la Mtambile

kuanzisha vitalu vya miche ya mikarafuu. Ningeomba siku moja nimkaguze katika jimbo langu ili waweze kuombea msaada wa kujiendeleza kwa sababu wanasaidia kukuza uchumi wa taifa.

Mhe. Spika, yameelezwa mengi katika msimu wa uchumaji karafuu. Karafuu wakati wake wa kuvuna takribani kuanzia mwenye shamba, mchumaji, muanikaji na muokotaji hawa wote kila mmoja ananufaika na karafuu. Lakini baada ya karafuu kupata hii bei iliyopo, baadhi ya wamiliki wa mashamba ya karafuu wamebadilika hawako tayari kuona kama kuna mchumaji juu anachuma. Lakini ujumla wake uokotaji wa karafuu ni jambo zuri na linawasaidia watu kuongeza kipato chao. Mhe. Spika, katika kazi ngumu usiku au jioni ni ya kuhesabu shada moja moja na kulichambua, kuchuma unachuma moja moja unaingia katika hatari na usiku unakaa kitako na unachambua.

Mhe. Spika, pale inapotokea bahati mbaya yule mchumaji wa karafuu akaanguka, basi naomba ile fidia ya miaka ya 70-80 ningeomba irudishwe kwa huyu alieanguka mkarafuu ili iwe kama msaada wa kumsaidia katika maisha yake, kwa sababu wengine wanakuwa walemavu wa kudumu.
Mhe. Spika, mkarafuu unaishi unazaa na unakufa, sasa sheria hii haijaonesha hukumu ya mkarafuu uliokufa. Hofu yangu mtu anaweza kuja kukata mkarafuu mkavu akadaiwa kulipa milioni tatu alizokuwa hanazo na akenda jela ambapo hakuwezi.

Mhe. Spika, naunga mkono moja kwa moja kuchukuwa hatua kama zilizotajwa katika mswada huu. Naunga mkono hatua ambazo zitachukuliwa kwa mtu ambae atakata mkarafuu mbichi ambao bado una uwezo wa kuzaa, hatua hizi mimi naziunga mkono.

Mhe. Spika, sasa karafuu imepata bei nzuri na hadhi. Mhe. Spika, sasa kuna kunyang'anywa mashamba ya mikarafuu, kama mtu aliepewa mkarafuu mwaka juzi ulikuwa si wake, lakini mwaka huu anakwambia huu ni mkarafuu wangu, kwa sababu tu ya ile thamani ya karafuu.

Mhe. Spika, inaonesha kwamba kuna kitu katika mkarafuu kwa sababu mambo yote wameyawacha, lakini karafuu wamekataa kata kata kuitoa kuna nini ndani ya karafuu? Karafuu kama ni zao la biashara kwa nini serikali isiweka mfumo tu wa kutoza kodi kama walivyotoza kodi kwa mambo mengine na hii biashara ikawa huru kama walivyoziachia biashara nyengine.
Mhe. Spika, serikali ingelitilia mkazo juu ya kuimarisha mashamba na kuwaelimisha wakulima wa karafuu juu ya ukulima bora wa zao hili. Lakini hatimae hii biashara wakaiwacha huru kama walivyoachia biashara nyengine.

Mhe. Spika, sheria hii iliyotunga ni nzuri kama itafanyakazi, itabidi na sisi tukawaelimishe wananchi katika majimbo yetu juu ya umuhimu wa kutokwenda kinyume na sheria hii. Vyenginevyo watakutwa na madhara makubwa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema sitosema sana kwa sababu mengi niliyopanga kuyasema yameshasemwa na walionitangulia. Kwa hivyo, sitaki nipoteze muda wako mwingi kwa kurudia yale ambayo yamezungumzwa. Ahsante sana kwa kupata nafasi hii.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi usiku wa leo nikaweza kutoa mchango wangu juu ya mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu namba 11 ya mwaka 1985 na kuweka sheria mpya ya Maendeleo ya Karafuu na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika,niseme tu kwamba zao la karafuu ni zao muhimu sana. Lakini katika miaka iliyopita tunajua kwamba ilifanyakazi kubwa sana uzalishaji ulikuwa mkubwa sana na lilikuwa ni zao kuu la taifa. Tani ambazo zilikuwa zinazalishwa miaka mingi ya nyuma, zilikuwa ni nyingi zaidi kuliko hivi sasa.

Lakini bado tunasema kwamba zao hili la karafuu ni zao la kitaifa na hatimae liliendelea kuzoofika kidogo kidogo mpaka kufikia hali ya sasa. Lakini nashukuru kwamba Wizara hii ya Biasharan imeweza kufahamu majukumu yake ya kulisimamia zao hili ambalo hivi sasa linaanza kuibuka na kuingia katika sura mpya.

Mhe. Spika, zao hili limewekewa mkakati maalum wa kitaifa. Zamani tulikuwa tunazalisha karafuu kwa wingi na zinachukuliwa na walanguzi. *ZSTC* wanauza karafuu bila ya mpango jambo ambalo kwa kitaifa huwezi kuleta tija. Mhe. Spika, Zanzibar ilikuwa haitajiki katika mataifa kuwa hili ni zao la Zanzibar. Wanaotajika katika zao la karafuu ni watu wa Kenya, ndio wao walijinasibisha kuwa wao zao hili ni lao. Wakati zao hili lilikuwa letu sisi Wazanzibari. Lakini walanguzi ndio waliokuwa wakizisafirisha kwenda Kenya.

Mhe. Spika, niipongeze wizara hii pamoja na waziri na watendaji wake wote na mrajisi wa biashara, hawa kwa kitu kimoja wamekaa kitako kufikiria kwamba biashara hii tuifunge ili mtu mwengine yoyote asiweze kujinasibisha kwamba zao hili ni lake yeye. Badala ya kutajwa Zanzibar wanatajwa watu wengine, sasa hilo suala limekwisha. Nafikiri tutaweza kuuza kwa sifa yetu,

hakuna mtu ambaye anaweza kutia mkono katika zao letu la karafuu. Kwa hivyo, na mimi niwapongeze na niwashukuru.

Mswada huu tulionao leo usingekuja ni kwa sababu ya utambulisho. Suala hili ni muhimu sana. Kwa hivyo, hali hii ndio iliyofanya kuwepo kwa sheria hii ambayo tunayo leo. Sote tunafahamu Mhe. Spika, kwamba zao la karafuu ni zao ambalo linanufaisha taifa letu na sisi tumefaidika kwa miaka mingi sana. Maendeleo ya nchi hii awali yake yamepatikana kwa karafuu.

Kwa hivyo, serikali bado inayo nia ya kuliendeleza ingawa sasa hivi limekuwa la pili, la kwanza ni utalii. Lakini tunashukuru hivi sasa jitihada kubwa za wizara hii kuhakikisha kwamba zao linakuja tena kama siku za awali lilivyokuwa.

Kwa hivyo, kuwepo kwa sheria hii ni suala muhimu na kwa sababu sheria hizi zinataka kuwa madhubuti kulinda zao hili la karafuu na hii sheria itaweza kunufaisha sisi wakulima na taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, mimi nataka nirudi katika mswada wetu tulionao. Nataka nianzie kwenye kifungu cha 18 cha mswada huu. Hapa kinazungumzia msimu wa uchumaji karafuu. Kutakuwa na msimu wa zao la mwaka na msimu wa zao la vuli. Kama ni msimu wa uchumaji wa karafuu wa kila mwaka hii sawa.

Karafuu zinakuja kwa msimu wake, hazizai kila siku, ukiona mkarafuu unazaa kila siku ni ishara ya kifo na inafika wakati mkarafuu hata yale majani hayaonekani, kinachoonekana ni mashada ya karafuu. Kwa hivyo, hiyo ni salamu za kusema kwamba ule mkarafuu unakufa.

Lakini kama tutapata mvua za kutosha na hali ya hewa itakuwa nzuri na uzazi wake utakwenda kwa kipindi kama hivyo inavyozungumzwa kwenye vuli katika mwaka. Basi tunahakikisha kwamba zao litakuwa zuri na karafuu tutapata kwa wingi. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba hii ni sawa karafuu zitakwenda kwa msingi mzuri na tunafaidika katika hilo.

Lakini kila mmiliki na mkodishwaji mikarafuu ambaye anakusudia kuchuma na kuanika. Wakati wa msimu wa uchumaji karafuu, atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo vilivyothibitishwa na mamlaka. Sasa mimi hapa katika sehemu hii nimeona Mhe. Waziri, ni nzuri. Haya mliyoyataja chini yake ya kusema kwamba kila mtu atatakiwa na vifaa vya kuhifadhia karafuu, kuanikia na mahitaji mengine ambayo yanahusu habari ya karafuu yote kwa jumla. Lakini hawa watu vitu hivi hawana, mimi ningelisema hapa itakuwa ni jukumu la *ZSTC* kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinapatika kwa wakati. Kwa sababu karafuu bila ya kuwa na jamvi haiwezekani, karafuu bila ya kuwa na gunia la

kuhifadhia karafuu haiwezekani na ukiziweka chini kwenye sakafu zinapata unyevu na hasa ikiwa karafuu zenyewe hazikukauka.

Kwa hivyo, ni muhimu na suala la msingi kabisa kuhakikisha kwamba *ZSTC* inaagizia vifaa hivi kwa ukamilifu na wananchi watakwenda kununua kama kawaida yao.

Kwa hivyo, ningefikiria tu isiwe dhamana wao katika *passage* inavyozungumza kwamba wao ni dhamana. Wao wasiwe dhamana, dhamana iwe *ZSTC* kwa sababu wao ni shirika na shirika ni serikali. Kwa hivyo, liagizie vifaa kwa ukamilifu na viweze kuletwa kwa wakati wake.
Halafu kifungu cha 4 Mhe. Spika, kila mkulima mmiliki au mkodishaji wa mikarafuu atahakikisha kwamba karafuu zake ziko katika hali nzuri na hazijaharibika hapa. Mhe. Spika, hapa hatuna dhamana ya karafuu.

Kwanza karafuu maumbile yake ni mti au ni mmea ambao unaleta joto. Na miti hii ya mikarafuu wakati wa uzazi wake joto linakuwa jingi sana. Na ikileta joto kwa mzunguko wake wa hali ya hewa ni lazima mvua itakuwepo. Na siku zote katika uchumaji wa karafuu mvua zinakuwepo kwa wingi na huna namna ya kusema kuzizuia mvua. Kwa sababu ya joto la karafuu lina *high temperature* na ndio maana ikaambiwa hii karafuu ya Zanzibar ni *first class type*, ni *best* katika karafuu zote za duniani.

Hakuna mtu duniani au mwenye mashamba ya mikarafuu anaweza kupata *first class* ya karafuu zaidi ya Zanzibar, kwa uzuri wake, kwa utamu wake na mataifa wanaipenda kwa sababu inazalisha mambo mengi. Inatumiwa katika chakula, madawa, rangi za midomo, kuna mambo mengi sana. Kwa hivyo, ni zao la Zanzibar pekee ambalo lina sifa katika ulimwengu. Sasa lazima sisi Wazanzibari tulihifadhi, tulidumishe na tuliweke katika hali nzuri ili liweze kutusaidia.

Kwa hivyo, suala la kuharibika ni pale kunapokuwa na jua kali karafuu zitakuwa nzuri, tunasema *first quality* ya kwanza hiyo. Lakini unapata *grade* ya pili na unapata *grade* ya mwisho ambayo ni mbaya zaidi. Hizi zote zinanunuliwa, *grade* ya kwanza inanunuliwa, *grade* ya pili inanunuliwa na hizo mbaya zote zinanunuliwa.

Lakini cha msingi mimi ninachokiona hapa Mhe. Waziri, nataka nitoeushauri. Unajua hili suala ni la kitaifa na hatutaki kwa sababu watu wanakodi mashamba kwa gharama kubwa sana, inapofika wakati wa mvua nyingi, sasa hapa taifa litoe msaada kwenye suala hili. Wakulima hapa wamekodi mashamba, machungu kwa machungu ya mikarafuu yapo pale mvua zinapiga karafuu zipo uwanjani mpaka karafuu zinabadilika rangi yake. Na karafuu

ikipigwa na mvua inavimba, na ikivimba haiji katika *first quality,* karafuu ile ikivimba inakuwa ni mpeta, inapokuwa mpeta bei inaanguka.

Kwa hivyo, mimi hapa nafikiri kama kutakuwa na *system* maalum ya kuwasaidia wakulima. Unajua kuna suala hili la tumbaku wanayolima wananchi, ile inatengenezwa kienyeji kutiwa katika *oven,* majani yale ya tumbaku yanakauka kwa lile joto, yakishakauka wana-*pack,* wanauza majani wenyewe wanaisarifu wanavyotaka.

Sasa kwa nini hili zao la karafuu hatuweki *system* ambayo itaweza kuwasaidia wakulima watakapokuwa na karafuu zao siku za mvua pawe na maeneo maalum kila mahala ambapo uzalishaji unakuwa mkubwa tukaweka nyumba yetu moja nzuri ambayo inaweza kufanya *system* ya kuwasaidia wakulima wakakausha karafuu zao. Wakati wa jua tutategemea jua, lakini wakati wa mvua zao linapotea na sisi mapato tunayakosa. Kwa hivyo, mimi hapo ningemshauri Mhe. Waziri, angalau aweke *system* ambayo itaweza kutusaidia.

Halafu Mhe. Spika, kila mkulima, mmiliki, mkodishwaji wa mkarafuu atazianika karafuu kwa kutumia jua na vifaa vinavyothibitishwa kwa kuanikia. Hapa vifaa ni yale majamvi. Hivyo, tunasema *ZSTC* ijitahidi.

Mhe. Spika, jengine mtu yeyote ambaye atakusudia kuhamisha karafuu kavu au mbichi, makonyo au karafuu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine ni kuomba hii, ni taratibu zinavyowekwa. Hii *system* imezoeleka ni ya muda mrefu. Tunakubali kwamba kuhamisha karafuu kutoka eneo moja kwenda eneo jengine, hili ni suala linakubalika. Na huwezi kuichukua ovyo ovyo kwa sababu ile ni *product* ya kitaifa. Pengine *product* ile unaichukua unaipeleka pahala pengine mtu kaiba ile. Sasa kuthibitisha kwamba mali ile unaichukua mahala fulani kuipeleka mahala Fulani, hakuna ubaya kupata kitambulisho cha kuhamisha ile karafuu. Hili ni suala la kawaida, ile ni mali ya kitaifa hatuwezi kuiachia ikapotea kiholela.

Kwa hivyo, naona hapa suala la msingi ila tu labda utaratibu uwekwe ni nani na nani watakuwa wanahusika. Hapa imesema ni Sheha, lakini kama pia patawekwa na watu wengine katika vituo vyao, Sheha hayupo, lakini watu wa Kilimo wapo wenyewe wapewe kibali ili kuondosha ule usumbufu kwa wananchi hasa katika kipindi kile ambacho ni cha uzalishaji.

Jambo jengine Mhe. Spika, nimeliona mimi katika kifungu cha 18 (2) kinasema; "Kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hichi hakitotumika kwa wachumaji wa karafuu ambao watakuwa katika majukumu yao ya kawaida kurejea majumbani mwao kutoka katika sehemu za uchumaji wa karafuu"

Hapa Mheshimiwa, nafikiri unakusudia wale watu, lakini mimi *particularly* hapa hamu yangu ilikuwa katika *paragraph* hii tuwaelezee wale ambao wanakwenda kuchuma karafuu na kurudi na karafuu. Tatizo liliopo katika maeneo yetu ni kubwa sana, mwenye mali yupo mtaa huu huku, karafuu zinachumwa upande huu, mchumaji sie yule tajiri, mchumaji ni mtu wa kawaida, anakwenda kuzichuma halafu inabidi azichukue ndani ya polo lake azipeleke kule kwa yule tajiri akazinyambue.

Sasa matatizo yanayojitokeza ni kwamba wanapochukua karafuu hizi kutoka eneo moja kwenda eneo jengine, Sheha na askari wanawakamata njiani. Sasa nafikiri hapa hatukuweka kifungu cha kumlinda huyu mchukuaji wa karafuu aliyezichuma kutoka eneo lile kulipeleka kwa huyo. Kwa sababu wale hawana kambi, ni watu ambao vijana wanawake na wanaume wanakwenda wanachuma wanazipeleka kwa yule tajiri wao, kule ndio zilikuwa zinaanikwa.

Kwa usahihi na ushahidi nilionao Mhe. Waziri, Sheha wetu mmoja aliyepo Kifundi anazuia karafuu pale, anawaambia anika hapa hapa. Ni haki hiyo? Yule kishazichuma anataka pesa zake apate anamwambia zianike hapa hapa. Kwa hivyo, nafikiri hapa kidogo na huyu mbebaji wa karafuu hatukumuwekea sheria hapa ya kwamba huyu aruhusike ila ieleweke tu lile eneo analopeleka zile karafuu. Lakini asizuiwe njiani, maana yake anazuiwa huyu, anamwambia chambua karafuu zako, anika hapa hapa, tutazipima, tutazipasisha hapa hapa. Sasa yule anataka kutumia saa ile, yule Sheha hana pesa za kumpa. Kwa hiyo, kamlaza na njaa. Mimi nafikiri tumuwekee utaratibu huyu mbebaji wa hizi karafuu.

Mhe. Spika, kuna sehemu hii ya nne ya usimamizi wa mfuko. Kwa madhumuni ya kifungu 8 cha sheria hii, bodi itazingatia taratibu za ushindani na itachagua benki kwa ajili ya utoaji wa huduma na usimamizi wa fedha, mifuko ambayo inakuja hapa chini. Kusimamia fedha zilizotengwa kwa ajili ya wakulima wa karafuu, utoaji na urejeshaji wa fedha na kazi nyengine yoyote ambayo bodi itaona inafaa.

Mhe. Spika, kifungu hichi tatizo lake ni moja tu, haya yote uliyo-*draft* hapa yapo sawasawa, lakini *there is something missing*. Hapa hili suala la utoaji wa fedha kwa yule ambaye anakopeshwa katika kifungu hichi hakijaeleza masharti ya mkopaji. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri, kwa niaba ya Mhe. Spika, kwamba hapa huyu mkopaji ana masharti gani? *What conditions* ambayo yeye katika kukopa zile pesa kwamba yatakuwa haya, haya.

Sasa huu mtandiko uwepo wa kuonesha huyu mtu ambaye anakopa fedha ile, ile fedha inakopeshwa na inataka kurudishwa, lakini mwenye kukopa na kulipa hajajulikana *background* yake atailipa vipi, kwa masharti gani.Na hii

fedha unayokopa ni fedha ya kiwango gani. Kwa hivyo, hapa mimi nafikiri kidogo mtandiko tuuweke vizuri na mambo yetu yatakuwa mazuri.

Kwa hivyo, hapa ninachokiomba mimi katika mswada mzima huu tulionao tunahitaji kutoa elimu kwa wakulima wetu. Tangu ulivyoanza mswada huu mpaka tukamalizia wasije wakaacha kitu kuwafahamisha wananchi kwa kutoa elimu kwa usahihi na kuonesha kuanzia mwanzo mpaka kufikia kifungo ambao watu wanaochuma karafuu itawafika haya. Kuna adhabu mbele huko inakuja.

Kwa hivyo, katika kuisoma hii kuelimisha wananchi, tunahitaji kuwaelimisha tangu mwanzo mpaka mwisho umuhimu wa karafuu zetu za kitaifa, ulinzi ambao tunahitaji kuweka na mikopo ambayo sisi tunawasaidia wao kuweza kuirudisha mikopo kwa wakati. Hili ni jambo la msingi. Kwa hivyo, taaluma inahitajika kwa wakulima wetu wote. Tena isichelewe kwa sababu zao la karafuu sasa hivi lipo.

Mhe. Spika, nakushukuru na naendelea tena kwa mchango mwengine sehemu ya tano kuhusiana na wakulima wa karafuu, wauzaji, shirika, wadau wengine wa karafuu kama itakavyoelezwa katika kanuni itakayotungwa chini ya sheria hii.

Mhe. Spika, hapa kuna kasoro ya maandishi kidogo nataka nitoe ushauri. Ushauri wangu katika kifungu hichi cha 5, masharti ya fedha nipo hapa kwa hawa wauzaji. Hapa hatuja-*categorize* hawa wauzaji. Kwa sababu katika kuuza karafuu nani anauza karafuu. Mimi naweza kuwa nina shamba, lakini siendi mimi kuuza karafuu, pengine namtuma mtoto wangu akauze karafuu au namtafuta jirani tu ee bwana kaniuzie karafuu zangu.

Kibibi kikongwe hakiwezi kwenda kule, lakini karafuu anazo kavu, mwanangu njoo ukaniuzie. Yule anakwenda kuuza na pesa atapewa. Lakini sasa hapa katika mauzaji nafikiri tuweke lugha nyengine itakayoweza kuwasaidia. Sisi tunahitaji fedha, tunahitaji makusanyo kutoka kwao, kwa mkulima, kwa muuzaji na wadau wengine. Lakini sasa hapa kwa huyu muuzaji tunasema nini, aina gani ya muuzaji anahitaji kutoa kodi. Ni yule aliyepewa dhamana akauze tu kule? Kwa sababu huku wewe utakuwa tayari mkulima umeshamtoza mwenye shamba na huyu aliyekodi shamba la yule bwana atakuwa katoa kipato. Lakini sasa sisi hapa wawili hatuuzi karafuu, mimi nitampa mtu akaziuze zile karafuu kule *ZSTC,* yule ndie atakayepokea pesa. Hapa utaratibu utakuwa vipi? Hilo la kwanza.

Lakini la pili, nataka tuweke katika akiba ya mazungumzo kwamba wauzaji hawa kila mmoja na hali yake ya mauzaji, kuna wanaouza gunia 10, 20, kuna

wale watakaouza gunia 5, kuna wale watakaouza gunia 2, kuna wale watakaouza pishi moja ya karafuu au kibaba cha karafuu na vyote vinanunuliwa. Je, hawa katika suala la kutoa huo mchango watatoa vipi mchango wao kusaidia zao la karafuu. Naomba Mhe. Waziri, uje utusaidie hapa kwa hawa wauzaji tunawaweka katika *category* ngapi?

Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunigaia nafasi hii, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kazi nzuri ya leo na mpaka sasa tumemaliza kwa siku ya leo na kesho tutaendelea kwa kuwasikiliza Waheshimiwa Wajumbe ambao tayari wamepeleka majina. Nao ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Salma Mohamed Ali.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa niahirishe kikao hichi hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 24/01/2014 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 24/01/2014 saa 3:00 asubuhi)